

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Hamsini na Nne – Tarehe 20Juni, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Moja, leo ni Kikao cha Hamsini na Nne. Katibu.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na litaulizwa na Mbunge wa Nyamagana Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula. Mheshimiwa Mabula.

Na. 457

Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Nyamagana

MHE. STANSLAUS S. MABULA aliuliza:-

Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Nyamagana linalojengwa katika Kata ya Mkolani limechukua zaidi ya miaka minne sasa bila kukamilika:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(a) Je, Serikali haioni kuwa na miradi isiyokamilika kwa wakati kunarudisha nyuma maendeleo;

(b) Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha za kukamilsha jengo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, lenye vipengele (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ujenzi wa jengo la Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana ulioanza mwaka wa fedha 2008/2009 umechukua muda mrefu. Sababu kubwa ya kuchelewa kukamilika kwa ujenzi huo ni changamoto ya upatikanaji wa fedha za ruzuku ya maendeleo. Hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 1.34 kati ya shilingi bilioni 1.84 zilizokuwa zinahitajika zimetolewa na kutumika katika kujenga boma lenye vyumba 23 vya ofisi, kumbi mbili, mgahawa, chumba cha kuhifadhiya nyaraka, vyoo, kuezeka jengo lote, kupiga plasta, kuweka milango, vigae, kupaka rangi, kuweka dari, kufunga milango na madirisha na mfumo wa maji safi na maji taka.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kumaliza jengo hilo, jumla ya shilingi milioni 420 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 ili kumalizia mfumo wa usalama wa jengo ikiwemo zimamoto, mfumo wa umeme, tanki la maji na uzio. Kwa maana hiyo, ujenzi wa jengo hilo unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2018/2019.

SPIKA: Mheshimiwa Mabula, nilikuona.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nataka kuuliza jambo moja kwamba majengo haya ya Serikali yanachukua muda mrefu kukamilika na

matokeo yake yanagharimu fedha nyingi zaidi ambapo yangejengwa na kukamilika kwa wakati yangesaidia sana matumizi ya fedha za Serikali kutumika kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na Serikali na jitihada zake kubwa, ni miaka 10 leo. Mwaka ujao wa fedha Mheshimiwa Waziri anatauhidi kwamba jengo hili litakamilika. Naomba sana tufanye jitihada hiyo ili fedha hizi ziletwe na jengo hili likamiliike. Hii itachangia hata ukuaji wa uchumi kwenye lile eneo ambalo Jengo la Mkuu wa Wilaya limejengwa. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Joseph Kakunda, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mabula na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, pamoja na mikoa yote na wilaya zote, tumepitisha hapa Bungeni shilingi bilioni 53 kwa ajili ya kujenga majengo ya Halmashauri na tumepitisha hapa shilingi bilioni 80 kwa ajili ya bajeti za maendeleo ya mikoa. Hizi fedha nataka niwahakikishie kwamba Serikali inaendelea kuwa *stable* kabisa katika masuala ya ukusanyaji wa fedha, fedha zitapelekwa, wala asiwe na wasiwasi wowote.

SPIKA: Tunaendelea na Swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

Na. 458

**Kupandishwa Hadhi Kituo cha Afya Mlandizi
kuwa Hospitali ya Wilaya**

MHE. HAWA M. CHAKOMA aliuliza:-

Kituo cha Afya Mlandizi kimetimiza vigezo vyote vya kuwa Hospitali ya Wilaya:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini sasa Serikali itapandisha hadhi Kituo hicho kuwa Hospitali ya Wilaya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Malandizi bado hakijakidhi vigezo vya kukifanya kiwe Hospitali ya Wilaya. Hata hivyo, Serikali haina mpango wa kukipandisha hadhi Kituo hicho kuwa Hospitali ya Wilaya. Serikali imeamua Kituo hicho kiendelee kutoa huduma kama Kituo cha Afya. Hata hivyo, Serikali illiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha itenye eneo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshatenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.5 katika mwaka wa 2018/2019 kwa ajili ya ujenzi huo. Pia Halmashauri imeshatenga eneo la ekari 32 lilitopo katika Kitongoji cha Disunyala, zamaani lilikuwa shamba la *United Farming Cooperation* kwa ajili ya ujenzi huo.

SPIKA: Mheshimiwa Hawa ameridhika.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Spika, hapana.

SPIKA: Wamesema hawana mpango wa kujenga Mlandizi.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Bado tuna maombi.

SPIKA: Endelea Mheshimiwa, swalii.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali

mawili madogo ya nyongeza. Kinachoendelea kwa sasa katika Kituo cha Afya cha Mlandizi ni kuelemewa na lundo la wagonjwa, hususan upande wa afya ya uzazi. Ndani ya mwezi mmoja kuna wanawake zaidi ya 250 wanaojifungua. Idadi hii ni mara tatu ya walengwa wa Kituo hiko cha Afya cha Mlandizi, kitu ambacho kinapelekeea kituo chetu kuwa na mahitaji makubwa ya matumizi ya dawa, vifaa tiba na huduma za kujifungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, sasa napenda kujua, wakati huu ambaa hatuna Hospitali ya Wilaya na Serikali haina mpango wa kujenga Hospitali hiyo ya Wilaya: Je, Serikali itakuwa tayari kutupatia fungu maalum la fedha kila mwaka kwa ajili ya huduma hii ya afya ya uzazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kufuatia ongezeko hilo la wagonjwa kuwa mara tatu ya walengwa wa Kituo hicho cha Afya na kupelekeea kituo chetu kuwa na deni kubwa takriban shilingi milioni 83 linalojumuisha matumizi ya dawa, vifaatiba, huduma ya uzazi na huduma nyingine, nangependa kujua, sasa Serikali itatusaidiaje ku-clear deni hilo, ukizingatia idadi hiyo ya fedha au kiasi hicho cha fedha ni mara mibili, tatu, nne mpaka tano ya mapato yote ya Kituo cha Afya cha Mlandizi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana kwa maswali hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri, wanajifungua siyo chini ya akinamama kumi kwa siku katika Kituo hicho cha Afya.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE): Mheshimiwa nakushukuru. Katika jibu langu la msingi, nimesema kwamba Serikali imeona uhitaji wa kujenga Hospitali ya Wilaya na tayari katika bajeti ya 2018/2019 tumetenga shilingi bilioni 1.5, ni kwa sababu tunatambua umuhimu na uhitaji mkubwa sana wa wananchi kwa suala zima la Afya. Kwa hiyo, tuko tayari na ndio maana tunajua kabisa kuna kuelemewa ndio maana tunaenda kujenga Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, anauliza, tunafanya je katika kuwasaidia deni la jumla kama shilingi milioni 80? Ni vizuri kwanza tukajua chimbuko la deni hili nini na tukikaa baada ya kipindi cha maswali na majibu, tuje tatizo ni nini ili tuweze kusaidiana ili wananchi waendelee kupata huduma, lakini wakiwa wamevuta subira, Serikali yao ya CCM inawajali na ndiyo maana tunaenda kujenga Hospitali ya Wilaya.

SPIKA: Nilikuona Mwenyekiti wa PAC.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nataka niombe tu kwamba Kituo cha Afya cha Kata ya Vunta, Tarafa ya Mamba Vunta kimepandishwa hadhi kuwa Kituo cha Afya takriban miaka 10 iliyopita, lakini hakijafunguliwa rasmi kutokana na kwamba kilikuwa hakijapata ukarabati unaofaa.

Mheshimiwa Spika, pamoja kwamba tunashukuru Serikali ilipeleka *Ambulance*, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba ni lini Kituo hiki kitafunguliwa rasmi ili kitambulikane kwamba kweli ni Kituo cha Afya cha Tarafa ya Mamba Vunta yenye kata tano?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Kaboyoka.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kwa sababu kuna sifa ya zahanati kupanda kutoka zahanati kuwa kituo cha afya, naye mwenyewe amekiri, ingekuwa vizuri baada ya kutembelea eneo hilo ambalo mimi nipo tayari, ili tukaone kama kweli inakidhi haja ya kuwa Kituo cha Afya itakuwa ni furaha kwangu mie kuhakikisha kwamba inapata hadhi ya kuwa Kituo cha Afya kwa mujibu wa kukidhi vigezo ambavyo vimewekwa ili kiweze kuwa Kituo cha Afya.

MBUNGE FULANI: Kimeshapandishwa.

SPIKA: Kimeshapandishwa ila anachotaka ni suala la uzinduzi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Kimeshapandishwa? Kama tayari kimeshapandishwa, maana yake kuna baadhi ya taratibu ambazo hazijafuatwa. Naomba tukishamaliza hiki kipindi cha maswali na majibu, nipaye fursa ili tuweze kuongea na *DMO* tujue hasa nini ambacho kimetokea kama tayari kimeshapandishwa, lakini hakiwi *treated* kama Kituo cha Afya.

SPIKA: Ahsante sana. Swali la Mheshimiwa Edwin Sannda, Mbunge wa Kondoaa Mjini, uliza swali lako, tafadhali Mheshimiwa.

Na. 459

Hitaji la *Mobile Clinic* – Jimbo la Kondoaa Mjini

MHE. EDWIN M. SANNDA aliuliza:-

Wananchi wa Vijiji vya Hurumbi, Dumi na Chandimo Kata ya Serya, Ausia, Mulua na Guluma (Suruke) pamoja na Hachwi, Kutumo na Chora (Kolo) katika Jimbo la Kondoaa Mjini, kijirografia wana changamoto kubwa ya huduma muhimu za afya ambapo wanalahimika kufuata huduma hizo katika zahanati za jirani au hospitali ya mjini:-

Je, ni lini Serikali itatupatia *Mobile Clinic* kutatua changamoto hii?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, Mbunge wa Kondoaa Mjini, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ni kweli wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa wanahitaji huduma za Hospitali Tembezi (*Mobile Clinic*) katika kuhakikisha wanapata huduma mbalimbali za kinga na tiba kwa urahisi. Hata hivyo, Serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma imekuwa ikitoa huduma za Hospitali Tembezi katika Halmashauri zote za Mkoa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa kuanzia tarehe 10 – 19 Agosti, 2017 Halmashauri ya Mji wa Kondoa, Chemba na Kondoa Vijijini kwa Kushirikiana na Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa ziliendesha huduma ya kibingwa kwa Hospitali Tembezi katika Hospitali ya Kondoa. Katika zoezi hili, jumla ya Madaktari Bingwa 31 walitoa huduma mbalimbali za kibingwa kwa wagonjwa 6,873 kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kupitia Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mji imeanzisha huduma za Hospitali Tembezi kwa watu wanaoishi na VVU kila mwezi katika Zahanati za Kingale na Kolo ili kuwapunguzia wagonjwa adha ya kufuata huduma hii katika Hospitali ya Wilaya.

SPIKA: Mheshimiwa Sannda, muuliza swali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, samahani.

SPIKA: Aahl!, Mheshimiwa Sannda, kumbe bado kuna majibu ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa itaendelea kutoa huduma hizi mara kwa mara kwa lengo la kuwasaidia wagonjwa kupata huduma za kibingwa na huduma nyingine katika maeneo yao na kuepusha kuingia gharama kufuata huduma za kiafya.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.
Mheshimiwa Edwin.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Hapa naweza nikasema ni pale ambapo Golikipa wa Simba anapigisha shuti la penati na mshambulaji wa Yanga halafu yeye anaenda kushoto goli linaingia kulia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, majibu yaliyotolewa na Serikali pamoja na shukrani zote, lakini kidogo yamekwenda tofauti na malengo ya swali lenyewe. Huu utaratibu wa Hospitali Tembezi tumekuwa tukiufanya hasa sisi wenyewe Wabunge tukishirikiana na Ofisi ya Mkoa. Tumefanya mara kadhaa, kama mara tatu na tunatarajia tena mwezi wa Septemba, 2018 tutapata nyingine kutoka Marekani.

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nikitarajia hapa ni ubunifu huu tulioanza nao kutokana na uchache wa huduma za kibingwa lakini pia na huduma nyingine za afya, kwenye ngazi ya Halmashauri na kwenye ngazi ya Wilaya tuupeleke kwenye vijiji, ndiyo maana niliainisha vijiji vingi ambavyo tunavizungumzia hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida tumekuwa tunachukua gari la chanjo na mengineyo ya miradi kufikisha huduma za kliniki za watoto, chanjo, huduma za akinamama wale, lakini sasa zinafanyika nje kwenye uwazi, jambo ambalo halina staha sana, ndiyo maana tukawa tunahitaji Kliniki Tembezi. Huu ni ubunifu tuliofanya kwenye ngazi ya Wilaya, sasa tuufanye kwenye ngazi ya Vijiji. Je Serikali haioni umuhimu wa kuenzi na kuiga ubunifu huu kwenye ngazi ya vijiji? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuweza kujenga Zahanati kwenye kila Kijiji kama ilivyo sera yetu, gharama yake ni kubwa sana na haya maeneo yote niliyoainishwa unaweza ukazungumzia maeneo matano mpaka sita ambapo ukipata gari moja la namna hiyo la Kliniki Tembezi, linaweza likakusaidia kuweza kumaliza huduma ya kujenga

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Zahanati nne. Je, ni lini basi, na kwa kuwa tunafahamu uwezo wetu ni mdogo bora tufanye...

SPIKA: Mheshimiwa Edwin naomba sasa unyooke kwenye swalii.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Eeh!

Mheshimiwa Spika, ni lini basi, Serikali itaiga ubunifu huu na kutuletea *Mobile Clinic Van* kwa ajili ya maeneo yetu ya Kondoa? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mawili ya Mheshimiwa Sannda, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kwanza nimpongeze Mheshimiwa Sannda kwa jinsi ambavyo amekuwa akipigania wananchi wake kuhusiana na suala zima la afya. Wiki iliyopita alikuwa anaongelea juu ya suala la gari la wagonjwa, lakini leo anaongelea juu ya *Mobile Clinic*.

Mheshimiwa Spika, katika swalii lake alilenga gari linalotembea kwa ajili ya kutoa huduma. Sasa kwa namna ambavyo swalii limekuja ndio maana anasema ni kama tumehamisha goli, lakini siyo nia ya Serikali kuhamisha magoli kwa sababu majibu yote tunayo.

Mheshimiwa Spika, katika swalii lake la kwanza anauliza uwezekano wa kuiga hili jambo zuri ili kuvipunguzia vijiji vingi badala ya kufuata huduma maeneo ya mbali. Naomba tukubalianae na Mheshimiwa Sannda kwamba ni nia ya Serikali, pale ambapo uwezo unakuwa umeruhusu hatuna sababu ya kutowapelekea wananchi huduma jirani yao.

Mheshimiwa Spika, katika swalii lake la pili, anaombaa tuige utaratibu mzuri ili kuwa na *Mobile Clinic Van*. Utakubaliana nasi kwamba wananchi wengi wamejitokeza,

wametoa nguvu zao katika ujenzi wa Zahanati na Vituo nya Afya. Pamoja na wazo jema hili, lakini itakuwa siyo busara nguvu ile ambayo imetumiwa na wananchi tukai-dump halafu tukaanzisha jambo lingine. Kwa kadri nafasi itakaporuhusu na nguvu ya kibajeti ikiruhusu, wazo hili ni jema, naomba tulichukue kama Serikali kulfanyia kazi kwa siku za usoni. (*Makofii*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Anna Gidarya na Mheshimiwa Musukuma.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mazingira yaliyopo Kondoa yanafanana na mazingira yaliyopo Babati Vijiini. Zahanati ya Galapo ni Zahanati ya muda mrefu, imepandishwa kuwa Kituo cha Afya, lakini mpaka sasa hatuna jengo la upasuaji. Kwa nguvu za wananchi tumejitahidi mpaka tumepaua hilo jengo. Mpaka sasa tuna vifaa nya hicho chumba cha upasuaji lakini tuna changamoto ya kumalizia hilo jengo ili litumike. Ni lini sasa Serikali itapeleka pesa za kumalizia hilo jengo? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Said Selemani Jafo, majibu tafadhali ya Kituo cha Afya, Galapo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeze dada yangu Mheshimiwa Anna kwa swali zuri, lakini nawapongeza Wabunge wa Babati na kaka yao Mheshimiwa Jitu Soni kwa pamoja. Nafahamu Babati Vijiini ina changamoto kubwa ya afya na ndio maana kwa Zahanati ya Galapo ambayo imepandishwa lakini kwa sasa kipaumbele chetu kwamba tumeanza na vituo viwili nya afya, kile ni cha kwanza na sasa hivi tunaenda katika Kituo cha Magugu, kwa sababu tunajua pale Magugu ni *center* kubwa sana gari nyingi zinapita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo tumeweka kipaumbele na hata hivyo ni mpango wa Serikali kuhakikisha

kwamba Kituo cha Afya cha Galapo tutafanya kila liwezekanalo kwa mipango ya Serikali tuweze kukiimarisha kwa ajili ya wananchi wa Babati Vijijiini waweze kupata huduma vizuri. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Kasheku.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa matatizo yaliyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni sawa kabisa na matatizo yaliyoko Jimboni kwangu. Jimbo la Geita Vijijiini lenye *population* ya watu kama 1,000,000 halina kabisa Kituo cha Afya hata kimoja, baada ya Kituo cha Afya Nzela kupanda hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya. Je, Wizara haioni umuhimu wa kutusaidia pesa ili tuweze kujenga kituo kwa wananchi walioko Ibisabageni na Rubanga kuliko na umbali wa kilometra 80 mpaka kukipata Kituo cha Afya kilichopandishwa hadhi ya kuwa Hospitali ya Wilaya? (*Makof!*)

SPIKA: Dahi! Aisee ninyi Wasukuma, watu milioni moja hawana Kituo cha Afya? Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala na Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu ya swali hilo muhimu sana. (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kweli tunafahamu changamoto kubwa ya afya kule Geita Vijijiini na hata hivyo namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kwa pamoja tumeshirikiana kuhakikisha Kituo cha Afya cha Nzela kile cha kwanza kimekuwa ni cha kisasa zaidi. Hata hivyo, kwa vile tunajua changamoto ni kubwa, ndiyo maana Geita DC sasa hivi tunaenda kuipa Hospitali ya Wilaya rasmi sasa katika bajeti yetu ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika Mpango wa Serikali wa sasa, nia yetu ni kwamba kabla ya mwezi wa Tisa mwishoni kuelekea mwezi wa Kumi tutakuwa tumeweka miundombinu ya kisasa katika Kituo cha Afya cha Nyarugusu, nadhani ni Zahanati lakini tutai-*upgrade*. Lengo kubwa ni

kwamba wachimbaji ambao ni *population* kubwa ya eneo lile waweze kupata huduma nzuri sana ya afya na kuwahudumia wananchi wa Geita kwa ujumla wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swali la mwisho la nyongeza.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii adimu. Wilaya ya Hanang' ina Kituo cha Afya kimoja ambacho ndicho kinakarabatiwa sasa lakini kuna Wilaya kubwa haina Kituo cha Afya kingine. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri Kituo cha Afya cha Basotu na Kituo cha Afya cha Endasak ambako kuna watu wengi ambao wanategemea huduma hiyo, atusaidie. Je, anaweza kutuambia ni lini ukarabati huo utaanza ili watu wa Endasak na Basotu waweze kunufaika na huduma ya afya?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI, tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOANA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba Mheshimiwa Mary Nagu, tena alikuja na wananchi wake tukiwa getini alileta hiyo hoja. Nakiri wazi pia kwamba Endasak na Basotu ni changamoto kubwa na ina *population* kubwa. Nia na mpango wa Serikali ni kwamba Mungu akijaalia kabla ya mwezi wa Tisa tutakuwa tumeshaanza ujenzi pale Basotu kwa kadri kama tulivyokubaliana siku ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Tuendelee na maji na umwagiliaji, swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad.

Na. 460

Kukamilisha Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Kijiji cha Ishololo – Wilaya ya Shinyanga

MHE. AZZA H. HAMAD aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji katika Kijiji cha Ishololo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa Bwawa la Ishololo uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini ni moja kati ya miradi iliyokuwa ikitekelezwa kuititia Mradi wa Uwekezaji katika Kilimo chini ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Utekelezaji wa mradi huo ulifikia ukomo wake mwezi Desemba, 2013 ambapo Benki ya Afrika ilisitisha kutoa fedha za utekelezaji wa mradi wakati utekelezaji wake ulikuwa bado haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina dhamira ya dhati ya kukamilisha skimu zote za umwagiliaji ambazo utekelezaji wake haujakamilika kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa fedha. Kwa sasa Serikali inakamilisha mapitio ya Mpango kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ambao unabainisha hali ya skimu za umwagiliaji nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji nchini Serikali itatoa kipaumbele kwa miradi yote itakayobainishwa ukiwemo mradi wa umwagiliaji katika Kijiji cha Ishololo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

SPIKA: Mheshimiwa Azza, swali la nyongeza.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga hawana mradi hata mmoja wa umwagiliaji na hivyo kuwepo kwa mradi huu tulitegemea kuleta tija kwa wakulima wetu, hasa wakulima wa mbogamboga na vitunguu.

Mheshimiwa Spika, mradi huu umetumia fedha nyingi sana na umeachwa na mashimo mengi ambayo hayana maana yoyote kwa wakulima wetu. Swali la kwanza, je, Serikali ipo tayari sasa kutoa kipaumbele katika mradi huu ili uweze kuleta tija kwa wananchi kama ambavyo Serikali ilikuwa imekusudia.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari sasa kwenda katika Kijiji cha Ishololo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga akajionee mwenyewe hali halisi ambayo iliachwa na Mkandarasi pamoja na fedha nyingi kutumika katika mradi ule? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso, upo tayari kwenda kwa watani zako Usukumani huko?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, ni Mbunge mfuatiliaji, ni mpambanaji wa matatizo ya wananchi wake wa Shinyanga, lakini kubwa la msingi kwa kuzingatia umuhimu wa umwagiliaji, Serikali itatoa kipaumbele katika suala zima umwagiliaji katika Kijiji cha Ishololo katika kuhakikisha wananchi wa Shinyanga wanawekeza katika umwagiliaji ili tupate bidhaa au fursa ambayo itaweza kuwekeza katika suala zima la viwanda.

Mheshimiwa Spika, la msingi lingine ambalo ameniomba nifike katika eneo la Ishololo, niko tayari, mimi ama Waziri wangu tumejipanga katika kuhakikisha Bunge

litakapokuwa limekwisha, kutembelea maeneo yote ambayo tuliahidi Waheshimiwa Wabunge kufika ili kujionea changamoto na maeneo yote ambayo tutakuta yana changamoto tutachukua hatua.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Bulembo, kule mwisho kabisa swali la nyongeza.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kutokana na swali la msingi lilloulizwa na Mheshimiwa Azza, kule Mkoani Mara kuna Wilaya moja inaitwa Serengeti, katika ile Wilaya ya Serengeti kuna Bwawa moja linaitwa Manchira, limeanza tangu mwaka 1988, mpaka leo maji hayatoki unaambiwa kuna chujio. Naomba tamko la Serikali, lini maji yale yataanza kutoka kuwasaidia wananchi wa Serengeti, maana ni miaka 10 leo? (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kweli Bwawa la Manchira tangu Mbunge Mheshimiwa Wanyancha alikuwa akiongelea jambo hilo. Unasemaje kuhusu swali hilo, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, hakuna jambo lisilokuwa na mwisho na sisi kama viongozi wa Wizara hii ya Maji, jukumu letu ni kuhakikisha Watanzania wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshleza. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge Baba yangu Mzee Bulembo, hebu tuonane tuweze kupata mawazo ya pamoja ili tuweze kusukuma katika kuhakikisha wananchi wale wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshleza. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Marwa Ryoba, swali lako limeshaulizwa huko. Mheshimiwa Mbunge wa Mvomero, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Ngalawa.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii. Naomba niungane na Mheshimiwa Azza, naomba niulize swali moja

dogo la nyongeza. Wilaya ya Mvomero imejaaliwa baraka kubwa na Mwenyezi Mungu, maji ni mengi, mabonde ni mengi, Waziri alituahidi miradi miwili ya umwagiliaji. Mradi wa Mbogo na mradi wa Kigugu yenze thamani ya shilingi bilioni tatu toka mwaka jana. Je, ni lini sasa fedha hizo zitatolewa ili wananchi wale waweze kuijendeleza katika miradi hii ya umwagiliaji. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli aliahidiwa na Mheshimiwa Waziri wangu kupewa miradi miwili ya umwagiliaji na kwa kuwa ahadi ni deni, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sasa hivi tunapitia mapitio ya mpango kabambe wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili tuweze kujiridhisha. Nataka nimhakikishie ahadi ile tutaitekeleza katika kuhakikisha wananchi wake wa Mvomero wanapata miradi hiyo yote miwili ya umwagiliaji.

SPIKA: Mheshimiwa Ngalawa, tafadhali.

MHE. DEO F. NGALAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Bonde la Mto Ruhuhu ambalo linaunganisha Wilaya ya Ludewa na Wilaya ya Nyasa, liliwekwa kwenye bajeti ya 2016/2017 juu ya ujenzi wa bwawa la umwagiliaji. Cha kushangaza, katika miaka hii miwili bwawa lile halipo kwenye bajeti. Je, Serikali ina mpango gani na ujenzi wa Bwawa la Mto Ruhuhu.

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Spika, tunatambua umuhimu wa umwagiliaji, lakini katika suala zima la umwagiliaji tangu tumeingia katika Wizara hii tumekuta changamoto kubwa sana. Kutokana na changamoto tulizobainisha katika umwagiliaji, Waziri

wangu akaona haja sasa ya kupitia mpango kabambe wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2002 ili tuweze kubainisha zile changamoto na kuweza kuzipatia majibu.

Mheshimiwa Spika, tumeona baadhi ya miradi ya umwagiliaji imejengwa lakini haijakamilika, vile vile hata hiyo iliyokamilika imekuwa ikiwasaidia wakulima katika kuvuna msimu mmoja wakati tunapozungumzia umwagiliaji ni mbadala kwa maana ya wakulima waweze kulima kiangazi na hata masika.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, baada ya mapitio, sisi kama Wizara ya Maji na Umwagiliaji, tutaona umuhimu wa kuhakikisha kwamba tunampa kipaumbele, wananchi wake waweze kupata kilimo cha umwagiliaji.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Haonga, uliza swali la mwisho la nyongeza.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, naskushukuru sana. Naomba na mimi niulize swali la nyongeza. Skimu nydingi za umwagiliaji ambazo ziko Mbozi, Kata ya Bara kuna Skimu ya umwagiliaji ambayo ni ya miaka mingi sana, miundombinu yake imechoka na skimu hii haifanyi kazi vizuri. Sasa Mheshimiwa Waziri yuko tayari kukarabati skimu hii ya umwagiliaji ambayo iko Kata ya Bara ili iweze kuwasaidia wananchi wa Kijiji cha Bara, Kata ya Bara, Wilaya ya Mbozi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la wananchi wa Mbozi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kama nilivyokuwa nimeeleza kwamba, katika Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji tumeona kabisa tumekuwa na changamoto katika suala zima la umwagiliaji. Moja ya changamoto tumekuwa na miradi mingi lakini haijakamilika, tunapitia mapitio yetu kabambe

lakini nataka nimhakikishie, maeneo yote ambayo miradi haijakamilika sisi kama Wizara ya Maji na Umwagiliaji tutahakikisha tunaikamilisha ili wananchi wale waweze kufaidika katika suala zima la umwagiliaji.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunahamia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali litaulizwa na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini.

Na. 461

Utaratibu wa Kupima Mizigo na Kusajili Abiria Katika Vyombo vyaa Majini

MHE. MUSSA B. MBAROUK aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isianzishe utaratibu wa kupima mizigo na usajili wa abiria katika vyombo vyote vya majini kama inavyofanyika *Airport* ili kuepusha ajali za mara kwa mara?

NAIBU WAZIRI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inao utaratibu wa kupima mizigo na usajili wa abiria katika vyombo vya usafiri kwa njia ya maji na utaratibu huo hutekelezwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) ambapo kwa hivi sasa utekelezaji wake unadhibitiwa na Wakala wa Meli Tanzania (*TASAC*).

Mheshimiwa Spika, vyombo vyote vya majini husajiliwa na kupewa vyeti vya ubora (*Sea Worthiness Certificate*) ambayo huonesha uwezo wa chombo husika

kubeba mizigo au abiria. Aidha, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) imeipa dhamana Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*) kutoa kibali cha kuondoa chombo bandarini (*Clearance Certificate*) kutoka bandari moja kwenda nyingine baada ya kujiridhisha kuwa chombo husika kimebeba abiria au shehena kulingana na viwango vya usalama vilivyokusudiwa kwa shughuli ambazo chombo husika kimesajiliwa kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwenye kibali cha kuondoa chombo bandarini hujazwa takwimu kama vile; idadi ya wafanyakazi wa chombo (*crews*), idadi ya abiria (*passengers*) idadi ya mizigo (*cargo*) na huambatanishwa na majina ya abiria (*passenger manifest*) na idadi ya mizigo (*cargo manifest*) kwa ajili ya ukaguzi, ukamilishaji wa miamala ya kibiashara, ufuatilaji pindi ajali inapotokea na kumbukumbu za ofisi. Hivyo, vyombo vyote hubeba shehena au kupakia abiria kulingana na uwezo wake na hivyo kuepusha ajali zisizo za lazima.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe wito kwa Watanzania wenzangu hususani wanaishi katika mwambao wa Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Tanganyika na Ziwa Nyasa kuacha kutumia vyombo vya usafiri visivyo sajiliwa na *SUMATRA* au *TASAC*, hususan vinavyotoa huduma katika bandari zisizo rasmi (bandari bubu) kwa upande wa Bahari Kuu na mialo kwa upande wa maziwa makuu ili kuepusha ajali za mara kwa mara na hivyo kunusuru maisha ya watu na mali zao.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Tanga, uliza swali lako.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri kwa maneno yake ya mwisho amekubaliana na mimi kwamba viro vyombo ambavyo vinatumia bandari bubu na havijafanyiwa usajili na wala havikaguliwi mzigo yake. Sasa kama wanavyosema watu nywele nyeupe ni sababu ya kuwa na busara zaidi. Sasa je, atakubaliana na mimi kwamba sasa

Serikali ipo haja ya kuhakikisha hata hivi vyombo vinavyotumia bandari bubu sasa vinakuwa na vyombo/zana za uokoaji kama *life jacket* na vitu vingine? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza la pili ni kwamba, kwa nini kuna bandari bubu ni kwa sababu kuna tozo na kodi za kuudhi kwa watu wanaotoka Zanzibar na maeneo mengine katika bandari zetu ndiyo maana wanatumia bandari bubu. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuondoa hizi kodi kama kwenye *TV* moja, radio moja au nguo chache kwa watu wanaotoka Zanzibar na Pemba wanaokuja maeneo ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge unatetea bandari bubu? Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano *Engineer Nditiye*, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kama nilivyoeleza mwanzo, umuhimu wa kutumia bandari rasmi tunapata *data* na kuhakikisha uimara na utayari wa chombo husika kusafirisha abiria kwa usalama zaidi. Kama Serikali, hatuwezi kuruhusu bandari bubu zitumike.

Mheshimiwa Spika, suala la tozo nikijibu swali lake la pili, tozo zinazotozwa kwenye vyombo vyaharini na maziwa makuu siyo kubwa sana kiasi cha kuruhusu watu waendelee kutumia bandari bubu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na Serikali kwamba tozo zinazotozwa na *affordable* kabisa na zinatumika na watu ambao wanataka kufanya kazi kwa uhakika na kwa usalama zaidi kwa ajili ya abiria wao.

SPIKA: Mheshimiwa Zainab Vulu nilikuona, uliza swali la nyongeza tafadhali.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, bandari ya Nyamisati

na bandari ya Kilindoni zimekidhi kigezo cha Serikali; na kwa kuwa wananchi wa kutoka Nyamisati kwenda Mafia au kutoka Mafia kwenye Nyamisati wanapata shida ya usafiri, uwezo wa majahazi yao hauzidi abiria 50 pamoja na mizigo yao. Je, ni lini Serikali itaondoa kadha hiyo kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo kwa kuwapelekea boti ambayo itakuwa salama na uhakika wa kusafirisha, ukizingatia kunakuwa na wazee, akinamama wajawazito, watoto, wanaokaa sana bandarini na kukosa usafiri wa uhakika? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Atashasta Nditiye, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana kwa jinsi anavyofuatilia hasa Bandari ya Nyamisati mpaka nimeshaizowea kuisikia kutoka kwake na Mheshimiwa Dau na wadau wote ambao wako Mkoo wa Pwani bila kumsahau Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu Mheshimiwa Hawa Mchafu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna vyombo vinafanya kazi maeneo yale, lakini niwapongeze sana Wabunge wa eneo lile kwa sababu vyombo karibu vyote vinavyofanya safari kati ya Mafia na Nyamisati vimesajiliwa na ndiyo maana hata ikitokea ajali, huwa kuna utaratibu maalum ambao tunaweza kupata taarifa rasmi za ajali hiyo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali ina mpango wa kupeleka boti muda huu wakati tunaendelea na utengenezaji wa *land craft* kubwa tumewapatia TEMESA Sh.3,800,000,000 kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, hivyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoo wa Pwani wasiwe na wasiwasi Serikali ina utaratibu wa kutengeneza kivuko kile pamoja na *boat* la kuwasafirisha abiria. (*Makofii*)

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa uliza swali la nyongeza tafadhalii.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imebaini kuwa kuna bandari bubu na henziepukiki bandari bubu hizo. Je Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hizi bandari bubu, wenyewe vyombo katika bandari bubu wanasaajiiliwa ili kuepusha ajali za mara kwa mara? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, bandari bubu za *boat* za kutoka Pemba kwenda Tanga ambazo henziepukiki hizo bandari bubu unasemaje Mheshimiwa. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna changamoto ya bandari bubu na kama Serikali tumekuwa tukiendelea kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuzirasimisha bandari hizo kwa msaada mkubwa sana wa Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuwasiliana na wadau ambao wanaendesha bandari bubu. Kwa sababu nyingine huwa zinakuwa zinachangamka kabisa na zinatakiwa zipewe miundombini mbalimbali ya Kiserikali ili ziwe salama kwa ajili ya Watanzania. Nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kuzitembelea na kuwapa elimu na inapotakiwa tutaendelea kuzirasimisha ili kuokoa maisha ya Watanzania waweze kusafiri salama. (*Makofi*)

SPIKA: Bahati nzuri Wabunge wote wa Pemba wamekaa kimya, nilitaka niwape nafasi lakini kumbe mnakubali, Mheshimiwa Khatibu swalil ya nyongeza tafadhali. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Toka asili bandari bubu ndiyo msaada mkubwa kwa wananchi hususani wa Visiwani baina ya Zanzibar na Mwambao wote huu wa Bahari ya Hindi. Linapokuja suala la bandari bubu na vyombo hivi mara nyingi vinaangaliwa vyombo vyaa baharini na vyombo vyaa maziwa vinakuwa vinaachiwa huru. Nataka kujua ni kwa nini bandari bubu

ambazo wanazisema lakini zinakidhi viwango mfano Kipumbwi, Kigombe Tanga ambazo zinakidhi viwango hawazirasimishi haraka na kufanya kazi wananchi wakapata tija kwa safari zao?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, bandari bubu ni bandari bubu tu, hakuna namna ambavyo unaweza ukaifanya ikawa rasmi kwa kuibadilisha kwa maneno. Ni lazima taratibu za Kiserikali na Sheria zifuatwe kuifanya bandari bubu iweze kuwa rasmi. Nimewahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba bandari bubu zote ambazo zinakidhi vigezo tumekuwa tukizitembelea na kutoa elimu na kuwapa mapendekezo mbalimbali Kiserikali ambayo yatasababisha ziweze kuwa bandari rasmi.

Mheshimiwa Spika, Serikali haiwezi kufurahia kuendelea kuwa na bandari bubu na wala hatuwezi kuruhusu bandari bubu ziwepo, kikawaida bandari bubu zote hatuziruhusu. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba, hizo bandari alizozitaja tutazitembelea, tutaongea na wadau, tukiona zinakidhi vigezo tutazisajili halafu zitakuwa bandari rasmi. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Tuendelee na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Swali la Mheshimiwa Anna Gidary, tafadhalii.

Na. 462

**Huduma za Msingi Katika Kituo cha Wazee
Sarame – Babati Vijijini**

MHE. ANNA J. GIDARYA aliuliza:-

Kituo cha Wazee Sarame kilichopo Magugu, Wilaya ya Babati Vijijini ni kituo cha muda mrefu ambacho

kinahudumiwa na kusimamiwa na Wizara ya Afya. Kituo hiki kina changamoto nyingi ikiwemo uhaba wa watumishi, usafiri wa dharura, huduma ya kwanza, vifaatiba na miundombinu ya barabara:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma zote za msingi katika kituo hicho ikizingatiwa kuwa wazee wengi ni wale mavu wa viungo, vipofu, waliopooza na viziwi pia?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Joram Gidarya, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikihakikisha upatikanaji wa huduma za msingi katika makazi ya wazee na watu wenye ulemavu, wasiojiweza ikiwa ni pamoja na wanaotunzwa katika makazi ya Magugu yaliyopo katika Halmashauri ya Babati Vijiji. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Serikali imepeleka fedha kiasi cha Sh.14,631,935.47 kwa ajili ya chakula na Sh.900,000 kwa ajili ya dharura zinazojitokeza, bajaji moja katika makazi hayo kwa ajili ya kurahisisha usafiri.

Mheshimiwa Spika, aidha, makazi ya Magugu yamepata huduma ya upulizaji wa dawa za kuuwa wadudu kwa maana ya *fumigation* mwezi Mei, mwaka huu 2018. Wizara imeendelea kupeleka vifaa vya usafi na huduma ya kwanza kwenye makazi yote ya wazee ikiwa ni pamoja na makazi ya Magugu. Aidha, uboreshaji wa huduma na miundombinu katika makazi utaendelea kufanyika kadri ya fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na haya, Serikali bado inatambua kuwa zipo changamoto zinazokabili utoaji wa huduma za msingi kwenye makazi ya wazee na ili kukabiliana nazo Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, imetenga

jumlah ya fedha Sh.27,032,000 kwa ajili ya chakula na Sh.3,600,000 kwa ajili ya dharura. Aidha, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, ilitenga bajeti ya Watumishi wa Ustawi wa Jamii wapatao 24 na katika bajeti ya Mwaka 2018/2019, Wizara imetenga bajeti ya watumishi 60. Wizara inaabidi kuwapeleka baadhi ya Watumishi hawa kwenye makazi ya wazee Magugu yaliyopo Sarame-Babati Vijijini pale tu tutakapopata kibali cha ajira zao.

SPIKA: Mheshimiwa Anna Gidarya, uliza swali lako sasa.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, natambua kazi kubwa wanayofanya Waziri wa Afya na Naibu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri waliyompelekea haya majibu wamemdanganya, kwa sababu mimi ni tomaso, naomba niambatane naye, nikapapase mwenyewe. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumsikilize Mheshimiwa anauliza swali.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyoko kwenye hiki kituo ni matatizo makubwa sana. Kama kuna kitu ambacho Wizara haifahamu katika kile kituo kuna wazee 52 na katika hao 52 kuna wazee wanne ni kati ya wazee waliyopigania Vita vya Pili vya Dunia.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo makubwa ya Watumishi wa Afya tuna Watumishi wawili tu, mmoja anakaa Babati Mjini na mwagine anakaa kilometra moja na nusu kutoka kwenye kituo, maana yake usiku kukitokea dharura wale wazee hawapati huduma za haraka. Je, ni lini sasa Serikali itawajengea nyumba wale watumishi wapate kuishi karibu na wale wazee?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa nchi nzima idadi ya wazee inajulikana na kwa kuwa umri mkubwa wa

uzee ndio unaopatikana na magonjwa makubwa nyemelezi pamoja na kuwa Serikali imesema huduma ya wazee ni bure. Je, Serikali iko tayari kuwapatia bima wazee wote nchi nzima? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo muhimu sana ya wazee, Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Ndugulile, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, labda nianze kwa kusema kwamba kuwepo na idadi kubwa ya wazee ambao sasa hivi wanafikia milioni 2.7 ni ishara kwamba kumekuwa na maboresho makubwa sana katika huduma ambazo tumekuwa tunazitoa katika ngazi ya afya, vilevile hali ya lishe na matunzo ambayo tumekuwa tunayatoa kwenye jamii yetu, kwa hiyo ni kitu ambacho najivunia. Sasa hivi umri wa kuishi wa Mtanzania umefikia miaka 65 wastani, kwa hiyo, ni jambo jema ambalo tunapaswa kujivunia.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na maswali ambayo ameuliza Mheshimiwa Anna Gidarya ni kweli tunatambua kwamba Serikali tumeendelea kuwa tunaboresha makambi haya ya wazee kadri uwezo unavyoongezeka. Pia hili ombi la kuhakikisha kwamba tunakuwa na nyumba katika kituo hichi cha Magugu, tutalifanyia kazi katika bajeti kama nilivyokuwa nimesema kwamba tuna fedha ambazo tumezitenga katika bajeti hii ambayo ipo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, sasa hivi Serikali ipo katika mapitio ya sera ya afya. Katika sera ambayo tunaenda nayo sasa hivi ya mwaka 2017/2018 ambayo tunayo sasa hivi, tumekuwa tunasema kwamba matibabu kwa wazee yatakuwa ni bure, lakini sasa hivi Serikali tunaelekea katika mfumo wa kuwa bima ya afya kwa wote na masuala ya haki ya wazee yatazingatiwa katika sera hii mpya.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema tu kwamba kuhusiana na ombi lake la ziara kwenda kupapasa niko tayari kufanya Jumapili. (*Kicheko*)

SPIKA: Hilo sitakuruhusu, nitamruhusu Mheshimiwa Waziri wako ndiyo aende hiyo safari. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Ester Mahawe, sasa uliza swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Manyara ni mkoa mkubwa tu na una wilaya tano na majimbo saba na haiwezekani kuapeleka wazee wote katika kituo kimoja tu kinachopatikana Magugu. Je, ni nini juhudzi za Serikali katika kuhakikisha Wilaya ya Hanang', Simanjiro, Kiteto na Mbulu tunapata kituo kingine cha wazee?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Ester Mahawe kwa kufuatilia maendeleo ya Manyara na Babati Mjini. Kwanza kwa mujibu wa Sera ya Wazee tunahamasisha wazee walelewe katika familia. Kwa hiyo Serikali haina mpango wa kujenga makazi ya wazee zaidi ya makao ya wazee 17 ambayo tunayo.

Mheshimiwa Spika, tunakusudia kutunga Sheria ya Wazee ambayo itatoa wajibu kwa watoto kutoa matunzo kwa wazee wao. Kwa sababu katika yale makambi kuna wazee wana watoto wao, wametelekezwa na familia zao. Kwa hiyo nitoe wito, niwausie Watanzania wazee hawa, wazazi wetu, wametulea, wamepigania nchi na sisi ni wajibu wetu kuwalea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na niwaambie hata Wabunge tukichukua mzee mmoja au wawili tukakaa nao kwenye familia zetu ni baraka kwa Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri hiyo Sheria ikishatungwa, kuna wazee wengine ndiyo wanaoa vibinti vigoli kabisa halafu unalazimisha watoto watunze mzee wa namna hiyo kweli! Jamani maswali ya nyongeza mnapaswa kuwa wazee, lakini sasa wote nawaangalia ni vijana watupu.

MBUNGE FULANI: Wazee watarajiwa.

SPIKA: Ni wazee watarajiwa! Haya Mheshimiwa Parezzo, mzee mtarajiwa. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza ninasikitika hiyo kauli aliyotoa Mheshimiwa Waziri hapo na wale wazee ambao, maana yake mzee anaanzia kijana, mtoto ambaye inawezekana mazingira yake yote alikuwa ni yatima. Sasa huyu pia unamfanyaje, maana yake Serikali mnakwepa wajibu. Swali langu ni kwamba Serikali ya Awamu ya Nne iliahidi kutoa pensheni kwa wazee na tafiti zilishafanyika, kauli ikatolewa hapa Bungeni. Je, ni lini Serikali itatoa pensheni kwa wazee wetu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba nisitisite majibu ambayo amesema Mheshimiwa Waziri, kwa mujibu wa Sera yetu ya Wazee ya mwaka 2003 ambayo inatamka kwamba majukumu ya kwanza ya kumtunza mzee ni familia, ndugu na jamii husika kabla Serikali haijabebe majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea tunahudumia wazee zaidi 500 ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo bado tunaendelea kusitisiza kwamba majukumu ya awali ya msingi yawe katika ngazi ya familia na jamii kabla ya Serikali haijachukua majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake ambalo anauliza kwamba ni lini na tumefikia wapi katika pensheni hii ya wazee, bado Serikali inaendelea kulitafakari jambo hili, kuangalia utaratibu mzuri zaidi wa kuweza kulitekeleza. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani nilikuona, swali la mwisho la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa tunaamini kwamba wazee ni hazina ya Taifa letu, kama ilivyotengwa kitengo kwa ajili ya vijana, asilimia tano ya vijana na wanawake, Wizara haioni sasa ni busara kutenga pesa kwa ajili ya kuwalipa wazee wetu iwe kama...

SPIKA: Mwishihi haukusikika, rudia tena.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushuru. Tunaamini kwamba wazee ni busara ya Taifa na ni hazina ya Taifa letu. Kwa kuwa asilimia tano imetengwa kwa ajili ya vijana na wanawake, Wizara sasa haioni ni busara kutenga fedha kwa ajili ya kuwalipa wazee wetu kama baraka katika Taifa?

SPIKA: Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, tafadhalii majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Spika, nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa kuhusu masuala ya wazee. Kama Serikali na kama ilivyo sema katika llani ya Uchaguzi miundombinu yote ya kuwezesha wazee hawa kuweza kulipwa imekwisha andaliwa. Kama Naibu Waziri alivyo sema ni taratibu za ndani zinaendelea na pindi taratibu hizi zikikamilika, basi Serikali itatekeleza azma yake ya kuweza kuwalipa wazee pensheni kama ilivyo sema katika llani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Swali la Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi na kwa niaba yake Mheshimiwa Hawa Ghasia muulizie swali lake tafadhalii.

Na. 463

Nyumba na Usafiri kwa Askari Polisi Masasi

MHE. HAWA A. GHASIA (K.n.y. MHE. RASHIDI M. CHUACHUA) aliuliza:-

Jeshi la Polisi katika Wilaya ya Masasi halina nyumba za makazi na usafiri kwa muda mrefu sana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea askari hao nyumba za kuishi kwa sababu nyumba wanazoishi sasa zimechakaa sana na pia hazitoshelezi mahitaji yao?

(b) Je, ni lini Serikali itawapatia usafiri wa uhakika Askari hao ili waweze kusimamia usalama wa raia na mali zao kwa uhakika?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la uhaba wa nyumba za makazi kwa Askari wa Jeshi la Polisi nchini ikiwemo Wilaya ya Masasi. Hata hivyo, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kupunguza tatizo la makazi ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wananchi na wadau kujenga nyumba kwa ajili ya makazi ya Askari.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itajenga nyumba za kuishi

Askari kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Wilaya ya Masasi ina magari matatu ambapo kati ya hayo magari mawili ni mabovu. Jeshi la Polisi hugawa magari kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo hali ya uhalifu, sababu za kiutawala na jiografia ya mahali husika. Kwa kuzingatia vigezo hivyo hususani jiografia yake, Wilaya ya Masasi itapewa kipaumbele katika mgao wa magari mara yatakapopatikana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri naona Bunge zima limesimama. Mheshimiwa Hawa Ghasia uliza swali lako. (*Kicheko*)

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Wizara inayo dira na inayo dira na mpango mkakati ambapo inatambua matatizo yaliyopo na hayo matatizo yanaiwekea katika mipango yake mikakati. Je, kwa mujibu wa mpango mkakati wake hizo nyumba za Askari wa Masasi zitajengwa lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa mujibu wa mpango wa mkakati huohuo na dira yake haya magari mawili au zaidi kwa Wilaya ya Masasi yatatolewa lini badala ya kuacha tu bila kuwekewa muda?

SPIKA: Majibu ya swali hilo *Engineer Masauni*, Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwamba kulingana na mipango tuliyokuwa nayo kuhusiana na ujenzi wa nyumba za Polisi Masasi pamoja na kupeleka gari, kama ambavyo nimejibu katika swali langu la msingi kwamba mipango hii inategemea na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la nyumba bahati njema ni kwamba tayari tumeshapata fedha za kuanzia ambayo tunatarajiwa kujenga nyumba 400. Kwa hiyo, katika Mkoa wa Lindi pia nyumba hizo zitajengwa,

naomba baada ya Bunge hili ni nganjalie ili niweze kumpa takwimu halisi za wilaya ya Masasi kuhusiana na nyumba hizo zipoje.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la gari nimezungumza kwamba, kulingana na hali ya uhalifu, hasa kubwa zaidi jiografia ya Masasi ilivyo inastahili kupata gari. Nikaeleza kwamba, pale ambapo magari yatapatikana basi katika maeneo ya vipaumbele vilevile Wilaya ya Masasi ni mojawapo. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira magari yakipatikana tutapeleka na bajeti ikikaa vizuri nyumba tutajenga. (*Makofi*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Ndassa na Mheshimiwa Mbunge wa Vunjo utafuatia.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, kama Waziri mwenye dhamana, nyumba za Magereza zilizoko pale Isanga hazifai, hazifai, kabisa kukaliwa na binadamu.

Mheshimiwa Spika, hata wewe kwa sababu ni mtu wa Dodoma, ukienda pale ukiona zile nyumba utasema hizi nyumba wanakaa binadamu? Naomba kupata tamko la Serikali, lini nyumba hizo zitajengwa upya kwa ajili ya Askari wetu hawa wa magereza katika Gereza Kuu la Isanga?

SPIKA: Anauliza Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu nyumba zisizofaa kabisa za Gereza Kuu la Isanga Dodoma. Wizara ina mpango gani na nyumba hizo ambazo kwa kweli zinapaswa kuwa *condemned*, hazifai kabisa.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli hata katika Jeshi la Magereza tuna changamoto ya uhaba wa nyumba na uchakavu wa nyumba za Askari Magereza. Ndiyo maana tunatumia njia mbalimbali ukiachilia mbali utaratibu wa kawaida wa kibajeti, tumekuwa tukitumia rasilimali katika maeneo husika kuzikarabati nyumba hizo, hasa ukililia maanani kwamba,

Jeshi la Magereza lina kitengo madhubuti kabisa kinachojishughulisha na ujenzi pamoja na nguvu kazi ya wafungwa.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukifanya hivyo maeneo mbalimbali katika nchi, lakini fursa kubwa ambayo inaangukia katika Gereza la Isanga lililopo Dodoma ni juu ya hatua ya Serikali kuhamisha Makao Makuu yake rasmi kuja Dodoma. Jambo hilo limesababisha sasa hivi kuwa na fursa pana ya kutanua wigo wa mazingira ya ufanyaji kazi pamoja na makazi ya Askari wa vyombo vyetu vyote. Ndiyo maana mtaona sasa hivi kwamba, katika eneo la Magereza, Uhamiaji na Jeshi la Polisi kuna maendeleo makubwa ya kuboresha makazi ya Askari Dodoma ili kwenda sambamba na kasi ya ongezeko la ukuaji wa Mji wa Dodoma kutokana na maamuzi thabiti ya Serikali ya kuhamishia Makao Makuu Dodoma.

SPIKA: Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kituo cha Himo kiko mpakani na kinahudumia zaidi ya watu 500,000 na ukiangalia hali ya uhalifu, hasa mambo ya biashara za magendo mpakani ni kubwa. Serikali imekuwa ikiahidi kupatia kituo hiki gari, gari lililopo ni la zaidi ya miaka 10 na tulipewa na CRDB na gari hili limekuwa ni kazi ya Mbunge kulikarabati kila mwaka. Serikali imeshawahi kutoa ahadi zaidi ya mara tatu kuhakikisha wanapeleka gari Kituo cha Himo ili haki ya ulinzi na usalama wa Taifa ni kazi namba moja ya Serikali. Serikali watamke hapa ni lini wanapeleka gari hilo waliloahidi hapa *immediately* kabla Bunge hili halijamalizika kituo cha Himo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kuhusu kituo hicho cha Mpakani.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbatia

amekuwa akiguswa sana na hili suala, nadhani si mara yake ya kwanza kuuliza hapa, mara ya mwisho nilimjibu na narudia jibu ambalo nimempa mara ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, tunatambua changamoto za vituo vya Polisi vilivyopo mipakani, kikiwemo kituo cha Himo kama ambavyo amezungumza. Changamoto ambayo tunaipata sasa hivi ni kwamba, bado hatujapata magari mapya. Kwa hiyo, nikazungumza kwamba, tutaangalia sasa magari yatakapokuja yamekuja magari mangapi na wapi panahitaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, natambua kituo ambacho amezungumza ni moja kati ya maeneo ambayo yanahitaji zaidi, itategemea wapi panahitaji zaidi sana na idadi ya magari yaliyopo. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira naamini kabisa kama siyo leo, kesho kama siyo kesho keshokutwa, Iakini Serikali inatambua sana umuhimu wa maeneo haya, hasa mipakani kuwa na usafiri imara zaidi ili kudhibiti uingiaji na utokaji wa watu na bidhaa haramu katika nchi yetu.

SPIKA: Nilikwishakutaja Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, matatizo yanayotokea Masasi ni sawa kabisa na matatizo ya ndani ya Jimbo la Mlimba lenye kata 16, halina Kituo cha Polisi wala halina gari la Askari, hivyo kusababisha mahabusu kukaa muda mrefu kwenye kituo kidogo cha Polisi kilichopo pale *TAZARA*. Je, ni lini sasa na Waziri Mwigulu alishatembelea, Halmashauri tumeshatenga kiwanja na tuna baadhi ya matofali. Je, ni lini sasa Serikali itafikiria kuweka kituo cha Polisi Mlimba na kupata Askari wa kutosha ili kuwatawanya kwenye vituo ambavyo wananchi wamejitolea na tunakosa Askari kwa sababu hatuna mahali pa kuwaweka Askari kwa wingi pale Jimbo la Mlimba na hatuna kabisa usafiri na anajua?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli mazingira yale aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge nimeyashuhudia. Nilifika mazingira yale yanafanana kabisa na mazingira ya Jimbo la Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli.

Mheshimiwa Spika, niseme tu Serikali inatoa uzito mkubwa kwenye maeneo kama hayo ambayo jiografia yake inalazimisha tuwe na usafiri wa kujitegemea ili kuweza kuwatengenezea mazingira mazuri Askari wetu ya kufanya kazi. Kwa hiyo, tunaweka uzito kwenye jambo hilo la usafiri pamoja na kituo hicho kikubwa anachokisemea. Punde tutakapoanza kutekeleza bajeti yetu na *balance* itakapokuwa imeruhusu tutatengeneza hili la kituo, lakini na hilo la gari tutakapokuwa tumeanza kugawa magari tutaweka uzito mkubwa katika Jimbo hilo.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ina umri wa miaka 43 sasa, licha ya kukosa nyumba za Askari walioko kule hata kituo cha Polisi hatuna, umri wa miaka 43. Ni lini Serikali itatujengea Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Liwale, kuondokana na adha ya kupanga kwenye nyumba ambayo wamepanga, nyumba yenye nayo ni mbovu? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu sana la watu wa Liwale, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni sahihi. Liwale pia, inahitaji kuwa na kituo, niliwahi kuongea na Mheshimiwa Mbunge tukakubaliana kwamba, mara litakapomalizika Bunge twende pamoja mimi na yeye Jimboni kwake tuweze kushirikiana tuone jinsi gani tunawenza tukafanya ili kuharakisha huu mchakato wa ujenzi wa kituo hiki

ikiwezekana kwa kuanzia kuwashirikisha wananchi na wadau mbalimbali wakati tukisubiri jitihada za Serikali za kukamilisha ujenzi wa kituo hiki zitakapokuwa zimekamilika. Kwa hiyo, ahadi yangu na Mheshimiwa Mbunge kama tulivyozungumza iko pale pale. (*Makof*)

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo ni la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, linaulizwa na Mheshimiwa Devotha Mathew Ninja, Mheshimiwa Devotha Tafadhalii.

Na. 464

Ahadi ya Serikali Kutaifisha Mashamba Yasiyoendelezwa

MHE. DEVOTHA M. MINJA aliuliza:-

Serikali iliahidi kutaifisha mashamba makubwa ya uwekezaji yasiyoendelezwa:-

Je, mpaka sasa mashamba mangapi yametaifishwa?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Ninja, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Morogoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua dhidi ya wamiliki wote wa ardhi nchini ambao wameendelea kukiuka masharti ya umiliki yaliyomo katika Hati Miliki walizopewa. Kwa upande wa mashamba, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015, Disemba mpaka sasa imebatilisha miliki za mashamba 32 yenye ukubwa wa jumla ya ekari 67,393.6, Mashamba haya yapo katika Halmashauri za Kinondoni, Temeke, Kilosa, Mvomero, Morogoro, Iringa, Kibaha, Busega, Muheza, Lushoto, Bukoba na Arumeru.

Mheshimiwa Spika, mbali na mashamba hayo Wizara yangu imeendelea kupokea mapendekezo ya kubatilisha miliki za mashamba yasiyoendelezwa kutoka kwenye Halmashauri mbalimbali nchini, zikiwemo Halmashauri za Wilaya ya Tarime, Serengeti na Mkinga ambapo taratibu za ubatilishaji wa mashamba hayo zinaendelea kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Halmashauri zote nchini ambazo zimebaini kuwepo kwa mashamba yasiyoendelezwa au mashambaporu katika maeneo yao kuendelea kuwahimiza Maafisa Ardhi wa Wilaya zao kutuma ilani za ubatilisho au ilani za utelekezaji ardhi kwa wamiliki wa mashamba hayo kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Sura 113 na kuwasilisha mapendekezo ya kubatilisha miliki za mashamba hayo katika Wizara yangu ili taratibu za kuyabatilisha zikamilishwe kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Mheshimiwa Devotha Minja, swali la nyongeza.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nilitegemea Waziri angeniambia kwa sababu kutaifisha ni suala lingine na kuendeleza ni suala jingine, kwamba hizi ekari zaidi ya elfu 67 ambazo zimetaifishwa Serikali hii imeziendeleza vipi? Sasa maswali yangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kumekuwa na matumizi mabaya ya hii sheria ya kutaifisha mashamba. Wapo watu ambao walikuwa wakimiliki mashamba kihalali na wana hati, lakini wamenyang'anywa mashamba hayo. Wapo watu ambao walishinda hata kesi Mahakamani, lakini mashamba yao wamenyang'anywa. Ni lini Serikali hii itaacha uonevu kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wananchi wa Kata ya Tungi, eneo la Kiyegeya katika Manispaa ya Morogoro tangu mwaka 1984 walikuwa wakimiliki mashamba ya Tungi Estate, lakini mwaka 2014 wananchi wamenyang'anywa mashamba yale kwa maana ya kuachia ujenzi wa *Star City*.

Kwa kuwa, Serikali mpaka sasa haina lengo la kuanzisha mji ule wa *Star City*, lakini vilevile mpaka sasa Serikali haijalipa fidia. Naomba kufahamu ni kwa nini Serikali isiwaache wananchi hawa wakaendelea na shughuli zao za kilimo?

SPIKA: Mheshimiwa Devotha swali lako la kwanza una mfano wowote? Maana umetoa kama tuhuma tu kwamba Serikali inanyang'anya watu mashamba, wapi, ili Waziri aweze kukujibu *specifically*?

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko na tumekuwa tukifutilia hata kwenye vyombo vya habari. Baadhi ya mashamba ambayo yanafutwa na wamiliki ambao wamekuwa wakilalamikia kwamba, walikuwa na mashamba hayo kwa muda mrefu, lakini wamenyang'anya. Kwa hivyo, naomba Waziri anayaafahamu vizuri, yakiwemo ya Mvomero, yakiwemo ya Hananasifu...

SPIKA: Basi kama mnafahamiana sawa. Nilitaka uniambie ni mashamba ya akina nani? Basi, Mheshimiwa Waziri majibu, tafadhali.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali hatujataifisha mashamba. Nilimsahihisha kidogo kwenye swali lake nikasema, yaani kwa Kingereza ni *revocation, revocations* iyo kutaifisha. Rais anaweza akayachukua mashamba kwa manufaa ya umma, lakini hajafanya hivyo. Haya mashamba yote tuliyochukua niliyoyataja ni yale mashamba ambayo waendelezaji wamekiuka sheria.

Mheshimiwa Spika, kila mwananchi anapopewa shamba au kiwanja lazima azingatie sheria na masharti aliyopewa kwenye hati yake yameandikwa. Kama amepewa shamba kwa ajili ya mifugo, lazima alitumie kwa mifugo na ali pe kodi stahili na aliendeleze. Kamishna ana uwezo wa kulipima uendelezaji wake kila mwaka ameendeleza kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, nataka kuku hakikishia mashamba haya niliyoyataja hayakutafishwa kama anavyosema Mheshimiwa Devotha, isipokuwa wenyewe mashamba haya na wana hati. Ukipikia Mheshimiwa Devotha shamba limefutwa maana yake lina hati, kumbe afutiwe nani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hawa watu wenyewe hati wamefutiwa kwa sababu, wamekiuka masharti ya Sheria ya Ardhi ya Mwaka 99, Sura 113, wakiwemo hao unaowasema, mimi siwajui, lakini hao ambao anafikiri tumewaonea, hakuna hata mwanchi mmoja ameonewa katika utekelezaji wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwahimiza wamiliki wote wa mashamba nchini, mtu ye yeyote ambaye ana shamba amepewa, lazima afuate masharti. Kama haliendelezi, kama halipi kodi stahili, shambapori, sheria itafuata mkondo wake. Sheria inaanzia kwenye Halmashauri husika, Afisa Ardhi husika anatoa *notice* kwa mhusika ya siku 90 ajieleze kwa nini hatua zisichukuliwe. Wengine hawa wote hawajibu hata *notice*, baada ya hapo Halmashauri inapandisha zoezi hilo mpaka kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na mimi nampelekea Mheshimiwa Rais anatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Devotha Minja jambo hili wakikusikia wenyewe Halmashauri zao watakushangaa kweli kwa sababu wao ndiyo wamefanya, Halmashauri hizi ndiyo zimeleta maombi ya kufuta mashambapori. Nasi tutaendelea kutekeleza hili jambo na ninawahimiza Waheshimiwa Wabunge mahali popote mtakapokuta mashamba yasiyoendelezwa, bila kujali ya nani, bila kujali siasa, bila kujali mashamba haya alikuwa anamiliki mkubwa gani au mtu gani, yaleteni kwa mujibu wa sheria na sisi tutachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu Shamba la Tungi. Shamba hili la Tungi ni la watu, linamiliikiwa kwa mujibu wa sheria, lina mmiliki halali. Nataka nimwombe tu kwa sababu, maelezo haya ni mengi, nimwombe Mheshimiwa Devotha Minja aende pale kwa Mkuu wa Mkoaa

atampa maelezo mengi kwa sababu, mimi mwenyewe nimeshakaa na timu ya Mkoa, hawa wananchi walipelekwa tu pale kulima wakati wa siasa ya Kilimo cha Kufa na Kupona, lakini walikuwa wanalima kwenye shamba lisilo lao.

Mheshimiwa Spika, pale pana hati ya mtu na Mkuu wa Mkoa amefanya jitihada sana, Mheshimiwa Dkt. Kebwe ya kuwatetea wale wananchi na wenyewe shamba wamewapa ardhi wale wananchi wa pale ili waweze kuendeleza shughuli zao kwa hiyo, jambo hili Serikali imeshalishughulikia.

Mheshimiwa Spika, lile la mwisho ulilotaka kuuliza ushahidi la Mvomero, anajua Mvomero kuna shamba limefutwa na naamini bado limefutwa na Mheshimiwa Rais ametimiza wajibu wake. Mashamba yote yaliyofutwa Viongozi wa Mikoa na Wilaya tunawaomba watupe mapendekezo namna bora ya kuyatumia katika Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, sisi hatuamrishi tunataka mashamba yaliyofutwa wayapange viongozi kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge na Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ili wananchi wale ambao wameyachungulia kwa muda mrefu na hawana nyenzo za mashamba ya kulima waweze kugawiwa yale mashamba. Kwa hiyo, kama kuna shamba Mvomero limefutwa, namwomba Mheshimiwa Murad na Viongozi wote wa Mvomero wapange utaratibu wa kutumia lile Shamba la Mvomero lilihofutwa.

SPIKA: Mheshimiwa Selasini, Mvomero shamba limefutwa, swali la nyongeza Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pia niruhusu nimshukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu nilimpelekea shida ya mpaka wa Kenya na Tanzania kule Tarakea, alikwenda kule amesaidia sana kuleta utulivu kule mpakani. Mheshimiwa Waziri namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana eneo la Holili, viwanja vimegawanywa hovyohovyo, vimechukuliwa kiholela kabisa na ni tatizo la miaka zaidi ya 10. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, akipata tena nafasi, kama timu yako inaweza kwenda pale kuangalia uhalali wa namna ambavyo vile viwanja vimegawanywa kwa sababu, ni tatizo ambalo limeshindikana, Wakuu wote wa Mikoa wamejaribu wameshindwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, majibu ya swali hilo la Holili.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA

MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikwenda Rombo, lakini tulikuwa na zoezi la kuangalia mpaka. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeamua kuweka mpaka wenye alama zinazoonekana kwa wananchi kati ya nchi ya Tanzania na Kenya, Wilaya ya Rombo ni Wilaya ya mpakani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kweli nilikwenda huko na nimekwenda mpaka Mkoa wa Mara na zoezi hili litazinduliwa na viongozi wa nchi hizi mbili hivi karibuni. Tumeweka mipaka ya alama mia mia, ili wananchi waweze kuona alama zile waweze kujua nchi yao ya Tanzania inaishia wapi. Kama tunavyojua kwamba, alama hizi zilikuwa zimewekwa kwa umbali wa kilometra elfu moja, mpaka elfu mbili, nyingine mpaka kilometra mia mbili mpaka mia tatu. Kwa hiyo, zilikuwa hazionekani na watu walikuwa wanaingiliana, wananchi wa upande mmoja walikuwa wanaingia upande mwингine bila kujua na wananchi wa upande mwингine walikuwa wanaingia.

Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa pongezi zake na tutaangalia hayo maeneo mengine, sina taarifa kamili hizo alizoniambia nitafurahi zaidi kama Mheshimiwa Selasini akiniandikia vizuri ili nipate *message* vizuri. Amezungumza

kwa haraka sana lakini kwa kadri tutakavyolielewa, tutalishughulikia. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, William Lukuvi kwa majibu hayo mazuri, naona Mheshimiwa Devotha Minja alivyojibowi akaridhika kabisa.

Tunaendelea na wageni tulionao, naomba niwatambulise wageni watano (5) wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni Viongozi wa CCM na Jumuiya za Chama hicho katika Wilaya ya Kigamboni Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana popote pale mtakapokuwa. (*Makofi*)

Wageni watatu (3) wa Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Viongozi wa Kwaya Kuu ya Kanisa Kuu la Anglikana, Mkoani Iringa wakiongozwa na Mchungaji Alex Malogo. Karibuni sana Waimbaji wetu kutoka Iringa Mjini. (*Makofi*)

Wageni wanne (4) wa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ambao ni Wajumbe wa Bodi ya Ruvuma Kwanza SACCOS kutoka Songea Mkoani Ruvuma karibuni sana. (*Makofi*)

Pia kuna wageni 12 wa Mheshimiwa *Engineer Gerson Lwenge* ambao ni Madiwani pamoja na kikundi cha Wakulima wa Parachichi kutoka Jimbo la Wanging'ombe Kata ya Makoga Mkoani Njombe, karibuni pia. (*Makofi*)

Wapo wageni watatu (3) wa Mheshimiwa Felister Bura, ambao ni waumini wenzake wa Kanisa la Waadventista Wasabato kutoka Kizota Jijini Dodoma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni wa Mheshimiwa Hawa Ghasia ambaye ni Diwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Mheshimiwa Ahmad Chingoda, karibu sana Mheshimiwa Chingoda. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wageni wawili (2) wa Mheshimiwa Venance Mwamoto, ambao ni Mheshimiwa Isdor Iyenge, Diwani Kata ya Mrafu na Ndugu Killian Mienzi kutoka Jimboni kwake Kilo Mkoani Iringa, karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (*TWPG*) ambaye ni Mchekeshaji, Ndugu Shafii Omary maarufu kama JK *Comedian*, ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni 18 wa Mheshimiwa Marwa Chacha, ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Sayansi ya Afya Kisare wanaotokea Wilayani Serengeti, Mkoani Mara, karibuni sana kutoka Mugumu. (*Makofi*)

Pia yupo Mgeni wa Mheshimiwa Oscar Mukasa ambaye ni rafiki yake kutoka Jimbo la Biharamulo Ndugu Kisula Gerald Yeyeye, karibu. (*Makofi*)

Wageni saba (7) ktuoka Shirika la *JHPIEGO* ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendeshwa, karibuni popote pale mlipo. (*Makofi*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Godfrey Mgimwa ambao ni Wachezaji wa timu ya mpira wa miguu ya wanawake ya Panama kutoka Mkoani Iringa, karibuni sana wachezaji wa Panama kutoka Iringa, mmependeza kweli. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi 32 kutoka Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala, Tawi la Dar es Salaam ambao ni wanachama wa UVCCM, tawi la chuo hicho. Karibuni sana Kampala *University*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Matangazo mengine niliyonayo ni pamoa na tangazo la Mheshimiwa Ngeleja ambaye anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge mnaoshiriki mazoezi ya *fashion show*, sebene na nyimbo kwa

ajili ya usiku wa *TWPG* leo mwendelee rasmi na mazoezi kuanzia saa saba Mchana. Kama mnavyojua siku ya *TWPG* itakuwa tarehe 22 Juni, 2018 ambayo ni kesho kutwa tu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote tuendelee kujijandaa kwa ajili ya siku hiyo muhimu sana.

Mheshimiwa Mama Margaret Sitta anaendelea nae kusizitiza kwamba Waheshimiwa Wabunge mara tu baada ya kusitisha shughuli za Bunge, saa saba Mchana mazoezi yanaendelea yale ya miondoko *catwalk* na vichekesho (*comedy*) katika Ukumbi wa Pius Msekwa ambapo Mwanamitindo Hadija Mwanamboka na mchekeshaji Shafii Omar '*Jk Comedian*' watakuwa na Waheshimiwa Wabunge watakaoshiriki kwenye maonesho ya siku ya hafla ya uchangishaji fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo bora vya mfano katika Majimbo 264 ya Uchaguzi nchi nzima. Waheshimiwa Wabunge mliokwishajlrorodhesha mnaombwa mjiotopeze wote.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Shally Raymond anasema leo Jumatano Tarehe 20 Juni, 2018, kutakuwa na Ibada ya Misa kwa Wakirsto Wakatoliki mara baada ya kuahirisha Bunge katika Ukumbi wa Pius Msekwa Ghorofa ya pili, aidha, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kushiriki Ibada hiyo au Misa hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, Kurugenzi ya Shughuli za Bunge inawataarifu kwamba Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa anaomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba leo tarehe 20 Juni, 2018 kutakuwa na kongamano kuhusiana na masuala ya VVU, UKIMWI kuanzia saa saba mchana. Kongamano hilo litafanyika katika Ukumbi wa Msekwa.

Vile vile kutakuwa na maonesho ya shughuli zinazofanywa na AZAKI mbalimbali katika kufikia malengo ya '90-90-90' ifikapo mwaka 2020. Maonesho hayo yatafanyika nyuma ya Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote tunaombwa kuhudhuria kongamano hilo na

masuala ya itifaki yatazingatiwa. Narudia tena Wabunge wote leo tarehe 20 Juni, kutakuwa na kongamano saa saba na itifaki inazingatiwa. Pia kuna kupima kidogo hasa wale wanaume wenzangu wale, ukishapima itifaki inazingatiwa. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunaomba Waheshimiwa ambao mlitoa ahadi zenu kwenye zoezi la kuosha magari siku ile katika Uwanja wa Jamhuri basi tunakumbushwa kutekeleza ahadi zetu.

Waheshimiwa Wabunge, jana tarehe 19 Juni, 2018 Mheshimiwa Peter Serukamba aliomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni 47(1) na kutoa hoja ya kuomba shughuli za Bunge ziahirishwe ili kujadili jambo la dharura kuhusu kitendo cha Maafisa wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuingia Bungeni na kufanya ukaguzi wa samaki kwenye kantini ya Bunge bila idhini ya Uongozi wa Bunge.

Baada ya kuridhika kuhusu udharura na uhalisia wa jambo hilo Kiti kiliruhusu hoja hiyo itolewe ambapo iliungwa mkono na kisha ikajadiliwa na baadhi ya Wabunge humu ndani, Mheshimiwa Naibu Spika akiwa hapa kwenye Kiti. Baada ya mjadala Mheshimiwa Serukamba alitimidisha hoja yake ambapo alipendekeza suala hiyo ipelekwe kwenye Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili wahusika waitwe na kuhojiwa kufuatia kitendo walichokifanya ambacho kimelidhalilisha Bunge kwa maoni yake.

Waheshimiwa Wabunge, katika uamuzi wa jambo hilo Naibu Spika alipokuwa hapa aliagiza kwamba Serikali itoe maelezo Bungeni leo tarehe 20 Juni, 2018, kuhusu jambo hilo na namna lilivyofanyika, kwa sababu hiyo sasa natoa nafasi kwa Serikali kwa maana ya Waziri husika kuwasilisha maelezo hayo kama jinsi ilivyoelekezwa na Kiti hapa mbele jana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namkaribisha Waziri Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Waziri wa Mifugo na

Uvuvi atupatie maelezo yake. Mheshimiwa Waziri karibu sana.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa ridhaa na maelekezo yako kutoa maelezo ya Serikali juu ya kilichotokea jana hapa Bungeni ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa shughuli za Wizara katika usimamizi wa rasilimali za nchi ambapo kwa bahati mbaya na kwa masikitiko makubwa utekelezaji huo haukuifuata taratibu za Kibunge.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo ya tukio liliyyotokea jana hapa Bungeni na kuliomba radhi Bunge lako Tukufu naomba kutoa maelezo yafuatayo ya utangulizi:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea na mapambano dhidi ya uvuvi haramu na biashara haramu ya mazao ya uvuvi hasa kwa samaki aina ya sato na sangara kutoka Ziwa Victoria. Mapambano haya yanafanywa kwa njia ya operesheni ambayo inaitwa '*Operation Sangara 2018*' inayoendelea katika maeneo mbalimbali ya Mikoa ya Mwanza, Geita, Mara na Simiyu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara inafanya operesheni katika Ukanda wa Pwani ijulikanayo kama *operation MATT* Pia *operation*nyingine nyingine inafanyika katika ukanda wa uchumi wa Bahari ya Hindi ijulikanayo kama *Operation Jodari*. Aidha, *Operation Sangara 2018* itaendelea katika Maziwa Makuu ya Tanganyika, Nyasa pamoja na Maziwa mengine madogo ya Rukwa na Manyara. Mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu na Mito.

Mheshimiwa Spika, *Operations* hizo zinafanyika kwa mujibu wa sheria ya nchi ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lbara ya 27(2) ambapo inasema na ninanukuu:

"Watu wote wanatakiwa na sheria kutunza vizuri mali na mamlaka za nchi na ya pamoja, kupiga vita aina zote za

uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa lao”.

Mheshimiwa Spika, aidha *operation* hizi zinatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015/2020, Ibara ya 27(p) ambayo inaelekeza Serikali pamoja na mambo mengine:

“(p) Kuendelea kupambana na uvuvi haramu ili uvuvi uwe endelevu na wenye tija.”

Pia katika kiapo cha ahadi ya uadilifu kwa Viongozi wa Umma ambapo ni pamoja na kulinda kwa nguvu zote rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Spika, *Operation* dhidi ya uvuvi haramu zinafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Uvusi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni ya Uvusi ya mwaka 2009. Sheria ya Uvusi wa Bahari Kuu ya mwaka 1998 na marekebisho yake mwaka 2007. Sheria ya Mazingira ya Na. 20 ya mwaka 2004 na Sheria ya Uhujumu Uchumi (*Economic Organize Crime Act. Cap 2000 Revised 2002 as Amendment as Act. No. 3 of 2016* na Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya 1994.

Mheshimiwa Spika, katika *Operation* Sangara 2018 ambapo ilianza Januari, 2018 hadi sasa jumla ya watuhumiwa 3,033 walikamatwa, samaki wachanga na wakubwa wasioruhisiwa kilogram 332,080, mabondo kilogram 5,723 makokoro 9,730, kamba za kokoro mita 578,178, mitumbwi 1,076, magari 141, pikipiki 125, engine 582 na nyavi haramu 545,336 zilikamatwa. Kuwepo kwa hali hiyo kunathibitisha kwamba uvuvi haramu na biashara haramu ya mazao ya uvuvi imekithiri katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, katika ukanda wa Pwani *operation MATT* inaendelea kufanyika ambapo hadi sasa mtandao wa walipuaji mabomu umesambaratishwa, mabomu ya milipuko 720, V6 explosive vipande 600, denominator 362, mbolea urea kilo 324, mitungi ya gesi 68, vifaa vya kuzamia jazi 252 na compressos 12 zimekamatwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na *operation* hii idadi ya milipuko imepungua kwa asilimia 88. Katika Ukanda wa Bahari Kuu *Operation Jodari* ya kupambana na uvuvi haramu inaendeshwa baharini na angani kwa kushirikiana na taasisi ya Kitaifa ya *Sea Shepherd Global*/kwa kutumia meli ya *Ocean Warriors* ya taasisi hiyo ambayo ukaguzi hivi sasa umedumu kwa miezi sita mfululuzo, kwa kutumia ndege aina ya Dunia 228 kutoka Serikali ya Mauritius.

Mheshimiwa Spika, kuititia *Operation Jodari* meli 22 zimekatwa kwa makosa mbalimbali ya uvuvi katika ukanda wa uchumi wa Bahari Kuu na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Kutokana na mkakati huu hadi sasa hakuna meli hata moja ya kigeni inayovua kiholela katika maji ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo za kupambana na kutokomeza uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi nchini bado kumekuwa na taarifa nydingi sana za utoroshaji kuuzwa na kupatikana kwa samaki wasioruhusiwa kisheria hasa samaki wachanga katika mabucha, *super market*, mahoteli, migahawa na masoko hususan katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuendelea na tatizo hilo Wizara yangu iliunda timu ya uhakiki ya kudhibiti hali hiyo ambayo inafanya kazi katika mikoa tajwa hapo juu, hadi sasa kumekuwa na mageti maalum kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa mazao ya uvuvi katika maeneo ya Singida na Shinyanga. Aidha, timu imekuwa ikifanya kaguzi za kushtukiza za mara kwa mara katika maeneo ya mabucha, *Supermarkets* mahoteli na migahawa na masoko pia katika vyombo vya usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, tarehe 19 Juni, 2018 nilipokuwa katika Mgahawa wa Bunge niliona samaki aina ya sato nikashuku kuwa walikuwa ni wachanga wasioruhusiwa kisheria. Ndipo nikamuagiza Katibu wangu katika uhakiki unaoendelea Wakaguzi wajiridhishe na samaki wanaouzwa katika Mgahawa wa Bunge baada ya kupata vibali husika.

Mheshimiwa Spika, wakaguzi walimhoji Mmiliki wa Mgahawa alikiri kuwa samaki hao ni sato kutoka Ziwa Victoria ambapo walibaini kuwa baadhi ya samaki hao ni wachanga kwani walikuwa na urefu chini ya sentimita 25 kinyume na Kanuni ya Uvuvi ya mwaka 2009 Kanuni ya 58(2)(b), nanukuu:

" Notwithstanding the provision of sub regulation one, a person shall not fish, land process or trade the Nile tilapia of fish locally known as sato, the total length of which is below 25 centimeter".

Mheshimiwa Spika, baada ya kukiri kosa mmiliki wa mgahawa huo Ndugu Daniel Lamba alitozwa faini ya Sh.300,0000 ikiwa ni faini kwa kosa hilo ambapo alizilipa kwa kutumia akaunti ya Wizara iliyopo Benki ya NMB na kupewa risiti ya Serikali na samaki hao samaki wasioruhisiwa waliondolewa katika mgahawa huo.

Mheshimiwa Spika, Ndugu Lamba aliwaonesha Wakaguzi duka alilonunua samaki hao kilo 100 lilitopo maeneo ya Mtaa wa Uhindini karibu na uwanja wa Nyerere Square na kufanya ukaguzi ambapo hawakukuta samaki hata mmoja. Hata hivyo, Wakaguzi waligundua maduka ya jirani na kubaini uwepo wa samaki wachanga katika duka la Ndugu Samweli J. Kamone na kumtoza faini ya Sh.200,000 na kulipa faini hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kwamba watumishi hao katika kutekeleza kazi hiyo waliingia eneo la Bunge bila kibali cha kuwezesha kufanya zoezi hilo kwa kutokujua taratibu za Kibunge na kwa kupima chakula kilichopikwa. Kwa sababu hiyo, Wizara inaliomba radhi Bunge lako Tukufu na wewe mwenyewe. Aidha, nasisitiza kwamba Wizara yangu haikuwa na lengo lolote la dharau kwa Bunge lako Tukufu na Ofisi ya Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa mara nyingine, naomba radhi kwa niaba ya Wizara yangu

kwa kutokufuata taratibu kwa za utaratibu wa ukaguzi katika eneo la Bunge lako Tukufu, pia naliomba Bunge lako Tukufu liendelee kuunga mkono jitihada za kulinda rasilimali zetu nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nafikiri mlinisikia nilipotoa maelezo yangu mwanzoni kuhusiana na hoja iliyotolewa na ilivyoenenda jana na hapa tulipofikia tumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo mazuri ambayo ameyatoa.

Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo, tuseme tu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu tunasikitishwa sana na kilichotokeea, Bunge la Tanzania siyo Bunge pekee duniani, ni sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa. Wenzetu wote watakaposikia kuna Waziri katika nchi fulani kama yetu na Maafisa wake aamefanya kilichofanyika, ni dharau ya hali ya juu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hata panapokuwa na kosa la jinai limefanyika katika eneo la *compound* ya Bunge, *RPC* anapaswa kunijulisha na Bunge siyo kazi yetu kulinda jinai, Bunge hatulindi wahalifu, lakini lazima tujulishane, lazima tuambiane, lazima tutaarifiane. (*Makofi*)

Mtu anaponunua samaki kilo mia moja (100), kwa akili ya kawaida watu wanunua samaki kwa kilo, watu hawanunui samaki kwa futi. (*Makofi*)

Halafu samaki mwenyewe kapikwa, ameshakuwa ni kitoweo, sasa hii sheria ya kupima vitoweo hii, inabidi hizi sheria tuzisome vizuri jamani. Hivi Watanzania sasa wawe wanafunga milango ndipo wale samaki? Yaani samaki mbichi aliyevuliwa huko, atafika Dodoma baada ya muda gani? Halafu awe *processed*, bado urefu wake ni huo huo na ameshapikwa na kadhalika?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, kibaya zaidi, haijalishi, wapimaji wenyewe hao watu wa Wizara wanapima wakiwa mikono yao haina hata *gloves*, chakula cha Waheshimiwa, mikono mitupu kabisa (*barehanded*) hivi wanapima, wanashikashika wale samaki. Si wao peke yao, wamealika na Waandishi wa Habari na watu gani, wamejaa zaidi ya 20 ndani ya jiko. (*Makofi/Vigelegele*)

Baada ya pale zikarushwa mitandao yote, yaani ni kama *mission* fulani ya kuliweka Bunge mahali ambapo hapastahili. Kwa hiyo, kwa kawaida Waheshimiwa Wabunge naomba mkubaliane nami, ukikasirishwa sana na jambo unasamehe, kwa hiyo tusamehe.

SPIKA: Ahsante sana, Katibu tuendelee.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

SPIKA: Tunaendelea, Katibu!

NDG. ATHUMAN B. HUSEIN – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019
na

Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Majadiliano yanaendelea, tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Bungara, Mheshimiwa Dkt. Sware.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili kutoa mchango wangu katika hoja iliyomezani kwetu. Kwenye kitabu cha Mpango

Hotuba ukurasa wa 15, mpaka 16, Mheshimiwa Waziri ameonesha changamoto tulizonazo ambazo zinatuletea mkwamo katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo zilizotajwa, zipo tano, na tatu kati ya hizo, ameonesha kwamba ni ukosefu wa fursa za ajira, changamoto katika sekta ya kilimo, akisema kuna uwekezaji mdogo, tija ndogo, kutegemea mvua, sambamba na mchango mdogo wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa. Pia kuwepo kwa wigo mdogo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani, ambao uwiano wa mapato ya ndani na Pato la Taifa ni takribani asilimia kumi na tano tu, ikilinganishwa na wastani asilimia kumi na saba.

Mheshimiwa Spika, niliposoma hivi, hizi kurasa za kwanza, nilitegemea kwamba huko mbeleni kurasa zinazofuata basi ni kuzigeuza hizi changamoto, kuwa *opportunities* (fursa). Sasa tukienda ukurasa zinazofuatia wanasema fursa, zipo, anakiri kwamba kuna nguvu kazi kubwa katika Taifa; halafu vikaishia hapo akaenda kuanza kuelezea mafanikio.

Mheshimiwa Spika, nilisikitika baada ya kuona hivi, kwamba ahhaa kumbe tunajua shida yetu ni nini, kwa hiyo kwa nini hizi changamoto zisiwe *reflected kwenye mipango yetu tunayojiwekea?* Kwa nini changamoto hizi zisiwe *reflected kwenye bajeti ambayo tutaitenga?* Ukiangalia mipango tuliyonayo linganifu na bajeti tunayoitenga haviendani. Mpango wetu wa Miaka Mitano wa Taifa na mpango wa mwaka mmoja mmoja kwa kila mwaka wa fedha na bajeti tunazositenga katika huo mwaka husika ni vitu vitatu tofauti. Hotuba ya mpango, hotuba ya bajeti, kitabu cha mpango, mapendekezo ya mpango havina uhusiano, ni kama vile vimeandikwa na taasisi tatu tofauti.

Mheshimiwa Spika, pia kuna mkinzano mkubwa sana kati ya sera na vipaumbele vyetu. Tunasema tuna Sera ya Serikali yetu ya Tanzania ni ya Viwanda. Viwanda hivyo haviwi *reflected kwenye mipango strategyni viwanda vya aina gani, sources za raw materials za hivyo viwanda ni vipi?* Mheshimiwa

usitingishe kichwa, kila kitu kimeandikwa kwenye vitabu, sijavitoa hewani. Ukiangalia pia na kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa letu, vivyo hivyo haiwi *reflected* japo inaonesha kwamba Kilimo kina *contribute* zaidi, nikisema kilimo, ni kilimo chenyewe, mifugo, uvuvi na mazao ya misitu; tunasema ina-*contribute* asilimia thelathini, kinachofuata ni asilimia kumi na tano kutoka sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Sasa tunatokaje hapa kwa sababu tuna maandishi ya tofauti tofauti? Nikawa nawaza shida ni watendaji, shida ni matamko ya kisiasa au kuna kitu cha ziada? Mfano tu wa haraka haraka labda kuna sintofahamu ya wafanyakazi katika Wizara husika inayohusiana na mambo yetu ya bajeti na mipango. Aidha, wafanyakazi hatuna *motivation* au kuna *hidden agenda* ambayo siielewi, kwa sababu kila kitu kiko wazi na Waziri mwenyewe amesema changamoto ni zippi zinazotukwamisha tusiende lakini hakuna *solution*, tunaruka hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu chetu cha Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano ilisemwa kwamba tutahitaji takriban trilioni mia moja na saba kwenye shughuli za maendeleo ili tuvuke, ikimaanisha kwamba Serikali yenyewe itakuwa inatoa trilioni 11.8 takribani na sekta binafsi zitachangia trilioni 9.6, jumla trilioni 21 kwa ajili ya shughuli za maendeleo ili tuweze kuvuka.

Mheshimiwa Spika, lakini bajeti hii inayoishia na bajeti inayokuja tumetenga tuu trilioni 11 na kwa ajili ya shughuli za maendeleo na ni *contribution* ndogo sana kutoka katika Sekta binafsi. Mwaka huu unaoishia kati ya trilioni kumi na moja tuliweza kutoa trilioni 5.12 tu. Kati ya fedha hizo za maendeleo, kilichotolewa katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ni asilimia 34. Tunaenda kujenga reli, kununua ndege na kadhalika, trilioni 1.7 zilitoka. Hizo zilizobaki sasa trilioni 2.43 ndizo zilienda kwenye sekta nyingine zilizobaki katika wizara nyingine. Cha kushangaza, katika hizo trilioni mbili zilizobaki, mifugo na uvuvi, hawakupata hata senti tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia sasa hiyo sekta ambayo ndio wananchi wengi tunasema wapo humo, *according to statistics* za nchi inasema inaajiri asilimia 66 lakini ninahisi ni zaidi ya hiyo asilimia 66.3 ya kaya zote nchini, ambao wanajishughulisha na shughuli za kilimo, mifugo, uvuvi na mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, tunasema kwamba kilimo huchangia kwa ujumla wake, asilimia 20 ya mauzo ya nje na kinakua kwa *pace* ndogo sana, haishangazi kwa ni nini kwa sababu hatujawekeza katika hii sekta. Mifano tu dhahiri ya nchi za wenzetu, mfano nchi ya Brazili, wenyewe wametoka, ni nchi ya nane kwa uchumi mzuri duniani. Hata hivyo walitokaje? Wali-*invest* kwenye kilimo hususan kilimo cha kahawa. Wali-*invest* kwenye kilimo cha kahawa na waka-*invest* kwenye viwanda ambavyo vinashughulika na shughuli za kahawa, ikainua sekta nyingine baada ya kufanikisha kilimo.

Mheshimiwa Spika, sasa leo hii Tanzania labda tuna shida ya kuwa na rasilimali nyingi mno ambazo zinatakiwa zijenge uchumi, kwa hiyo hatujui Tanzania inasimamia wapi. Tanzania uchumi wake unaendeshwa na nini, tukimwuliiza leo Waziri wa Fedha, Tanzania inaendeshwa na nini? *Is it* kilimo, kilimo chenyewe ambacho hatuja-*invest*? Ni utalii, madini au ni kitu gani? Leo hii ukiwafundisha watoto wa shule Tanzania inajivunia kwenye nini katika kuendeleza uchumi wake hatuvezi kusema.

Mheshimiwa Spika, kama sekta hiyo sasa, ambayo tunasema ndio inayoajiri watu wengi zaidi, yaani wananchi ndio wanayotegemea hii sekta imenyamaziwa kimya, mifugo na uvuvi imenyamaziwa kimya. Sana sana sasa hivi tuna sintofahamu ya jinsi ya kutoka kwa kudhibiti uvuvi haramu tena kwa kutumia njia ambazo si sahihi, za kuzidi *ku-frustrate* hawa wananchi wachache.

Mheshimiwa Spika, mfano tu, sawa tumewanyima fedha za kufanya shughuli za maendeleo, lakini sekta hizi; si kilimo, si uvuvi, si kwenye sekta ya mifugo, kuna upungufu

wa zile asilimia 50 ya wale maofisa wanaotakiwa wawaguse wananchi na kuwashika mkono kuinuka hapo walipo. Kwa mfano, Maafisa Ugani ambao ni muhimu sana waliopo ni elfu saba na kat i ya vijiji elfu kumi na tano na, wakati kila kijiji kilitakiwa kiwe na Afisa Ugani mmoja.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa tunatokaje tokaje? Hatuwezi kutoka tutakuwa kila siku uchumi uko mdogo, kila siku tunaletewa makablasha na maandishi ambayo hayaendi kufanya kazi. Sasa unajiuliza ni kwa nini, wakati kila kitu kiko *obvious* na tunaweza tukatoka hapa? Nia ya Serikali ni nini?

Mheshimiwa Spika, katika kutuchanganya pia sasa Serikali kwa hiyo hela kidogo iliyonayo na hatuoni mkakati dhahiri wa kulea hizi sekta ambazo zinaweza zikatutoa, sasa wanakuja na *proposal* ya kuweka fedha zote za Taifa hili katika Mfuko mmoja ilhali kuna mifano mingi ambayo inawakwaza Wananchi. *TRA* wanasema wanakusanya mapato lakini *literally* wanakuwa wanashikia wa sekta binafsi fedha zao. *TRA* inadaiwa bilioni thelathini na sita kutoka katika sekta ya sukari, hii sukari ya viwandani, ile asilimia 15, wamegoma kurejesha. *TRA* hawa hawa wanadaisha na Bodi ya Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) bilioni 14.8. *TRA* hao hao wanadaisha na *REA*.

Mheshimiwa Spika, *apart from* hayo madai wanayodaiwa ambayo hela sio zao nao wanazi-*claim* kama mapato na kudanganya Bunge lako kwamba in *totality* uchumi unakua, uchumi haukui, hizi ni hela za watu, Bod i ya Korosho wanadai bilioni themanini na moja, lakini in *totality* mwaka wa Fedha uliopita na huu wanawadai milioni mia mbili na, lakini wanaziweka kwenye Mfuko Mkuu na kusema kwamba mapato yameongezeka, lakini si mapato hizi ni hela walizokopa kwa watu wa Sekta tofauti tofauti.

Mheshimiwa Spika, kuna *issue* pia ya ucheleweshaji wa malipo ya watoa huduma, kama ni wakandarasi, na kadhalika. Mfano, *TANROADS* na *TBA* nchini wamekuwa

wana-delays za kulipa wakandarasi na watoa huduma mbalimbali. Kwa mwaka huu wa fedha unaoisha *TANROADS* na *TRA* wanadaiwa jumla bilioni mia tano themanini na saba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kidogo.

SPIKA: Malizia

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, sasa kwa mwenendo huu, kuna mchezo sasa hivi wa Serikali kupora mapato ya wengine kwa kusema kwamba tunawawekezea lakini hawayarejeshi, kuna mtindo wa kuchelewesha au kutokupeleka kabisa kwa wale wanaowadai Serikali. Sasa inasikitisha kwamba na changamoto zote hizi Serikali bado sasa inataka kurudi kwenye *Centralization System* na kuacha *Decentralization* ili tu kuficha ile aibu kwamba tuna shida ya fedha katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii haiwezi kututoa hapa kama hatuwezi kuleta mikakati mahsus ya kututoa hapa zaidi ya wao Serikali, kung'ang'ania mapato ambayo si yao ili kuficha tuu aibu kwamba tuna shida katika uchumi wetu. Naomba kama Serikali kama inataka kurudi kwenye *Centralization System* waache *D by D*, walete sheria hapa Bungeni ili tuweze kuja na mkakati wa kusema kwamba tumeshindwa huku tunataka kurudi huku kuliko kutuchanganya wananchi na Bunge lako kujua kwamba *direction* ya Serikali hii inaendajeendaje.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sware. Mheshimiwa Selemani Bungara, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne Mcemba.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa akili Watanzania lakini hatuwezi kuitumia sawa sawa. Pili, ninakushuru wewe leo kwa kutumia busara kwa kuwasamehe wale waliokuja kupima samaki kwa kutumia *ruler*; na ndivyo inavyotakiwa kwamba mzee kama wewe uwe na busara. Tuwasamehe watu kama hawa; hawajui walitendalo, wanasema watu wengine huko.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Waraka wa Maaskofu na Mashekhe, ili Serikali ya CCM irudi katika mstari unaotakiwa. Nawapongeza sana Mashekhe na Maaskofu, na Serikali muwe wasikivu myafuate yale waliyoyasema. Sisi wengine si Wachumi, sisi wengine wanasiasa. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema ili tuendelee tunahitaji vitu vinne, ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Tatizo ninaloliona mimi ni siasa safi na uongozi bora; hapa ndipo penye matatizo hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siasa yetu ya mfumo wa vyama vingi, siasa ambayo ilikuwa kama tungeitumia vizuri maendeleo yanepatikana kwa haraka sana. Hata hivyo, kutokana na uongozi wa nchi hii, ambao unatumia sana ubaguzi katika siasa zake nina wasiwasi hatutafika lengo tunalotegemea la maendeleo ya nchi hii. Sisi watu wa kusini tulikuwa nyuma sana kimaendeleo na ndiyo sababu Mkoa wa Lindi tuko *draw*sasa hivi CCMwanne Wabunge na CUF wanenye Wabunge ngoma *draw*; na kwa kuwa tuko wanenye kwa wanenye, mambo yako safi sasa hivi Mkao wa Lindi; upo safi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Mkao wetu wa Lindi mimi ndiye Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkao wa Lindi, mimi hapa ndiye Mwenyekiti; na tunafanya kazi vizuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu kwa upande mwingine lakini katika mambo ya ubunge mimi ndiye Mwenyekiti wake. Tunakaa, tunapanga kwa pamoja na mambo mazuri kabisa yanapatikana katika Mkao wa Lindi sasa hivi. Leo... (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Bungara Spika hana taarifa kwamba wewe Mwenyekiti. (*Kicheko*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, ndiyo nakupa taarifa hiyo ndiyo Mwenyekiti mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo kutoptaka na mchanganyiko huu wa *CUF droo* na CCM mambo mazuri wakulima wetu sasa hivi wanapata leo ufuta bei inauzwa Sh.2,750. Tunakaa pamoja na Waziri Mkuu mimi nikiwa Mwenyekiti hapa. Tunapanga, tunaongea, tukishamaliza; leo tumeanzisha jambo lingine jambo jipyaa. Siyo stakabadhi ghalani, ni malipo ghalani ya ufuta. Jana tumeuza Sh.2,750 kwa kilo, siyo CCM huo ni mpango wa Mkoa wa Lindi. Kwa kuwa tunakaa pamoja tunashauriana tunamkosoa; Waziri Mkuu hapo sivyo hapo siyo stakabadhi ghalani, tatizo wanunuzi hakuna. Sasa hivi tuna Wachina, tuna Wahindi basi aah mambo yanakwenda vizuri tunakaa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuna njama ya makusudi ya Serikali ya CCM, ya makusudi ya kuturudisha nyuma Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa makusudi na sisi hiyo hatukubali. Leo katika gesi tulikuwa tunapata asilimia tatu wanataka kutuchukulia, *service levy* wanataka watuchukulie. Halmashauri zetu zilikuwa zinapata asilimia 0.3, leo Mheshimiwa Dkt. Mpango anapanga mpango hela hiyo itolewe katika gesi ije katika Serikali Kuu ili sisi turudi nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, korosho! Serikali hawawezi kuhudumia korosho; tukapanga mpango wetu wa Kusini tuingiziwe fedha kwa mujibu wa sheria, *export levy* asilimia 65 irudi kule kwa mujibu wa sheria wakachukua, wakaweka, waaa. Bilioni themanini na moja ya mwaka 2017/2018 wamechukua wamekula na wana mpango sasa hivi walete sheria humu kwamba jambo lenyewe kabisa lisiwepo kabisa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakwambia sisi mpaka tarehe 30 kama hela yetu haikurudi tunakuomba Mheshimiwa Spika uje Mtwara kupokea maandamano ya wakulima wa korosho

wa Mikoa ya Kusini. Kwa sababu inaonekana Serikali ya CCM sawasawa na patasi haifanyi kazi mpaka igongwe. Kwa hiyo nakuomba Mheshimiwa Spika tarehe Mosi Julai, ufile Mtwara upokee maandamano ya wakulima wa korosho wanataka fedha zao. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Bungara kuna taarifa huko. Nilisikia taarifa eeh. Aaah basi endelea Mheshimiwa. (*Makofi*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, na utuelekeze isiwe kama mpima samaki, utuelekeze Mheshimiwa Spika, tunakupataje, kwa sababu maandamano ya vyama vyaa siasa yamekatazwa; maandamano ya Wabunge wa Mkoa wa Lindi na Mtwara kutaka hela zetu zirudi. Tunakwambia Mheshimiwa Dkt. Mpango. Tunamwambia Mheshimiwa Mpango fedha zetu atuletee kama hakutuletea tutafanya maandamano Wabunge wa Mkoa wa Lindi na Mtwara mpaka asubuhi na Mheshimiwa hivyo hivyo... (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Kuna taarifa Mheshimiwa Bungara.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, nipe taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Kakunda tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa msemaji anayeendelea kusema kwamba maandamano yanatakiwa yafanyike kwa mujibu wa sheria za nchi. Sasa kama ameshakamilisha utaratibu wa kisheria ndipo anaweza akayatangaza. Kama hajakamilisha hawezo kuyatangaza.

SPIKA: Pokea taarifa hiyo Mheshimiwa Bungara.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, taarifa yake butu. Namwambia Waziri kwanza mpaka tarehe 30 hela yetu watupe kama hawakutupa tunafanya maandamano, sasa una wasiwasi gani. Kama hakutupa tutafuata sheria zote na tunakuomba Mheshimiwa Spika uje kupokea maandamano ya Wabunge wa Mikoa ya Kusini kwa ajili ya Dkt. Mpango aidha atoe hela au ajiuzulu kama si hivyo; varangati lile la gesi linaanza tena Kusini. Varangati lile lile! *Wamandharaba nafsi la yabuki* (ajipigaye mwenyewe halii). Tunakuomba Mheshimiwa Spika utupokelee maandamano yetu, tunaanza upyaaa! Hiyo moja. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pili, Kiwanda cha Mbolea cha Kilwa kijengwe. Leo sisemi mengi, nawashawishi Wabunge wote wa Mikoa wa Kusini tuungane tupambane na Mheshimiwa Dkt. Mpango, huyu Mheshimiwa ana matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nasema bajeti hii iongezewe katika mifugo, kilimo, maji; waongeze fedha, kama sivyo nitasema hapana, mkiongeza katika habari hii mwaka huu kwa mara ya kwanza nitasema ndiyo. Wakiongeza bajeti katika kilimo, maji, uvuvi *Wallah* Mheshimiwa utaona ajabu leo ndiyoooo, lakini kama hamkuongeza katika kilimo, uvuvi, mifugo; hapana!

Mheshimiwa Spika, sisi tunapigiwa kura na wakulima. Wakulima wakisema hawakupigii kura Mheshimiwa Dkt. Magufuli hapiti; na mimi nawajua CCM wajanja kweli kweli, wanataka mwaka 2019 ndipo wakulima wawape, wafanyakazi wawape hela! Nheheheeee! Tuseme wanawafanya Watanzania wajinga, waseme mwaka 2019 eeh! Sasa hivi barabara safi ooooh, tunaongeza mshahara. Nasema wakiongeza tutawapiga, wasiongeze tutawapiga, wasitufanye sisi wajinga. Wajanja, wanatuuaua mwishoni, mshahara unaongezwa leo 2019, kuwafanya watu wapate tabu kwa miaka mitano mwishoni *akhlini!* Wanawazunguka Watanzania. Hizi siasa za hila hila na uongo uongo hizi ziishe mwaka huu; wakiongeza mwishoni tunawachukua tunawaweka, goli. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi leo sisemi mengi leo mimi sisemi mengi, mgeni rasmi ni wewe. Inaonekana Bunge wameshindwa kumdhibiti Mheshimiwa Dkt. Mpango, wanatuambia tutawaletea habari za korosho, sisi maandamano, tutaandamana kweli kweli mwaka huu... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Bungara muda wako umeisha.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Umenikubalia kuwa Mgeni Rasmi. (*Makofi/Vicheko*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Huyo ndiyo Mheshimiwa Selemani Bungara, Bwege. Nina rafiki yangu mmoja yuko Kilwa huko, sasa mwaka 2005 baada tu ya kupiga kura siku ile kanipigia simu nauliza jamani huko mmemchagua nani, aaah tumemchagua Bwege wetu! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mcemba.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie machache kwenye bajeti hii ya Wizara ya Fedha, lakini pia nichukue nafasi hii pekee kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anayoifanya. Uongozi wa Awamu ya Tano umejipanga na umejipanga kwa mambo mazuri matupu na yenye kufanikisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Dkt. Mpango, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Kijaji, nina sababu zangu. Nawapongeza kwa sababu muda hautoshi, lakini nampongeza na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyofanya kwenye Kamati ya Uongozi na Bajeti (Kamati ya Bajeti). Wamefanya kazi nzuri mionganoni mwa kazi nzuri kwa sababu kwa mara yangu ya kwanza

nimeweza kukaa nao meza moja na kuona wanafanya nini. Mheshimiwa Waziri amekuwa mtiifu na amekuwa kiongozi pekee kwa ufanuzi wa Wizara yake; hiyo nafasi nampongeza sana na amekuwa mtiifu sana.

Mheshimiwa Spika, niombe yale yaliyokuwa yamezungumzwa na maombi yaliyotolewa kwenye Kamati Mheshimiwa Waziri wa Fedha ayazingatie kwa sababu ni Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti. Sasa Kamati ya Uongozi maana yake Mheshimiwa Spika alikaa kwenye kitihicho na akabariki yale aliyokuwa ameyaahidi.

Mheshimiwa Spika, lakini la kwanza tulikuwa na ombila Kamati ya Bajeti kwamba ajitahidi katika utaratibu wake na mipango yake kuhakikisha kwamba hii Sh.50 iongezwe kwenye *petrol* na *diesel* kwa ajili ya maji. Mfuko wa Maji ni muhimu sana, kero yote hii, mazunguzo yote haya, yanajitokeza na lawama kwake ni kwa sababu hiyo kwamba bajeti ya maji ni ndogo, kama hataongeza basi atafute vyanzo vingine vya kuhakikisha kwamba anaongeza kwenye bajeti ya maji ili tuondokane na matatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo alikubali yeye mwenywewe kwenye Kamati ya Bajeti ni kupeleka fedha kwenye miradi ambayo wananchi wamejitokeza na wameifanyia kazi kubwa, miradi ya afya, maji, elimu ambayo haijakamilika. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mpango kwamba anapokuja sasa ahakikishe pesa zinapelekwa kwa wakati; hilo ndilo tatizo. Pesa zipo kidogo lakini haziendi kwa wakati. Kuna fedha ambazo zilitakiwa kukidhi bajeti iliyopita ya 2017/2018, lakini mpaka sasa kwa bahati mbaya au kwa makusudi au bahati mbaya hasa mimi nasema kutokana na makato kutokamilika kwa wakati basi amepeleka asilimia kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la *TARURA* na *TANROAD*, ile asilimia 30 kwa 70 bado *TARURA* wana kazi kubwa sana. Kwa hiyo, niombe kama hatapunguza kwenye *TANROAD*, basi ni vizuri akaangalia jinsi gani ya kuibeba *TARURA* kutoka kwenye vyanzo vingine ili angalau wapate

asilimia 40. Kwa sababu kwa mwaka huu mvua imeharibu asilimia kubwa ya miundombinu vijijini. Kwa hiyo barabara ambazo ni mbaya ni vijijini na barabara pia za mjini ambazo ni barabara kuu pia zimeharibika. Kwa hiyo, ingekuwa ni vizuri zaidi zote zikaangaliwa ili pesa ziende kwa usawa.

Mheshimiwa Spika, pia niombe pia kuhusu suala la kuongeza fedha kwenye Mifuko hii ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuna mfuko wa Rais wa Kujitegemea, *TASAF*na MKURABITA. Mheshimiwa Dkt. Mpango haya mambo sisi tumeyaona kwa sababu ni Kamati yangu ya Utawala na Serikali za Mitaa, mimi kama Makamu. Mifuko hii inafanya kazi vizuri sana. Mfuko wa Kujitegemea wa Rais unaweza ukasaidia ukaitoa hata ile milioni 50 ambayo inakwenda kila kijiji ingepitia kule. Tumejifunza mengi kwenye Mfuko wa JK ambao ulikwenda hovyo; sasa huu asikurupuke, asifanye haraka wala asikosee tena.

Mheshimiwa Spika, ziende kwenye *TASAF* na MKURABITA, kwa sababu uelewa sasa hivi wa wananchi kuhusu msaada wa Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ni mkubwa na sasa hivi wameenea nchi nzima mpaka vijijini. Kwa hiyo hawa tukiwalea nadhani Mheshimiwa Mpango ataondokana na hii kadhia ya milioni 50; kwa hiyo awe na utaratibu wa kupeleka fedha kwenye Mifuko hiyo. Pia hata asilimia 10; akiiveka vizuri hii asilimia 10 ikapita mle, wananchi wengi sana watanufaika, kwa sababu sisi tumekwenda moja kwa moja na Kamati yangu kwenye maeneo hayo na tumeona nini wanachokifanya, kwa hiyo mafanikio ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni suala zima la korosho, ila mimi sitaunga mkono kwa kuandamana, alishatupa ufanuzi wa deni hilo la korosho. Niiombe Serikali, mimi naweka msisitizo tu, niiombe Serikali ione jinsi gani ya kusaidia hili zao la korosho kwa sababu imekuwa ni kero, kero hiyo itatuathiri. Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza tunaona kama ana dhihaka lakini ana maana ya kulizingumzia ndani ya Chama cha Mapinduzi tatizo hili.

Kwa hiyo, hili tatizo ningeomba; kwenye Kamati alizungumzia kwamba kunatakiwa uhakiki, kuna mambo mengi wameyaona. Sasa yale ambayo wameshahakiki basi hizi pesa zipelekwe kwa wakati angalau *surphur* basi ipelekwe kwa wakati ili waweze kuokoa zao hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine la mwisho, Mheshimiwa Dkt. Mpango, nimejitahidi sana pamoja na Naibu wake nimepeleka taarifa nyngi sana za kuhusu *TRA* na kuhusu jinsi makusanyo ya Serikali yanavyopotea. Nimempelekea na nashukuru ndiyo maana nimesema ni watifu kwa sababu walitekeleza na waliona. Kwa hiyo, ningeshauri kuitegemea *TRA* peke yake si mbadala, ni vizuri tukajipanga tukaanzisha pia kitengo maalum cha kufuatilia hizi mashine za *EFDs*; kwa sababu watu kweli hawazitumii kwa neno la kusema kwamba mashine mbovu kwa sababu walishatangaza kwamba hizi mashine zinasumbua, kwa hiyo watu wengi wanachukulia *advantage* hiyo kwamba mashine ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vizuri sasa ufuatiliji uwe ni wa makini na zile barua ambazo wanaandika baada ya mashine kuharibika, nadhani sasa atoe mkakati maalum, atoe agizo maalum kusiwe na zile barua ambazo wameweka kwenye *lamination* wanazungumzia tu kwamba tumeambiwa wanabadilisha tu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Tanzania hii tena wameelimika ujanja ni mwingi, matapeli ni wengi, kwa hiyo tunapokwenda kwenye maeneo ya biashara mtu anapiga magoti kuomba kwamba apunguziwe. Kwa hiyo niombe Wizara ya Fedha, niombe kwa msisitizo mkubwa iendelee kutoa elimu ya maana ya ulipaji kodi kwa wananchi wote kwa kutumia *local radios* kutumia *TV*, vipindi maalum. Mheshimiwa Waziri asione ubahili wa kutumia vipindi maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka kuishauri Serikali ijitahidi itoe elimu, Watanzania hatukuwa na tabia hiyo ya kulipa kodi. Kwa hiyo wengi watakwepa kwa lolote

atakalotaka kwa ajili ya kuongeza mapato ya Serikali. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwa kazi nzuri anayofanya, ni wakati mgumu lazima atapata matatizo mengi, lakini lazima tujipange, tushirikiane katika ulipaji kodi na matumizi yake. Tukifanya hivyo vikaenda pamoja Serikali itakwenda juu na tutatoka hapa tulipo. Nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mwanne Mcemba, tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Richard Philip Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Japhary Raphael Michael.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo wameweza kufanya kazi vizuri na hasa Mheshimiwa Rais kwa sababu katika hotuba ya Waziri ameweza kutueleza mambo 10 ambayo kimsingi Mheshimiwa Rais ameweza kuyafanya vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na kwenye Kitabu cha Hotuba ya Waziri ya mapendekezo ya bajeti. Kwa upande wa mapato ya ndani amezungumzia kwamba kuna changamoto ambazo zimekuwepo au matatizo ambapo yamepelekea makusanyo yetu ya ndani hatufikii malengo katika utekelezaji wa bajeti ya 2017/2018 ambayo makusanyo ya ndani trillioni 19.9 lakini kwa mpaka Aprili tumekusanya trillioni 14 na *point*; ila ukichukulia miezi miwili mpaka kufikia mwezi Juni huu tarehe 30 tunaweza kufikia labda kwenye trillioni 16.

Mheshimiwa Spika, katika matatizo ambayo ameweza kuyaeleza la kwanza ni suala la ukwepaji kodi. Ningependa matatizo ambayo ameyaeleza yote, ukwepaji kodi, sekta isiyo rasmi ambayo haijaweza kurasimishwa, mazingira siyo rafiki, masuala ya *EFD*, udhaifu katika kuvuna maliasili na utegemezi wa mashirika ya umma, kiujumla haya

matatizo Mheshimiwa Waziri hajatueleza sasa haya matatizo anaenda kutatua kwa njia gani; ningeomba Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye suala kwanza la ukwepaji kodi. Siku zote Serikali imekuwa ikifuatilia na inaweka jitihada mbalimbali na hasa kwenye TEHAMA lakini bado kuna udhaifu sana katika maeneo hayo. Kwa hiyo tuombe Serikali iangalie kwa undani na kikubwa zaidi katika kuweza kudhibiti ni suala la kuwa na takwimu. Bila kuwa na takwimu huwezi ukaingia kwenye namna bora ya kudhibiti. Kwa mfano, tumekuwa tukipata malalamiko kwenye suala la *flow meter* kwa upande wa mafuta, kwamba kumekuwa na wizi sana na Serikali inapoteza sana mapato.

Mheshimiwa Spika, ningeomba hebu Serikali ijaribu kuangalia; kwa mfano tukiweka kwenye hizi kodi kwa upande wa mafuta twende kwa *capacity* ya meli kama inabeba lita 10,000 au lita milioni mbili basi tuchaji kodi kutokana na *capacityya* meli ambavyo imeleta hayo mafuta. Kwa hiyo mtu akibeba *under capacity* au *full capacity* itamlazimisha ajaze meli yote mafuta na sisi tu-base kule na kwa hiyo huu wizi unaotokea kwenye *flow meter* tutakuwa tumeukwepa.

Mheshimiwa Spika, tuna suala la sekta isiyo rasmi, hawa Machinga; mwaka jana Serikali illahidi kwamba itafanya usajili na vitambulisho watapewa na tuweze kuweka tozo; na Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba utekelezaji wake bado ni hafifu. Sasa je, ni lini itafanyika kwa haraka ili sekta isiyo rasmi iweze kuchangia katika mapato ya Serikali na tuweze kukidhi katika kufanya kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *EFD's*; mwanzoni kwa juhudzi za Mheshimiwa Rais aliwahi kuibua kwamba kuna watu walikuwa wanacheza na hizi *EFD's* ripoti haziendi *TRA*, wanatoa risiti na wanaiba pesa nyngi. Je, Serikali kwa sasa hivi ina mkakati upi wa kuhakikisha kwamba *record* za hizi *EFD's* zinasoma huko katika mitambo yetu ya *TRA* na ziko

sahihi? Je, wamewahi kulinganisha na kama kuna utofauti wowote umetokea nini ambacho kimeweza kufanyika ili kuweza kuboresha ukwepaji wa mapato?

Mheshimiwa Spika, kwenye halmashauri zetu tunatumia PoSlakini maeneo mengine hizi PoShazitumi ripoti katika mfumo, ni eneo lile ambalo tayari lina udhaifu. Kwa hiyo watu wanakusanya ripoti haziingii katika mfumo na wanasingizia *network*. Kwa hiyo hapa ni mahali ambapo tunapoteza mapato, tumeona kwamba tunadhibiti lakini bado tunatakiwa tuongeze juhudi katika kusimamia.

Mheshimiwa Spika, kuna udhaifu katika uvunaji wa maliasili, kama ni udhaifu je, ni udhaifu wa mfumo, tatizo ni mfumo au tatizo ni watendaji? Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri aje atueleze kuhusu haya udhaifu katika uvunaji wa maliasili na tumpoteza mapato, tatizo ni mfumo au tatizo ni watendaji.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mashirika. Waziri amesisisitiza sana kwamba Ofisi ya Hazina itasimamia mashirika ambayo Serikali inapata gawio. Niombe tu, kwamba juzi hapa Mheshimiwa Rais ameteua Msajili wa Hazina, basi *staff* waongezwe katika hiyo ofisi na kuweza kusimamia vyema ili Serikali ipate mapato ambayo hayatokani na kodi kutokana na hisa zilizokuwa kwenye makampuni au na mashirika mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vile vile ipo pia chini ya Kamati yako ya Uwekezaji wa mitaji ya Umma (*P/C*). *P/C* inahitaji ipate muda mzuri ambao wa tofauti ili kuweza kusimamia hayo mashirika 270 na tuweze kuishauri Serikali namna bora ambavyo itaweza kuongeza zaidi mapato yasiyotokana na kodi kutokana na hizi *dividend* za sehemu mbalimbali. Kwa hiyo tutaomba Kamati yako ya *P/C* uiwezeshe zaidi kwa muda ili iweze kufanya kazi ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna mabadiliko mbalimbali ya sheria ambayo Waziri aliyapendekeza katika hotuba yake. Kwanza kuna suala la tozo kwenye mvinyo *HS code*

2206.00.90. Mvinyo unaotokana na ndizi mwanzoni walikuwa hawa hawalipi, lakini sasa mapendekezo kwa lita moja watalipa Sh.200.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupiga vita suala la viroba watu wetu ambaao walikuwa wanatumia zaidi viroba wamehamia kwenye *banana wine* ambayo ni *very cheap* lakini imewekewa tozo ambayo ni kubwa ukililinganisha na kwa lita. Kwa hiyo, tutaomba Waziri uone namna ya kuipunguza hii badala ya Sh.200 iwe ndogo ambayo itaweza kukidhi, kwa sababu hizi *banana wine* zinazuwa Sh.2,000/= elfu moja na, tofauti na hizi zingine ambazo zinazuwa karibuni Sh.8,000/= mpaka Sh.12,000/=, Sh.15,000/=. Kwa hiyo hii tutaomba, nami naweza kuweka hata *schedule of amendment* tutakavyoweza kukubaliana.

Mheshimiwa Spika, kwenye mabadiliko ya kodi kuna suala la asilimia 10. Awali mapendekezo wameweka tu kwamba ni *youth and women*, lakini tulikuwa tuna vijana, wanawake na walemavu, kwa hiyo ilikuwa ni *four, four, two*. Kwa hiyo nitaomba hii ibadilishwe iendane na haya mapendekezo kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, pia tulifanya mabadiliko ya *produce cess*, mwaka jana kutoka asilimia tano mpaka tatu. Hii imepunguza sana mapato kwenye halmashauri zetu ambapo kwa mfano wanunuzi wa tumbaku halmashauri mapato yameshuka. Sasa kwa nini wasiangalie kwa sababu hajjamfaidisha mkulima na imefaidisha zaidi hawa wanunuzi wa haya mazao kama ya tumbaku.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika mabadiliko ya sheria hapa kwenye *Amendment of Local Government Finances Act, clause 35*; kwamba *corporate entity* ambayo *ina-produce* hizi *agricultural crops* na *hai-add value* ndiyo ambayo itaenda kulipa zile *produce cess*. Hata hivyo, tuna wakulima ambaao wengine wakubwa hawapo kwenye *corporate*, sasa hawa wanaenda kuchangia vipi katika kuweza kulipia mapato? Mtu anaweza akawa analima takribani heka 500, heka 200; sasa

hapa wamesema tu ni *corporate* na mtu hayuko kwenye *corporate*. Hilo eneo nalo ni bora kuangalia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri alizungumzia kuhusu *balance of payment* (Urari). Tumeona kwamba tunaagiza sana ngano nje na mafuta ya kula na tumeona kwamba katika hotuba yake mwaka mmoja wameweza kuongeza tozo kwenye mafuta ya kula ili tuweze ku-*promote* zaidi ukulima wetu wa ndani. Hata hivyo, naona tatizo hapa, kwamba ni jinsi gani tunawezesha na kuvutia wakulima wakubwa ambao watakuwa kwenye *economies of scale* na wanalima kwenye *large scale* ili tuweze kupunguza ulipaji wa fedha zetu za kigeni nje kwa ajili ya kuagiza malighafi za ngano na mafuta ya kula.

Mheshimiwa Spika, Jambo lingine ni kuhusiana na mambo mazuri ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya. Sisi Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Katavi umeme awamu wa tatu *REA* !!! bado mpaka tunavyozungumza hivi haujaingia; na tunamwangusha sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ya matatizo ambayo yametokea katika *tender* ambazo zimekuwepo, kesi inapigwa dana dana kila siku. Wananchi wetu wanaendelea kuulizia kuhusu huu umeme. Kwa hiyo niombe Serikali ifikie mahali sasa jambo hili liweze kukamilishwa na wananchi wakaweza kupata huduma ya umeme ambayo tayari tunaltegemea sana kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Richard Mbogo. Sasa Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ndiye anayefuata, changia tu hapo hapo. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Mjini.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuishauri Serikali katika Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2018/2019. Mwaka wa

fedha 2016/2017, nilipokuwa nachangia Hotuba ya Bajeti, nilisema kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ilivyokuwa na malengo yake inaonekana kama vile si Serikali ya CCM iliyokuwa inaongoza nchi hii kwa miaka yote. Nikasema kwamba kama watakwenda na *spirit* hiyo basi kutakuwa na mabadiliko tutakayoweza kuyaona.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa sababu niliamini kwamba watu wanaoiongoza Serikali ya Awamu ya Tano ni wale wale ambao wameongoza nchi hii kwa miaka yote tuliyonayo ya uhuru wa nchi hii, niliamini kwamba kusingekuwa na mabadiliko makubwa kama ambavyo inaonekana leo. Kwamba baada ya miaka mitatu bado hali ya maisha ya Watanzania yamezidi kuwa magumu sana, watu wameendelea kuishi katika shida na matatizo ambayo walikuwa wametegemea kwamba yangemalizwa katika Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii imeendelea kuwa *unpopular* kwa wananchi kwa siku zinavyoendelea kuliko hata ilivyokuwa huko nyuma. Kama hali hii itaendelea, kama uchaguzi utakuwa huru na haki 2020 nafasi yenu ya kushinda ni ndogo sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, angalau katika bajeti hii kuna harufu ya kuonesha kwamba kuna mambo wanataka kuyashughulikia ambayo ni ya msingi sana kwa Jamii na hasa katika eneo la kodi. Jambo ambalo tumelizungumza sana kama Kambi Rasmi ya Upinzani lakini wakati wote mmekuwa hamko tayari kusikiliza; na imekuwa ndio *traditional* ya Serikali hii. Kwamba kama jambo Mheshimiwa Rais hataamka alizungumze alitilie uzito basi wengine wakilishauri utekelezaji wake unakuwa ni mgumu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu Mheshimiwa Rais alikaa na wafanyabiashara angalau ukiangalia bajeti hii kuna vitu unaanza kuviona angalau vinaanza kutekelezwa. Hata hivyo, naona kama muda umechelewa sana wa kujenga *confidence* ya wafanyabiashara na wananchi kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, nashauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, Serikali ya Awamu ya Tano ijaribu kuondoa hofu wanayokuwa nayo wafanyabiashara na wawekezaji katika nchi hii; hakuna kabisa *confidence* ya kuwekeza. Mtu anapowekeza katika nchi hii uhakika wake wa kufanya biashara yake mpaka ifike mwisho umekuwa ni mgumu sana. Hana uhakika kwamba kesho kutaamka na nini, keshokutwa kutakuwepo na nini. Imekuwa kama vile kufanya biashara katika nchi hii ni kitendo kiovu. Mfanyabiashara anakuwa anaandamwa kwa kiwango ambacho ni cha kutisha, wala kufanya biashara tena katika nchi hii siyo baraka.

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani ni vizuri Serikali ibadilishe huo mtazamo, ifanye kwamba wafanyabiashara ni sehemu ya wadau muhimu sana katika Taifa hill na hasa kwa Serikali ambayo inategemea kodi. Iwafanye wafanyabiashara kuwa ni watu ambao ni kama ng'ombe unaowakamua ambao kimsingi unapaswa kuwalisha majani ili upate maziwa kuliko kufika mahali ambapo wafanyabiashara wanaonekana kama ni maadui katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, mtazamo kwamba wafanyabiashara wote ni wakwepa kodi si sahihi, wako wachache ambao wanaokwepa kodi lakini wafanyabiashara wengi katika nchi hii ya Tanzania hasa Watanzania kwa tabia zao na malezi yao hawapendi kusumbuana na Serikali katika suala la kodi; wanahitaji tu maelekezo sahihi, uongozi bora wa namna ambavyo wataongozwa katika kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri, kama ambavyo leo tunaleta *Tax Amnesty* katika maeneo mbalimbali, sheria za namna ambavyo tunafikiri kwamba riba na faini ambazo zimejilimbikiza angalau ziangaliwe. Tuangalie pia utaratibu ambapo kama mfanyabiashara amefanyiwa *auditing* na akaonekana kodi yake ni kiasi fulani apewe muda wa kuilipa taratibu. Haiwezekani mfanyabiashara apewe kodi ya milioni

mia moja umtake aliye wakati huo huo, anaipatia wapi hiyo fedha? *Unless* awe ni mwizi. Apewe muda taratibu hata wa miaka miwili, mitatu aliye hiyo fedha taratibu huku akiwezeshwa kuendelea kufanya biashara ili aweze kuisaidia Serikali na kuweza kusaidia mambo mengine ya maendeleo ya nchi hii yaende.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nafikiri ni vizuri sana Mheshimiwa Waziri akaliangalia hilo. Kukawa kuna roho ya huruma ambayo anatakiwa awe nayo na hasa kwa watu ambaao wame-*comply* kulipa. Wale ambaao wanakataa kulipa ndio waadhibiwe, lakini mtu amepewa *demand note* leo, baada ya siku mbili anafungiwa biashara yake, akaunti zake zinaanza kufungwa, fedha yote inachukuliwa na *TRA*, huyu mtu ana mikopo ya benki, ataendeleaje na biashara? Matokeo yake mambo yafuatayo yanatokea; wafanyabiashara wanakufa kwa presha, wanafilisiwa na matokeo yake na ninyi hampati chochote katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri sana tuangalie namna gani; kwa sababu Taifa hili la Tanzania hakuna njia nyingine ya kuishi zaidi ya kukaa vizuri na wafanyabiashara na wawekezaji, maana hawafanyi biashara wao, wanataka kujitahiditahidi kuanza kuingia kwenye biashara ambako kimsingi tulishatoka huko. *Automatically* naona kama wameshindwa na hawataweza kabisa kwa sababu tulishatoka huko kwa karne ya sasa hivi. Sasa watu ambaao wanaweza kuwasaidia ni wafanyabiashara na wawekezaji, wasaidieni hao watu. Nadhani hilo ni eneo la kwanza la muhimu sana, naishauri Serikali iliangalie kwa makini.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba hii wamesema mojawapo ya shida inayowasumbua ni sekta isiyo rasmi. Naamini bajeti hii waliyonayo *TRA* wana uwezo wa kukusanya kabisa hizi fedha, naamini kabisa, lakini inahitaji umakini katika kusimamia hili. Sekta isiyo rasmi lazima waigawanye katika makundi, sekta isiyo rasmi wanapoizungumzia kwamba ni Wamachinga tu siyo maana yake. Kuna watu

ambao wana maeneo kabisa wana-settlement vizuri, wako mahali pazuri, wanafanya biashara zao lakini hawajaingizwa kwenye mfumo wa kodi.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa tulilonalo ni kwamba tuna wafanyakazi wachache wa *TRA* ambao hawawezi kuwafikia hao wafanyakazi na wa bahati mbaya hawaoni umuhimu wa wajibu wa halmashauri zenu, hawataki kuzitumia halmashauri zao. Wangetumia halmashauri zao vizuri wakaamini kwamba halmashauri ni chombo muhimu cha kuwasaidia zingewasaidia ku-*trap* hawa wafanyakazi ambao wapo na hawana leseni lakini wanafanya biashara, wamejificha kwenye kivuli cha kutokuwa wafanyakazi wasio rasmi, leo wangekuwa wameweza kuongeza mapato yenu.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu kwa Serikali waongeze wafanyakazi wa *TRA*, kwa sababu ni *investment*. Kumwongeza mfanyakazi wa *TRA* si sawa na kumwajiri Mwalimu. Ni *investment* ya haraka ambayo pesa yako ipo ili waweze kufikia walipa kodi wengi. Sasa matokeo yake wanabaki na walipa kodi wachache ambao kila wakiamka ndio hao wanapambana nao.

Mheshimiwa Spika, walio wengi wamewaacha wako barabarani na bahati mbaya wamejifunika kwenye kigezo kwamba wao hawajafikia kwenye pato la mauzo ghafi ya milioni 20 kwa mwaka, kwa hiyo wanabaki hapo hapo wao hawaguswi, wala hawapo kwenye VAT, hawapo popote wapo tu. Siku zote wamezidi kuwapotezea mapato na wao hawawezi kulisukuma hilo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aongeze wafanyakazi wa *TRA* ili wafikie walipa kodi wengi ili waweze kufikia haya malengo waliyotarajia.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni suala la halmashauri. Mheshimiwa Waziri *a-revisit* uamuzi wa kuchukua vyanzo vyatya mapato vyatya halmashauri. Watajidanganya sana wakiendelea kuamini kwamba vyanzo vyatya mapato vyatya halmashauri vitasaidia Serikali Kuu. Serikali

Kuu wana vyanzo vingi, wazifanye halmashauri ziweze kukusanya mapato ili zitoe huduma kwa wale watu wa chini, watu wengi wako chini.

Mheshimiwa Spika, Rais atakuwa na nafasi na wao ya kupanga mambo ya *Bomberdier*, mambo ya reli na mambo mengine kwa sababu ya fedha zao za Serikali Kuu, lakini waache halmashauri zikusanye fedha kwa mambo yale ya maji, afya, elimu na kadhalika. Kama watajidanganya kwamba walioanza huko nyuma walikuwa hawaelewi wakaona wao wanaelewa zaidi wakaanza kururudisha kwenye *centralization* wanapotea katika mwelekeo. Nishasema hili narudia kulisema hili, hakuna kosa kubwa wanadolifanya Serikali ya Awamu ya Tano kama kuua halmashauri, kama kuua Serikali za Mitaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri katika nchi ambayo ina muundo mzuri wa Serikali za Mitaa, Tanzania ni mojawapo, lakini bahati mbaya katika nchi ambayo haitimizi wajibu wake vizuri kwenye Serikali za Mitaa, Serikali ya Awamu ya Tano ni ya kwanza. Sasa ni vizuri waone ni namna gani wanavirudisha vyanzo vya halmashauri ili ziweze kutengeneza barabara zake, halmashauri zitengeneze vituo vya afya, zitengeneze zahanati. Sasa wasipofanya hivyo kila pesa wakitaka tupige magoti kuwaomba mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, haya yalikuwa maoni yangu na ushauri wangu kwa Serikali. Nashukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Japhary, Mbunge wa Moshi Mjini ambaye alishakuwa Meya, kwa hiyo anatoa maoni yake kwa uzoefu wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Daimu Mpakate atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Rehani. Mheshimiwa Mpakate.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuongea siku ya leo kuchangia Hotuba hii ya Waziri wa Fedha. Jambo la kwanza napenda nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri kwa namna

ambavyo amejitahidi kukusanya mapato ya Serikali, mpaka kufikia Aprili amesema amefikisha asilimia 74.3. Kwa kweli amejitahidi sana kwa sababu nyingi ambazo tunaziona na nitazieleza mbele ya safari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo kuna mambo mawili, matatu ambayo inabidi tuyaongelee ili kuweka sawa na kumpa nguvu ili aweze kukusanya zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukweli uliokuwepo kama msemaji aliyetangulia alivyosema, vyanzo vingi vya mapato havikusanywi ipasavyo. Kwa mfano mdogo ambao upo kwa kila mmoja, kuna sekta moja ya kodi ambayo kwa asilimia kubwa haikusanywi, kodi hii ni ya *withholding tax*.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia wakazi wengi wa mijini zaidi ya asilimia 80 pamoja na sis Wabunge tulioipo humu ndani tunapanga nyumba ambazo tunaishi kwa sasa, lakini ukiangalia kiasi ambacho kinakusanya kwenye kodi hizi kama *withholding tax* kwa kweli ni kiasi kidogo sana. Hata wafanyabiashara walio wengi maeneo ya mijini, vibanda vyote vilivyopo mjini vinapangishwa na wafanyabiashara nao bado hawalipi *withholding tax*.

Mheshimiwa Spika, kwa jambo hili kama kweli *TRA* wangkuwa *very serious* wakiwa wana watumishi wengi wa kuwafuatilia kwa kila nyumba ambapo wapangaji wapo, kodi hii ikapatikana, naamini *gap* kubwa la kodi au mapato lingeweza kuzibwa kutokana na kodi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hiyo, tukiangalia taarifa yake, halmashauri zimeweza kukusanya mapato yake hadi Aprili kwa asilimia 64. Hapa kuna tatizo na tatizo hili ni kwamba usimamizi wa makusanyo ya Halmashauri umekuwa ni mdogo sana. Kwa kuwa makisio ya mapato ya Halmashauri yanatolewa na wao wenyewe, kwa hiyo vyanzo vile ambavyo wanavitoa wana uhakika wa kukusanya, ni kwa nini hawafikii kiwango cha kuridhisha ili kuleta mchango mzuri wa maendeleo katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili nilisikia mwaka jana Waziri mmoja alisema kwamba kuanzia mwaka wa fedha ujao halmashauri yoyote ambayo itashindwa kukusanya angalau kwa asilimia 80 ya makisio yake basi halmashauri hizo zijiandae kuondolewa. Je, mpaka sasa mpango huo ukoje, kwa inaonekana wanakisia kitu ambacho wanashindwa kukusanya?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Halmashauri nazo ziangalie wale wanaoshindwa kukusanya basi hatua ile ichukuliwe ili nafasi wapewe halmashauri nyingine zilizo kubwa kama Tunduru ambayo inaweza kukusanya zaidi ya asilimia 100 kutokana na makisio yake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nitaliongelea kwa uchungu mkubwa sana ni suala liliopo kwenye ukurasa wa 69 wa hotuba yake ambayo naona inahusiana na sheria zinazosimamia bodi za mazao. Naomba kwa ruhusa yako nisome kwa sababu ni mistari michache ili niweze kutoa mchango mzuri wa kuweza kumshauri Mheshimiwa Waziri namna ya kufanya. Amesema:-

"Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye sheria zote zinazosimamia Bodi za Mazao mbalimbali kwa lengo la kuwezesha ushuru wote unaokusanywa na bodi hizo kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kwamba mapato yatokanayo na ushuru unaotozwa kwenye mazao mbalimbali yanasmamiwa ipasavyo na kutumika kwa ajili ya shughuli zilizokusudiwa. Aidha, shughuli za kuendeleza pamoja na gharama za uendeshaji wa bodizitaghamariwa kupitia bajeti ya Serikali."

Mheshimiwa Spika, walivyoanzisha bodi hizi na mazao ilitokana na changamoto za uendeshaji wa kuendeleza mazao mbalimbali likiwemo zao la korosho na ndiyo maana zikaanzishwa bodi ili kusimamia mazao haya yaweze kuzalishwa kwa wingi na baadaye tuweze kupata fedha za kigeni kwa ajili ya kuendeleza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nitaenda kwenye zao la korosho; mwaka 2008 wadau wa zao la korosho walikubaliana kuanzisha *export/levy* ambayo katika makubaliano ikaundwa sheria mwaka 2009 na katika sheria ile kama tulivyoeleza siku za nyuma, tulikubaliana kwamba asilimia 35 ya mapato yaende Mfuko Mkuu wa Serikali na asilimia 65 irudi kuendeleza zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, huu ndio ulikuwa mkakati wa wakulima wenyewe baada ya kuona kwamba korosho zimekuwa zikiyumba na uzalishaji umepungua na tunamshukuru Mwenyezi Mungu tangu mwaka 2009 tulivyoanza kutumia sheria hii, uzalishaji umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka mpaka msimu uliopita tukapata zaidi ya tani 300,000. Katika tani hizo 300,000 Serikali ilikusanya zaidi ya bilioni mia moja hamsini na nne. Kati ya hizo, billioni mla moja na kumi zilitakiwa zirudi kwenye sekta; nina mashaka na mapendekezo haya.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali imeshindwa kurudisha kwa muda wa miaka miwili pesa hii ambayo tayari imezungumzwa kwa sheria kwamba asilimia 65 irudi kuendeleza zao husika la korosho, leo tunachukua pesa hii na tunabadilisha kwamba ziende moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu, nina mashaka kwamba yale yaliyotokea miaka miwili hii ambayo mpaka leo wakulima wa korosho tunalia yataendelea kujitokeza na hatimaye zao la korosho na mazao mengine yatauawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu dhamira na nia ya kuanzisha bodi hizi ilikuwa ni kulisaidia zao lenyewe ili liweze kuijendeleza baada ya kuonekana Serikali kupitia bajeti ya Serikali yenye imeshindwa kuendeleza haya mazao. Njia mbadala ilikuwa ni wakulima wenyewe kujinasua kwa kuanzisha hizi bodi na mifuko mbalimbali ambazo walianzisha tozo na ada mbalimbali zilizokubaliana na wakulima wenyewe ili kuendeleza mazao haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hiki kilio alichokizungumza Mbunge wa Kilwa ni kikubwa sana maeneo mengi ya Tunduru ambako wanategemea uzalishaji wa korosho kulingana na hii fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba, kwa kuwa haya ni mapendekezo, mapendekezo haya hayana tija kwenye bodi zetu za mazao kwa sababu zinaenda moja kwa moja kuua uzalishaji wa mazao na kama tulivyosema asilimia 20 ya *export* ya nje, pesa ya kigeni inategemea na mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia mwaka jana zao la korosho peke yake liliingiza zaidi ya trilioni 1.2, pesa za Kitanzania kwa ajili ya mauzo yake. Kwa maana hiyo, kama pesa zile hazitaenda kuhudumia zao kwa maana kwamba uzalishaji utapungua na hili lengo linalosema Serikali inaweza kupata fedha nyingi kutokana na hii pesa kupelekwa kwenye Mfuko Mkuu maana yake itashuka.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, kwa kuwa dhamira ni nzuri basi haya madeni ya nyuma yaende kuhudumia wakulima ili na sisi wanasiasa twende tukawaeleze wananchi wetu kwamba kuanzia mwaka wa fedha ujao tarehe 1 Julai mfumo utabadilika pesa hii itakuwa inapelekwa moja kwa moja Serikalini na kuamuliwa matumizi kwa njia ambayo amependekenza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana jambo hilo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mpakate.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Ooh! Ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Salum Rehani atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. SALUM M. REHANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye hotuba hii ya Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza mimi baada ya kuipitia bajeti ningeanza kwanza kujikita kwenye tasnia ya tafiti ndani ya nchi. Baada ya kupitia vitabu na maelekezo ambayo Serikali imesema kimaelezo tu itasaidia na kuhakikisha kwamba inatoa msukumo kwenye tafiti mbalimbali ili kufanya nchi iwe na vitu ambavyo vinaendana na uhalisia.

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza ambacho ninachokiona kwa kweli kimevunjisha moyo, Serikali haielekezi fedha kwa ajili ya taasisi za utafiti zilizopo nchini, pesa zinatengwa lakini haziendi. Sasa kama fedha haziendi matokeo yake yanakuwa haya; moja, kwenye upande wa kilimo suala zima la uletaji wa mbegu kutoka nchi za nje ndiyo unaotawala. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa inakuwa kama ni mpango maalum wa kuwawezesha makampuni ya nje yakawa yanaleta mbegu nchini kufanya biashara hizo na kuwaacha wazawa hapa ambao wana uwezo wa kuweza kuzalisha hizo mbegu kwa ajili ya mazingira ya nchi yetu wakishindwa kufanya chochote katika maeneo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumeona katika vituo ambavyo vinazalisha mbegu za mahindi tafiti zimeganda zaidi ya miaka miwili sasa hivi wale ambao walitaka kumaliza utafiti wao umekwama, lakini tunaona tatizo kubwa lililopo kwenye suala zima la mbegu za alizeti. Mbegu za alizeti tulizonazo ndani ya nchi hazifai, lazima tuseme ukweli. Ni asilimia 12 tu ya mafuta ambayo yanatoka ndani ya zile mbegu, kwa wenzetu mbegu hizi tunaziita ni makapi.

Mheshimiwa Spika, ukienda nje; leo hii kuna mbegu ambayo ipo Belgium ina uwezo wa kuzalisha mafuta mpaka asilimia 67, kitu ambacho kingeweza katuongezea mapato lakini kingeweza katuongezea mafuta mengi ya uzalishaji kama tungeweza kuwekeza katika haya maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali, katika hayo mazao ambayo ya mkakati ambayo yamekudiwa kuweza kuyawezesha maeneo ya kanda ya katì kuwa ni maeneo ya uzalishaji wa alizeti na kuwa ni sehemu ya mazao ya uchumi, kungekuwa na mtazamo wa aina yake. Kuiwezesha alizeti ya nchini inayozalishwa katika maeneo yetu hapa kutoa mafuta na si kuweza kutoa makapi au mashudu kama ilivyo hivi sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tukiweza kuwekeza hapa sasa hivi, tukifanya tafiti za kuzalisha mbegu ambazo zinatoa uwezo mkubwa wa mafuta itaweza kutusaidia kwa kiasi kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili...

SPIKA: Mheshimiwa Salum Rehani na mimi niweke mstari kabisa hapo, kwa kweli mbegu za alizeti zilizo nyingi hazifai kabisa, kweli kabisa. Tukipata mbegu nzuri za alizeti tunaweza kujitegemea kwa mafuta ya kupikia nchini hapa. Nilikuwa nakuunga mkono tu, endelea Mheshimiwa. (*Makof*)

MHE. SALUM M. REHANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pili, tunahitaji kuzalisha mawese. Mawese tuliyonayo katika nchi hakujawa na mwendelezo wa aina yoyote; Wizara ya Kilimo ipo, watafiti wapo na watu wamesema lakini mbegu zile za mawese za kwetu hizi kutoka Kigoma zimetumiwa kama *mother stock* kwa nchi mbalimbali duniani ambazo sasa hivi zinaleta mafuta ya mawese katika nchi yetu hii hapa. Kwa hiyo, sisi kama Watanzania tuliofa zile *mother stock* tunaletewa mafuta nchini hapa na yanauzwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Wizara ya Fedha na Waziri husika, atie msukumo kwenye *research* ambazo zitaweza kubadilisha tasnia ya uzalishaji wa mbegu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la mbegu za mboga mboga Tanzania imekuwa ni soko kuu la kampuni za Belgium, Uingereza, Switzerland na nchi nyinginezo, hata

Kenya, kutuletea mbegu za aina mbalimbali hapa, nyingine zikiwemo za *GMO* ambazo zinahatarisha na kuongeza kiwango cha kansa kwa mazao ambayo wanakula wananchi wetu hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wito wangu ni kwamba tuondokane na hii hali, tuweze kuwa na uwezo wa kuzalisha mbegu ambazo zitakubaliana na mazingira yetu na mbolea na udongo tuliokuwa nao na kuwafanya Watanzania waweze kufaidika na kilimo kilichopo nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwenye utafiti safari hii Tanzania tumeathirika karibu hekta 30,000 kwa *American worm* au viwavijeshi vya Amerika tunakiita. Hiki kiwavi jeshi kipyä kilichokuja hivi karibuni na matokeo yake kuingia tu Tanzania, tumeona athari katika maeneo ya Chemba, Mikoa ya Dodoma, Manyara, Kaskazini kote kwa ujumla, Tanga na maeneo mengine. Sasa wadudu wale au wale viwavijeshi wa aina ile tusifikiri kwamba wamemalizika. Wale sasa hivi mayai wametaga yapo, kama safari hii tulipata athari ya hekari 30,000 mwakani tutarajie zaidi ya hekari laki moja ziaathirika na *American worm* wale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wito wangu ninachokiomba tuiwezeshe *TFDA* na taasisi hizi ambazo zinaweza kushughulika kwanza na udhibiti, upatikanaji wa dawa na mafuta kwa ajili ya kuweza kuwaangamiza hawa wadudu; ziwepo fedha *standby* ili ikitokea *outbreak* ya kile kitu tuweze ku-harm kwa nguvu zote kuliko kwamba mnamatufuta Waziri wa Kilimo baada ya athari kuwa imeshatokea, wale wadudu wakiingia siku moja, mbili tatu tayari wameshamaliza maelfu ya heka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wito wangu ni kwamba tuwezeshe taasisi hizi za utafiti ambazo zinaweza kututengenezea dawa maalum, maana mpaka hivi sasa dawa tunazochukua tunachanganya tu. Hatujawa na dawa maalum kwa ajili ya kuangamiza viwavijeshi vya aina hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uwezo wa kutengeneza hizo dawa tunao, wapewe wataalam hiyo kazi tuingie maabara ili tutengeneze dawa ambayo itaweza kuwasaidia Watanzania na kuondokana na hili janga. Safari hii athari kubwa imeonekana kwenye mahindi lakini wadudu wale wanakula miche au majani ambayo yana siku kuanzia nne, saba mpaka 25. Vile vile wanakula mpaka ile *stem*, ule mmea wenyewe wanatoboa ndani katikati pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uwezo wake ni mkubwa tofauti na viwavijeshi wale wa zamani ambao tunaita *African worm* ambao wale uwezo wao kula hawazidi majani ya siku saba. Kwa hiyo, mazao kama maharage, njegere, kunde na hata mazao mengine madogo madogo ya mtama tujiandae kwamba yanaweza kuangamia kama hatukuchukua tahadhari ya mapema tuka-*harm* hiyo hali na kuinusuru nchi na kupata janga la njaa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wito wangu kwa kweli hizi fedha zilizokuwepo ziwekwe *standby* kwa kusaidia eneo hili na fedha hizi zilizokuwa *allocated* ziende, zisiwe nadharia tu za kila siku.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu suala zima la soko la bidhaa zetu. Sisi Tanzania tunazalisha na safari hii *projection* ya uzalishaji tunaweza kuwa na *excess* ya mazao zaidi ya tani milioni saba, hayo yamo ndani ya maeneo yetu. Hata hivyo suaona katika mpango huu kwamba nchi imejipanga vipi kukabiliana nah ii ziada ya mazao ambayo yatakuwa katika maeneo yetu; lengo ni kuwasaidia wakulima wetu. *NFRA* pamoja na Bodi ya Mazao Mchanganyiko uwezo wake ni mdogo wa kununua haya mazao na tumeona athari iliyotokea mwaka jana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, vile vile ukanda wetu huu wa Afrika Mashariki na nchi nyinginezo za *SADC* watu wamezalisha, kwa hiyo yale masoko ambayo tulikuwa tumeyatamani kwamba tungeweza kuwapelekea majirani zetu hayapo. Kwa hiyo nchi kama nchi iijiandae sasa kukabiliana na *surplus* ambayo itatokea katika uzalishaji

ambao watu wamezalisha ili tuweze kupeleka mazao yetu nje zaidi na kutanua wigo wa kuwaongezea kipato wakulima wetu hapa nchini. (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Mheshimiwa Rehani muda wako umeisha.

MHE. SALUM M. REHANI: Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Salum Rehani, inaelekeea wewe ni mkulima mtaalam kabisa. Nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Hussein Bashe utafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kumaliza mwezi Mtukufu wa Ramadhan na sasa tumeanza mwezi wa Shawali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru wewe na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mlionipa wakati nilivyopata msiba, nawashukuru sana na nathamini *support* yenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa maneno yafuatayo; Taifa lolote linapopanga bajeti linatengeneza *instrument* ambazo zitatumika kuisaidia bajeti hiyo kuweza kutekelezwa na wakati huo huo kuchochaea uzalishaji na kuisaidia Serikali kukusanya kodi yake. Kwa dhati kabisa, ni mara chache sana nimepongeza Waziri wa Fedha na mimi kwa dhati kabisa safari hii nimpongeze kwa *measures* alizochukua kwenye *fiscal/hasa* za kikodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza aliyoifanya ya kikodi ni maamuzi ya Waziri wa Fedha kutoa *amnesty* ya kipindi cha miezi sita kwa watu wanaodaiwa kodi, riba na

penalties kwa wafanyabiashara, hii ni taswira njema. Wafanyabiashara wengi wamekuwa na malimbikizo na kumekuwa na kesi nydingi za kikodi katika *Tax Tribunal*/ambazo wengi wanapambana na Serikali kupinga *either penalty/ama interest*, Waziri ametoa *amnesty*, kwamba watu wanaodaiwa kodi anawasamehe riba na *penalty* kwa kipindi cha miezi sita.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja kufanya *wind-up* naomba atoe *flexibility* ya kumpa *Commissioner General* wa *TRA* kwa sababu ndiye yaliye kwenye *daily operations* aangalie pale ambapo mtu anapokuja na *payment plan*, *either* ni ya mwaka mmoja, inategemea anadaiwa shilingi ngapi ili waweze kumpa hiyo *amnesty* isiwe *restricted* ndani ya kipindi cha miezi sita.

Mheshimiwa Spika, ye ye mwenyewe anafahamu *TRA* inadaiwa na wafanyabiashara hawana haki ya kudai *interests*, hawana haki ya kukupiga *penalty*. Kwa hiyo kama wanavyosema Wazungu, *scratch my back I scratch yours*, ameonesha *good gesture*, nakuomba u-extend hii *amnesty* ili Mtendaji Mkuu wa *TRA* aweze kufanya maamuzi kutokana na hali halisi ya mfanyabiashara huyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka niseme, wafanyabiashara na *it is natural*, kutumia *loopholes* za kisheria kutokulipa kodi na hii siyo dhambi na Serikali inafanya jithada ya kuboresha sheria zake. Waziri amekuja na Mfumo wa *ETS*. Moja ya maeneo ambayo wafanyabiashara hutumia nafasi ya ku-*avoid* kodi ni kwenye *VAT*. Eneo hili liko *connected* na *production*.

Mheshimiwa Spika, nimesikia mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, nami nataka nimwombe Waziri, *cautions* zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge juu ya mambo haya, juu ya hii Kampuni inayoitwa *SCIPA*, zifanyie kazi. Hata hivyo, *practice* na *studies* zinaonesha maeneo ambayo hii Kampuni ya *SCIPA* imewahi kufanya kazi kumekuwa na *positive result*.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo tunajua kwamba wana kesi Morocco ama wamekuwa wana tuhuma ya rushwa, suala la rushwa ni suala la watu. Kama mfumo utaruhusu watoe rushwa ili waweze *ku-yield more, it is our weakness*, lakini kama mfumo wao huu utatusaidia kufanya *production count*, kama mfumo wao huu utatuongezea mapato; nimwombe Mheshimiwa Waziri tunapokuja mwaka kesho ambapo atakuwa na miezi sita ya utekelezaji wa bajeti atuletee taarifa ya *performance* ya hii kampuni, imetuongezea mapato kwa kiwango gani na kama haijatuongezea mapato aweze kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwa na hofu kwa sababu *let us accept the reality*, wao wana *patent right*, wao ndio wana teknolojia, sisi tunahitaji huduma yao; tuhofie kwa sababu walitoa rushwa nchi fulani? Kama waliwapa watu rushwa *it is their problem* na sisi watu wetu wakipewa rushwa *it is our problem*. Sisi tunahitaji huduma tuangalie *mechanism* ambayo *we can yield more* kwa mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuongea, ukisoma taarifa hii ya uchumi ya Wizara ya Fedha kuanzia ukurasa wa nne mpaka wa saba, Waziri kaonesha *key economic indicators* ambapo jibu la *failure* zote hizi tulizozitaja ni sekta mbili; sekta ya kilimo na ya mifugo. Waziri ameonesha uzalishaji wa viwandani umeshuka kutoka asilimia 7.8 mpaka 7.1; biashara imeshuka kutoka asilimia 6.7 mpaka 6; malazi na huduma za chakula kwa maana ya hoteli na akinamama ntilie imeshuka kutoka 3.7 mpaka 3.2; shughuli za fedha na bima zimeshuka kutoka 10.7 mpaka 1.9; na hii ni *analysis*ya 2016/2017, ni taarifa ya hali ya uchumi. Shughuli za sanaa zimeshuka kutoka asilimia 8.6 mpaka asilimia 7.6; shughuli za kaya binafsi (*household activities*) kwa maana ya kuajiri wafanyakazi wa ndani, walinzi na nini zimeshuka kutoka asilimia tatu mpaka 2.7.

Mheshimiwa Spika, hizi *indications* zote ukienda kwenye mapato ya Serikali tuna-project kupungua kwa mapato yetu ya ndani kwa asilimia 10. Tafsiri yake ni moja tu,

kwamba *purchasing power* ya watu wetu kwa ajili ya kununua bidhaa, kufanya shughuli za kibiashara, zimeshuka.

Mheshimiwa Spika, sasa *what is the solution?* Nami nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwa mara ya kwanza *priority* yake ya bajeti ya mwaka huu ni kilimo, kwa mara ya kwanza. *Solution* ni ku-*invest* kwenye *agriculture*. Waziri kwenye *tax measures* alizoweka safari hii ametoa *corporate tax incentive* ya 20 percent kwenye viwanda vinavyozalisha mazao ya mifugo kwa maana ya *leather sector* na dawa lakini ni viwanda vipyta. (*Makofu*)

Mheshimiwa Spika, tuna viwanda saba katika nchi yetu vinavyozalisha mazao ya ngozi na viwanda hivi havifanyi vizuri. Kwa nini; sababu kubwa ni mbili. Sababu ya kwanza ni *export levy* ya 10 percent, kwamba Mtanzania aki-*process wet blue* ndani ya nchi yetu kuiiza nje anachajiwani *export levy* ya 10 percent, kwa nini? Wakati *competitors* wote, kwa maana ya ukanda wetu wa Afrika Mashariki hawachajiwani 10 percent ya *export levy*. Ushauri wangu kwa Waziri wa Fedha; tufute 10% ya *export levy* kwenye *wet blue*.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa pili kwenye Sekta ya *Leather*; sisi tumeweka 80 percent ya kodi kwa ajili ya *ku-export raw*, lakini unapoweka *export levy* ya 80 percent kinachotokea katika maeneo yetu ni jambo moja; bei ya raw nje ni nzuri, kwa hiyo wanachokifanya wafanyakishara na Wizara ya Fedha inajua na *TRA* inajua; wafanyakishara wasiokuwa waaminifu wanachukua ngozi zetu *raw* kwenye *container* ya 40 feet wanaweka just 10 percent ya *wet blue* wana-declare ni *wet blue* wakati wame-*export raw*, matokeo yake Serikali inakosa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika hili; *ban export* ya *raw*, aite viwanda vilivyopo vinavyozalisha ngozi ndani ya nchi yetu; na Mheshimiwa Waziri Mwijage anavijua, a-sign nao *performance agreement*, aondoe *export levy* ya 10 percent, *ban export* ya *raw*. Tunazalisha vipisi milioni nne. Kuna kiwanda kimekuja Tanzania kutoka Ethiopia, ni Wachina, wameweka *investment* yao pale kwenye *EPZA*

Bagamoyo, wanaomba leo kupewa haki ya ku-*import* ngozi *raw* kutoka Ethiopia kwa sababu wao uzalishaji wao kwa siku ni vipisi 30,000, hawavipati ndani ya soko letu *because of smuggling*. Kwa hiyo ushauri wangu; ili tuweze ku-*create value* kwenye mazao ya mifugo, achukue hatua hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, nimeona ametoa *exemption* ya VAT kwenye mashudu ya soya; hatukamui soya, sisi tunakamua alizeti, tunakamua pamba, aweke *VAT exemption* kwenye mazao ya pamba, kitatokea nini? Mifugo yetu na kwenye taarifa hii ya hali ya uchumi uzalishaji wa nyama na *consumption* ya nyama imeshuka kwa asilimia 14. Ushauri wangu huu ni kwamba Watanzania wataingia kwenye *feedlotting*.

Mheshimiwa Spika, leo ili uweze kumchinja ng'ombe, hawa ng'ombe wetu wa Kisukuma, Kigogo na Kinyaturu, ili umchinje uuze nyama yake *technically* anatakiwa achinjwe ng'ombe mwenye miezi 18 *maximum* miezi 20. Hatuwezi kwa sababu *the cost of feedlotting* ni kubwa mno. Mashudu ukinunua yana VAT, kwa hiyo ili tuweze ku-*create proper value chain* kwenye sekta ya mifugo nashauri *create an exemption* ya VAT kwenye mashudu kwa sababu kinachotokea sasa hivi mashudu yako yote unayozalisha ndani yanapelekwa Kenya, kwa sababu yana *exemption* kwao yanarudi ndani sisi tunageuka soko kwa *raw material* ya kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niishauri Serikali, Wizara imechukua hatua na ni muhimu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kama hatutachochaea ufanyaji biashara katika uchumi wetu, mwaka kesho atakuja hapa hajafikia *target* ya makusanyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hali ya benki zetu, *non-performing loans* Serikali imechukua *measures* ambazo mimi kwa kweli naziita *cosmetic*, samahani akinamama; kwamba mama amekaa kwenye *dressing table* anachukua poda anaweka haibadilishi alivyo *naturally*. *Cosmetic measures* tulizochukua ni nini; *BOT*imeamua kupunguza *some of the regulations* zake za *deposits* na *non-performing loans*.

Mheshimiwa Spika, lakini unawapa watu *extention* ya miezi mitatu ambao wameshindwa kulipa mkopo. Wameshindwa kulipa mkopo kwa sababu gani; kwa sababu wameshindwa kufanya biashara. Kwa hiyo ni wajibu wa Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba tunachochaea *trading* na ili tuchochee *trading* ni lazima tuchochee Sekta ya Kilimo. Kama kwenye kilimo hatutaamua kuanzisha price *stabilization*; wakulima wetu wanazalisha mahindi, kuzalisha kilo moja ya mahindi; narudia, ni Sh.357.

Mheshimiwa Spika, leo kilo moja ni Sh.150 au Sh.200, mkulima anapata hasara. Ni wajibu wa Wizara ya Fedha kwa kutumia *vehicles* tulizonazo ambayo moja ni Bodi ya Mazao Mchanganyiko na nyingine ni *NFRA*. Tuwape fedha wanunue haya mahindi kwa *competitive rate* kutoka sokoni halafu tuyatafutie soko wauze, kwa sababu hii fedha ni *revolving*. Nafahamu hofu ya Wizara ya Fedha, imekuwa kwamba wakitoa fedha kwenda *NFRA* huwa hairudi. Sasa ni udhaifu wetu sisi, kwamba mkulima kazalisha mahindi hana soko, tutachochaea vipi biashara? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo kule kwetu Nzega; natolea mfano kwangu Nzega; leo mkulima amelima mazao yake, amevuna anataka kuuza, tunatumia mifumo tuliyonayo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bashe, malizia.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, namalizia, *just a minute*.

Mheshimiwa Spika, leo kule Nzega wafanyabiashara wa mazao wanakuwa *disturbed*. Tumeleta vi-regulation kwamba eti mpunga usiweke kilo 90 kwenye gunia, ukikutwa unaweka faini. Waganda wanaokuja kununua mchele Nzega wanakuwa *disturbed*, wanahojiwa, kiko wapi kibali

cha kuja kununua mashineni, huna kibali faini 500,000. Tunawanyima fursa wakulima wetu kuuza mazao yao, matokeo yake hawawezi kubadilisha maisha yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwombe Waziri, kachukua *measures* nzuri lakini kama hataweka jitihada kwenye sekta ya kilimo na mifugo mwaka kesho tutakuja hapa hatujafikia malengo ya bajeti tuliyotarajia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene. Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza niungane na Bajeti Mbadala ya Kambi ya Upinzani na pia *ni-endorse statement* ya KUB, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe kwamba Awamu hii ya Tano imekuwa na bajeti hewa endelevu ikiwemo bajeti hii. Bajeti hii ni hewa kwa sababu haifikii malengo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016/2017 malengo yalikuwa triliuni 29 zilipangwa, lakini *only* triliuni 20 zilitoka. 2017/2018, triliuni 31 lakini *only* triliuni 21 zilitoka. Makisio wanaweka makubwa kuliko uhalisia wa vyanzo vya mapato, kwa hiyo wanaleta makisio hewa na wanajua kabisa kwamba ni hewa kwa sababu haliwezi *gap* lile likawa linajirudia kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii inafanya matumizi nje ya bajeti iliyopitishwa na Bunge lako. Kwa mfano ujenzi wa ukuta Mererani, hosteli za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ujenzi wa *airport* Chato, suala la kuhamia Makao Makuu Dodoma, haya yote yanaweza yakawa mambo mazuri, lakini ili yakamilike katika uendeshaji wa nchi yalitakiwa lazima yapite kwenye Bunge lako Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hata Sera ya Viwanda ni hewa kwa sababu kila siku tunaskia mnazindua viwanda vipyta na kuhesabu idadi imeongezeka, mara viwanda 3,000 tayari siku mbili unasikia kuna viwanda 4,000, hatuoneshwi ujenzi tunaoneshwa uzinduzi. Hii maana yake ni nini; maana yake ni kwamba hawa jamaa wanazindua viwanda ambavyo vipo toka zamani. Kwa mfano kulikuwa na kiwanda kimoja Mwanza, sitaki kukitaja, kilishazinduliwa toka mwaka 2013 huko na marehemu Kigoda, Waziri wa Viwanda, lakini juzi naangalia kwenye taarifa ya habari naona Waziri Mkuu anakwenda kuzindua tena kiwanda kile kile ambacho mimi taarifa zake za uzinduzi nilikuwa nazo. Kwa hiyo tunakwenda na vitu hewa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nabaki najiuliza; huyu Mheshimiwa Dkt. Mpango alikuwa ametoka, alikuwa ni Katibu wa Tume ya Mipango kwenye Awamu ya Nne chini ya Dkt. JK na nchi ilikuwa inakwenda, sasa hivi wamemweka juu zaidi, ni Waziri kwenye Awamu ya Tano, lakini mambo hayaendi kiasi kwamba najiuliza kweli hii mipango ni ya kwake au kuna mtu anapanga wana-*impose* tu kwenye makabrasha yake aje kusema humu Bungeni? Hivyo ndivyo vitu ninavyojuiliza, nina uhakika kabisa mipango hii siyo ya Mheshimiwa Dkt. Mpango, kuna mtu anapanga hii mipango sasa sijui anatumia vigezo gani.

Mheshimiwa Spika, sababu zinajulikana, *otherwise* Wabunge wa CCM hususani wamejaa unafiki. Asilimia 98/99 ya Wabunge wa CCM wanalalamika pamoja na sisi mambo yanavyokwenda, hawaridhiki na hali inavyokwenda katika Awamu hii ya Tano lakini hawasemi hadharani. Sasa sisi tukisema nje wanatulaumu, wanasema sasa ninyi tunawaambia halafu mkifika ndani... (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbilinyi, ukisema Wabunge wa CCM ni wanafiki unajua unamsema na Spika pia?

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Hapana, wewe uko *exempted* kwa sababu hata sasa hivi umeonesha kidogo unanyoosha Kiti kusema ukweli, kwa hiyo tunakupa tano

zako. Wakifanya vizuri tunawasifia, wakikosea tunakosoa na tunapokosoa hatuna chuki, *no personal vendetta against anybody*. Tunapochangia na kukosoa, yote ni kwa ajili ya Taifa hili tukiamini kwamba Taifa hili ni letu sote.

Mheshimiwa Spika, sasa hawa wenzetu wanalamika nje; kwenye korido huko, kwenye chai na ukisema wanasema kwamba ninyi tunawaambia mkifika ndani tena mmatutoa nishai. *Of course lazima tuseme ili nchi iende, wanataka tukae navyo sisi moyoni na sisi tupate presha, presha bakini nazo ninyi wenyewe.*

Mheshimiwa Spika, hawa watu wanaokaa kimya ni hatari zaidi kuliko sisi tunaosema. Niseme, mtu kama Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Nape, Mheshimiwa Alhaji Bulembo hawa siyo tatizo ndani ya CCM kwa sababu hawa angalau wanaongea, tatizo ni ninyi msiosema halafu mnalamika kwenye makorido (*corridors*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa tujue kitu kimoja; katika Taifa la watu *almost* 55,000,000, sisi tuliono humu 300 *plus*, sisi tuko *privileged to serve*, sasa tusije tukatumia hii *privilege to serve* kusaliti wananchi; huku unasema hivi huku unasema vile. Halafu kitu kimoja nimefanya utafiti nimegundua, *you guys don't love President Dr. Magufuli*, ninyi CCM hamumpendi Dkt. Magufuli. Hamumpendi Rais wetu wala hamlipendi hili Taifa kwa sababu mtu unayempenda lazima umwambie ukweli mambo yanapokuwa hayajakaa sawasawa na hili tunalisema kila siku.

Mheshimiwa Spika, hamuwezi kukaa mnalamika na sisi, mnasema mambo hayaendi lakini mkifika kwenye *floor* hapa hamsemi ukweli halafu kila mtu akisimama mnam-*personalize*, mpaka Mheshimiwa Dkt. Mpango anakuja kumfananisha na madikteta wa *North Korea* kwa ajili ya kupitiliza upambe, yaani unakuwa mpambe mpaka tajiri ananuna, anaona hapa unaharibu, unanifananisha na watu ambaao sitaki kufananishwa nao. Kwa hiyo *you guys don't love our president*, mngempenda lazima mngemwambia ukweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme, kama nilivyosema, penye ukweli tunapongeza penye tatizo tunasema. Nampongeza sana Rais Magufuli kwa kum-*demote*, kumtumbua Mkurugenzi Msaidizi wa Usalama wa Taifa *TIS*, kutoka kuwa *Deputy Director* mpaka kuwa *RASKwa* sababu toka Mheshimiwa Rais amefanya kitendo kile hali ya nchi imetulia kidogo, hatusikii sana mambo ya kuokota watu kwenye viroba, hatusikii watu kupotea toka yule *Deputy* amekuwa *demoted* kuwa *RAS* haya mambo hatuyasikii. Kwa hili nampongeza Rais na aendelee kuchukua mawazo yetu yeye sisi tutampa kwa sababu wao hawataki kutoa mawazo wanafanya unafiki dhidi ya Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nchi hii sasa Mheshimiwa Mbunge kila Taasisi imekuwa kama polisi. Tumetoka kuongea hapo unaona Maafisa wa Wizara wanaanza kutembea na rula kupima samaki, sasa dagaa utapima kwa rula gani, inabidi watutengenezee rula za kupimia dagaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, BASATA nao hawako nyuma kila Taasisi imegeuka kuwa kama polisi, kazi ni kamata, fungia sijui nini. Mimi jana wamefungia nyimbo yangu, inaitwa namba 219, wakati nyimbo hata sijaitoa upambe huo... (*Makofii*)

SPIKA: *Declare interest* kwanza Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, na-*declare interest* mimi ni msanii pia na ni msanii nguli wa *hip pop* Afrika na duniani na ndiyo nilikotokea na nimetoa mchango mkubwa sana katika sanaa ya muziki wa kizazi kipyta, bongo fleva mpaka hapa ilipofikia. Hilo Serikali inatakiwa ilitambue sana na isikilize sana tunapozungumzia masuala ya wasanii na namna inavyotengeneza ajira.

Mheshimiwa Spika, sasa wewe unafungia nyimbo ambayo sijatoa, nyimbo *ime-link* katika katika *industry* ya music *ku-link* kupo, mimi najandaa kushuti *video* nyimbo *ime-link*, BASATA hawajaniita kunihoji, pengine ndiyo nilikuwa nawapelekea hiyo nyimbo waisikilize; wao wanatoa tu

statement wanafungia nyimbo ya msanii wakati hawajawahi kuingia *studio* hata siku moja, hawajui hata mihangai ko ya *studio*, hawajui hata gharama wanakurupuka tu kufungia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumejenga hii sanaa miaka mingi mpaka imekuwa ajira, wanataka sisi wote tuimbe mapenzi. Sisi siyo kila mtu lazima aimbe mapenzi, sisi tunaimba masuala ya kijamii...

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, sisi tunaimba masuala ya kijamii...

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Mbilinyi pokea taarifa ya Mheshimiwa Shonza.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kaka yangu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kwamba anachozungumza hapa Bungeni siyo sahihi. Kwa sababu akisema kwamba amefungiwa nyimbo, wimbo ambao ume-/leak, sasa wimbo una-/leak vipi? Kwa sababu kama wimbo angekuwa hajautoa sasa hivi wimbo upo kwenye mitandao na hata mimi nilipo mashairi ya wimbo ninayo. Kama hiyo haitoshi katika Bunge hili mmekuwa mkilalamika kwamba BASATA wanafungia nyimbo bila kuwapa taarifa.

Mheshimiwa Spika, tumeshatoa *statement* kwamba kwa msanii yoyote anayetoa wimbo cha kwanza anapaswa apeleke mashairi yake BASATA, yahakikiwe kwanza. Sasa kama Mheshimiwa Sugu ametoa wimbo ambao BASATA hawajauitisha. Halafu leo anakuja analalamika kwamba wimbo umefungiwa, wakati wimbo upo kwenye mitandao na mimi ninao na mashairi yake hapa ninayo. Kwa hiyo kosa si letu, kosa ni la kwake kutokufuata sheria na ndiyo maana hata *statement* ambayo BASATA imetoa iko *very clear*

kwamba wimbo una makosa mawili kosa la kwanza ametumia maneno ya uchochezi, lakini kosa la pili hajafuata sheria. Sheria mojawapo ni kwamba kabla msanii hajatoa wimbo lazima apeleke mashairi yake BASATA yahakikiwe. Ahsante.

SPIKA: Taarifa hiyo Mheshimiwa Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, kama alivyosema ni kaka yake, kwanza naomba mlinde muda wangu, ningempiga lakini kwa hali dada yangu naomba nimwache, tumsubiri mjomba, sitampiga namheshimu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ila tu ninachomwambia mimi siyo Roma wala mimi siyo Diamond, naiburuza BASATA Mahakamani kwa suala hilli na ndiyo watajua namna gani nchi inatakiwa iendeshwe kwa kufuata utawala bora na sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeshasema nyimbo imevuja, nyimbo sijaitoa rasmi, wimbo...

(Hapa walijibizana bila kutumia kipaza sauti)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe unalielewa suala hilli, wimbo umevuja, kwa hiyo BASATA nawasiliansa na Mawakili wangu sita ili niwaburuze BASATA Mahakamani, ndiyo watanyooka waache kuchezea kazi za wasanii. Huyo dada yangu Mheshimiwa Shonza mwenyewe hajawahi kuingia hata *studio ku-record* halafu anakuja anafungia nyimbo za watu kiholela.

Mheshimiwa Spika, nikiacha na hayo ujumbe umeshafika, niombe tu Mheshimiwa Waziri tuondoe siasa kwenye masuala ya uchumi na biashara, nikitangaza *interest* mimi pia ni mfanyabiashara mchanga ninayeanza...

SPIKA: Malizia Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, toka nimeanza kabiashara kangu hawa jamaa wameingiza siasa mara, sijui *TRA* wamefanya nini, wanakuja wanakuta *clear*, wanaenda sijui kwenye Taasisi gani wanakuja wanakuta *clear*, mwisho *RSO* Afisa Usalama wa Taifa Mkoa anaenda benki iliyonikopesha kuhoji ku-*check* anakuta kweli mimi nimekopeshwa. Anauliza toka lini mmeanza kukopesha wapinzani? Jamaa akamwambia, Joseph Mbilinyi Mkurugenzi wa kampuni fulani hajaja hapa kama Mbunge, hajaja hapa kama mwanasiasa, amekuja hapa kama mfanyabiashara na mpaka sasa hivi analipa marejesho yake vizuri. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri Mpango tuache kutumia *TRA*, tuache kutumia Taasisi zingine ku-*discourage* wafanyabiashara wachanga kama sisi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Geogre Simbachawene atafuatiwa na Mheshimiwa Joel Mwaka Makanya.

MHE. GEOGRE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ya Mipango na Fedha kwa kazi nzuri wanayofanya na sisi tunasema kama Wabunge wa chama kilichopewa dhamana na Watanzania kuongoza nchi hii, tuko nyuma yao na wasiwe na hofu yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa mengi juu ya uchumi wa nchi yetu. Leo nianze kwa kumuunga mkono nakubaliana sana mawazo ya mchangiaji aliyepita rafiki yangu Bashe kwa maeneo aliyogusa amefanya kazi nzuri ya kibunge na ni mfano mzuri wa Wabunge wengi ambao tunachangia michango yetu hapa inayokwenda sawasawa kabisa na tunachotakiwa kuwafanya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labla pengine nilikuwa nikisikiliza wenzangu wanavyochangia wakihoji uwezo wa kuweka

mipango ya nchi yetu na kuendesha uchumi wa nchi na wengine wakijaribu kubeza yanayofanyika. Nataka niwahakikishie na hasa Wabunge wenzangu wa CCM. Tusivunjike moyo watanzania wanatuelewa wanaona barabara zinajengwa, wanaona zahanati zinajengwa, wanaona vituo vya afya vinajengwa wanaona watoto wao wanasoma bure, wako pamoja na sisi na wanatuelewa sana tuendelee. Usitegemee adui yako akakusifia na ukiona anakusifia basi jambo hilo uliache, ukiona anakupinga jambo hilo lifanye sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie Bunge lako kukumbusha misingi ya uchumi wa nchi yetu unapangwaje. Maana hapa zimekuwa zikielezwa *theories* mbalimbali za uchumi na wengine hata siyo Wachumi na hata mimi na-*declare* kwamba siyo Mchumi, lakini nataka nijadili uchumi kwa *legal perspective*, kwa sababu mipango na uendeshaji wa uchumi haji nao tu Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa sababu ni Waziri, ipo kwenye sheria na katiba hakurupuki tu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango akaja tu na mambo hapa akasema imekuwa hivi imekuwa hivi, hapana.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nisome katiba na naomba niisome kwa ukamilifu maeneo yanayo-guide mipango na uendeshaji wa uchumi wa nchi yetu; ili tukiwa tunazungumza tuwe tunaelewana, maana wako wengine wana nadharia za kibepari, wako wengine wana nadharia za kijamaa hatuwezi kuelewana sisi wana *TANU* na *ASP* tunajua tulikotoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu Ibara ya tisa (9) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inasema hivi:

"Lengo la katiba hii ni kuwezesha ujenzi wa Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au wa chochote kati ya vyombo vyake na udugu..."

MHE. PASCAL B. HAONGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. GEOGRE B. SIMBACHAWENE: ...na amani kutokana na kufuata siasa ya ujamaa na kujitegemea, ambayo inasitisiza utekelezaji wa misingi ya kijamaa...

MHE. PASCAL B. HAONGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. GEOGRE B. SIMBACHAWENE: ...kwa kuzingatia mazingira yaliyomo katika Jamhuri ya Muungano...

Mheshimiwa Spika, naendelea anasema katika Ibara hii ya 9: ...Hivyo...

MHE. PASCAL B. HAONGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. GEOGRE B. SIMBACHAWENE: ...Mamlaka ya Nchi na vyombo vyake vyote inawajibika kuelekeza sera na shughuli zake katika lengo la kuhakikisha...

Mheshimiwa Spika, naruka (a), naruka (b) kwa sababu ya muda naenda (c):

(c) *kwamba shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kwamba utajiri wa Taifa unaendeleza, unahifadhiwa na unatumia kwa manufaa ya wananchi wote kwa ujumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine; (Makof)*

Mheshimiwa Spika, naomba niruke zote niende (i) inasema:

(i) *kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa yanatalilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada za kuondosha umaskini, ujinga na maradhi;*

(j) *kwamba shughuli za uchumi haziendeshwi kwa njia zinazoweza kusababisha ulimbikizaji wa mali au njia kuu za uchumi katika mamlaka ya watu wachache binafsi." (Makof)*

SPIKA: Mbunge wa Mbozi nimekuona.

TAARIFA

MHE. PASCAL B. HAONGA: Mheshimiwa Spika, mchangiaji anayeendelea kuchangia ameeleza Bunge hili kwamba mambo yanaenda vizuri kabisa, lakini wote tunafahamu kwamba ukuta unajengwa kule Mererani, kwa sababu mambo tu hayaendi vizuri kulikuwa na wizi na wizi unaendelea katika Taifa letu kwenye madini na ye ye ali kuwa ni Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba ana tuhuma ya Kamati, nataka niseme tu kwamba mambo hayaendi vizuri na ndiyo maana tu nchi hii tumekuwa na hofu, kumekuwa na wizi na ndiyo maana tunajenga ukuta ule kwa sababu hali si shwari. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Simbachawene endelea tu ndugu yangu.

MHE. GEOGRE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nia yake ilikuwa ni kuona kwenye TV umeonekana. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimenukuu eneo hili *theories* tunazozitoa nyingi hapa kila mtu anatoa *theory* yake na anachukua mfano *best practice* ya nchi anayoionna ye ye. Wakati asili ya uchumi wa Taifa lolote, asili ya mipango ya uchumi wa Taifa, mipango ya maendeleo ya Taifa lolote inatokana na historia yake. Sisi Watanzania kwa asili ni wajamaa na fikra zetu sisi ni za kiumoja umoja na ujamaa jamaa, huwezi kuwabadilisha Watanzania hapo.

Mheshimiwa Spika, leo hii mtu akija na mawazo ya *purelyubepari*, basi hatokani na misingi ya Kitanzania, ingawa katika lbara hii ya tisa (9) inasema tutafuata siasa ya ujamaa na kujitegemea kwa kuzingatia mazingira na mabadiliko ya wakati. Ndiyo maana katika sheria zetu tumetambua baadhi ya misingi ya kibepari, tukatunga sheria ya *PPP* kwamba wakati mwagine Serikali itapaswa kufanya biashara na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, tukapima tukaweka sheria ya ubinafsishaji kwamba tukaribishe sekta binafsi iingie kufanya kazi na Serikali. Ndiyo maana tuna viwanda na ndiyo maana shughuli mbalimbali zinazofanywa na sekta binafsi, lakini katika katiba hii inatukataza kupeleka njia kuu za uchumi mikononi mwa watu wachache maana huo ni unyonyaji. Ndiyo maana tunapokuwa tunazungumza mambo haya ni lazima twende kwa kiasi maana nchi yetu kwa asili na hata fikra za watu, utamaduni wa watu wanafikiria... (*Makofi*)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Waheshimiwa taarifa ziwe zina maana, vinginevyo michango yetu haitakuwa na mantiki, haya hebu toa hiyo taarifa.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, nilichokuwa naomba tu mchangiaji atuelekeze kwamba ye ye mtazamo wake ni nini kwa sababu mtazamo wa Serikali unaonekana ndo *encourage private sector* na *private sector* na *free market* hazihusiani na huu ujamaa unaozungumzwa. Sasa lazima pia na ye ye atuelekeze, je, haya ni mawazo yake ama ni mawazo ya Serikali yake ya Awamu ya Tano?

SPIKA: Mheshimiwa George endelea.

MHE. GEOGRE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nikubaliane kwamba wakati mwingine mtu unapochangia ukakatizwa katizwa inaondoa ladha nzima, lakini nime-cite hapa Katiba yetu na naomba nirudie maana sasa sina namna na kwa hiyo hata hotuba yangu haitakwisha.

Mheshimiwa Spika, eneo la katiba hili linazingatia kwamba ambavyo inasisitiza utekelezaji wa misingi ya kijamaa, kwa kuzingatia mazingira yalimo katika Jamhuri ya Muungano. Mazingira yatakavyojitokeza tutabadilika kulingana na ndiyo maana sisi hatuwezi kusema ni wajamaa *per se* au mabebari *per se*. Ukitaka kutengeneza misingi ya

uchumi wa Tanzania haiwezekani ikafafana na nchi nyingine *that's what I want to say!* Ni lazima itokane na asili ya watu wale ndiyo maana kwenye miaka ya 90 mpaka 2000 tulipoingia kwenye sera ya ubinafsishaji, tulipobinafsisha wengine walipotaka kutuondoa madarakani wakasema hawa wameuza viwanda, wakati wao wenyewe wanasesma tukumbatie sekta binafsi, wakasema tumeuza viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii tulikuwa tuna Shirika la Ndege ambalo tumejaribu kucheza na sekta binafsi tukaingiza South Africa wakachukua baadhi ya hisa na nini likashindwa kwenda. Tumeamua Serikali ya Awamu ya Tano kununua ndege zetu imekuwa nongwa. Leo hii tunayo reli ambayo tumeamua kujenga sisi wenyewe kama nchi na kwa kuanza na fedha zetu wanasesma kwa nini tusiwape sekta binafsi waweze kufanya mambo yenye gharama kubwa. Huku wakiona kabisa kwamba yako baadhi ya mabehewa ya watu binafsi yanayotembea kwenye reli...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante malizia, Mheshimiwa.

MHE. GEOGRE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia ni lazima Watanzania tuunge mkono tijihada hizi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano maana mengi haya yanayofanywa leo yalikwishashindikana kwa formula hizo wanazozisema. Ndiyo maana tunasema tuungane mkono kwa sababu hakuna kanuni moja ya uendeshaji wa uchumi na uchumi unatokana na historia ya watu wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Geogre Simbachawene, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma.

MHE. JOEL M. MWAKANYAGA: Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hotuba ya bajeti kuu ya Serikali iliyowasilishwa na Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango tarehe 14 mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, pili, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, nitaendelea kumpongeza kila nikisimama kwa sababu kazi yake anayoifanya tunaiona ni nzuri na moja kati ya vigezo kwamba kazi inayoyofanywa ni nzuri tunaona, bajeti hii imetolewa katika kipindi chake akiwa Rais. kwa hiyo, hii ni bajeti ambayo ina mwongozo moja kwa moja toka kwa Mheshimiwa Rais na ni bajeti nzuri kama tunavyoiona, nampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatu nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango ye ye pamoja na Naibu wake, lakini pamoja na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara ile kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuiandaa hotuba hii na bajeti hii ambayo sasa tunaijadili hapa Bungeni. Mwisho, nimpongeze ye ye binafsi kwa uwasilishaji mzuri sana wa bajeti alioutoa siku ile ya tarehe 14 hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba mpango ni mpango na mipango tunayo sisi sote, majumbani mwetu tuna mipango mingi na hakuna mtu anayepanga na mipango yake ikatimilika asilimia 100, si kawaida. Utapanga kufanya vitano, utatekeleza vitatu au vinne mpango ni dira, dira inapokuwa nzuri una hakika kwamba wewe unapiga hatua nzuri; mipango yetu ni mizuri na ndiyo maana tunasema bajeti hii ni nzuri sana. Bajeti hii ni nzuri kwa sababu imelenga kwa wananchi wa kawaida, wananchi wa chini kabisa. Kwa nini nasema hivyo, tukienda kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa kuanzia 42 kuendelea hadi 46 yako mambo mengi yaliyozungumzwa pale.

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye misamaha na mfumo wa kodi ambaa baadhi umejionesha pale. Serikali

imesamehe kodi ya ongezeko la thamani kwa baadhi ya malighafi muhimu zinazokuja kutumika viwandani kuzalisha bidhaa zinazotumika kwa Watanzania. Pia Serikali hiyo hiyo imeongeza ushuru wa bidhaa za kutoka nje kwa bidhaa ambazo pia zinazalishwa hapa nchini, lakini pia tumeona Serikali safari hii haijagusa kabisa kuongeza kodi kwenye bidhaa zote za mafuta ikiwemo *diesel* pamoja na *petrol*.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi ni muhimu sana, hatua hizi zitasaidia sana kupunguza mfumuko wa bei za bidhaa mbalimbali zinazozalishwa hapa nchini. Tunapopunguza gharama za uzalishaji maana yake bei za bidhaa zetu ama zitabakia *constant*, ama zitashuka chini kidogo. Kwa hiyo basi, kama tulivoona kwenye pungozo na ongezeko ya kodi mbalimbali ambazo tumezitaja hapo nyuma kwa mfano, madawa ya binadamu, vyakula vya binadamu, vyakula vya mifugo, hivi ni vitu ambavyo moja kwa moja vinamgusa Mtanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, vilevile hatua hizi zinalenga kulinda viwanda vya ndani jambo ambalo ndilo kipaumbele kikubwa cha Serikali yetu ya Awamu ya Tano ya Tanzania ya viwanda. Tunapolinda viwanda vya ndani maana yake tunakuza ajira kwa Watanzania. Suala la uchumi wa Tanzania limejitokeza wazi kabisa kwamba linakua kwa kasi kubwa sana, lakini ukiangalia upande wa pili wa mwananchi wa kawaida, uchumi wa mwananchi wa kawaida hauonekani kukua kwa kasi sambamba na kasi ya uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hili ndilo kipaumbele cha nchi yetu cha Serikali ya Awamu ya Tano kwamba Tanzania ya viwanda inalenga kuwe na viwanda vingi, viwanda vinavyotegemea sana mazao ya kilimo. Kwenye kilimo ndiko kunaajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania, sasa ukiwezesha kuwa na Tanzania ya viwanda maana yake unatengeneza soko kwa ajili ya mazao yetu yanayozalishwa hapa Tanzania, maana yake unawawezesha Watanzania wa kawaida kupata kipato kitakachowasaidia kukuza uchumi wao. Katika

kilimo utakuta Watanzania wote tupo, wapo Watanzania wa kawaida lakini wako vijana sehemu kubwa, wako akinamama na hata walemavu wako humohumo ndani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ili mipango hii iweze kuwa na tija, Serikali inatakiwa ijizatiti. Ijizatiti kweli katika kukusanya mapato yake, ihakikishe kwamba taratibu zote za ukusanyaji wa mapato, tumesikia baadhi ya Wajumbe wakichangia hapa wasiwasi unaokuwepo juu ya nani anasimamia nini katika ukusanyaji wa mapato haya. Ni vizuri tukajihakikishia kwamba tuko kwenye mikono salama, pesa yetu isichopoke chopoke huku na huko ili moja kwa moja itumike katika kuitekeleza hii Bajeti ya mwaka wa bajeti 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, niombe sana, pesa hii inapopatikana ielekezwe kule kunakohusika. Wizara mbalimbali zimeleta bajeti zao na ndiyo hii sasa imeletwa kwa ujumla, imeletwa kama Bajeti Kuu ya Serikali. Kama Wizara hazitapewa bajeti zao walivyoomba basi suala zima la Bajeti hii kutokuwa na manufaa sana kwa wananchi litakuwa limeleta shida.

Mheshimiwa Spika, nije kwa upande wa ardhi, bajeti hii inahitaji wananchi wafanye kazi. Wananchi wanatakiwa kuwa na *peace of mind* katika kuzifanya kazi zao. Kama wananchi watakuwa na hali ya migogoro ya hapa na pale ya ardhi maana yake ni nini? Zoezi zima la uzalishaji kwao litakuwa siyo la ufanisi mkubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana ndugu yangu Waziri wa Ardhi, kuna migogoro mingi ambayo unaishughulikia, naomba uishughulikie kwa kasi kubwa. Nakuamini sana Mheshimiwa Lukuvi kazi unayoifanya, lakini nikuelekeze pia, hata hapa Dodoma kuna migogoro ya ardhi, hata kule Chamwino kuna migogoro ya ardhi na bahati nzuri wewe ulishawahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma unafahamu nini ninachokizungumza, unayafahamu maeneo ya Wali kule kuna mgogoro wa ardhi kati ya Wilaya ya

Chamwino na Wilaya ya Kongwa. Inafika mahali wananchi wanakimbia maeneo yao, kipindi cha kulima wanakimbia maeneo yao wanashindwa kufanya kazi inavyostahili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia niseme upande wa viwanja...

SPIKA: Mheshimiwa Makanyaga malizia.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa pika, ahsante sana, labda nimalizie moja tu kwa upande wa viwanja kwako, Mheshimiwa Lukuvi viwanja pale Buigiri vimepimwa siku nyingi lakini zoezi zima la kuvigawa vile viwanja limekuwa tatizo. Mheshimiwa Waziri alikuja pale Wilayani akaotoa maelekezo lakini maelekezo hayo yajafuatwa. Naomba sana alitekeleze hilli ili wananchi wafanye kazi kwa amani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa leo nimevaa vazi adhimu la Kiislam na pengine nitasema maneno makali kidogo naomba nianze kwa Sala "Audhubillah mina-Shaitwani Rajeem, Bismillah Rahmani Raheem" (*Kicheko*)

SPIKA: Sheikh wa Kisukuma huyo. (*Kicheko*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake na watu wote wanaomsaidia kwenye Ofisi yake. Naomba niseme kwa hisia zangu kwamba yeye ni Waziri wa kwanza toka Serikali zote zianze, Waziri ambaye anapambana na Watanzania kuwabadilisha kuwatoa kwenye kukwepa kodi, kuwapeleka kwenye kulipa kodi. Kwa hiyo, nimwombe na nimshauri

asikate tamaa, hii mishale anayopigwa ni moja ya maboresho lakini kazi yake hata Wapinzani wanajua anafanya kazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nimshauri Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango, nianze na biashara ya dhahabu. Biashara ya dhahabu ameweka kodi ya asilimia 14 ukichukua makorokoro kuanzia kuchimba mpaka kuuza. Kodi hiyo hiyo anatozwa anayechimba gramu moja, anatozwa na mtu mkubwa kama *GGM* kodi moja. Ukiija kuchunguza wale ambao wanachimba kwa kiasi kidogo, wachimbaji wadogo ni kama wanamtumikia tu yule mkubwa apate faida, sisi tuendele kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, tulishawahi kushauri mara nyingi Mheshimiwa Waziri kwamba ukienda nchi kama Uganda wao wana-*charge* 0.5 kwa wachimbaji wadogo, ukienda Rwanda 0.6, ukiija Tanzania 14. Kwa nini Mheshimiwa Waziri asiondoe kodi kwa wachimbaji wadogo ikawa hata *zero* ili tukapate dhahabu nyingi kwa sababu kui-*control* dhahabu ni kazi ngumu, dhahabu wengine tunaiokota mashambani, ataidhibiti viyi?

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa nini asiondoe kodi huku kwa wachimbaji wadogo ikawa *zero* tuwavutie na wengine wauze Tanzania ili sisi tupate tu asilimia moja kwenye *export*. Mtu anayesafirisha ndiyo amlipe lakini kwa kodi asilimia 14 dhahabu ya milioni 100 unaweza ukapata faida ya milioni 2,500,000, unataka mimi nikalipe bei gani? Lazima nikwepe. Kwa hiyo, nimshauri sana Mheshimiwa Dkt. Mpango aliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusiana na mikopo ya halmashauri, nilikuwa napiga hesabu kwenye halmashauri yangu ni kama Mbunge wa nane. Ukipiga hesabu ya ambazo tumekopesha tuna karibu bilioni mbili toka tuanze Ubunge pale, lakini hizi hela hazina ufuatiliaji. Kwa nini Mheshimiwa Dkt. Mpango Waziri asizigeuze hizi halmashauri zikawa na Taasisi, tunapokopesha zile hela tuwe na taasisi kabisa, tuna karibu bilioni mbili Geita, ingekuwa ni benki tayari iliyokuwa

na sifa ya kukopesha ikawa na *commitment* ya kuwadai wakulima, lakini sasa kila mwaka tunakopesha, hakuna mtu anayedai, tukikopesha hela hakuna mtu anayedai, pesa zinakwenda na hazina mfuutiliaji. Ukimweka Afisa Ushirika kufuutilia akienda kule na yeYe anaomba kuku tu na mkaa. Kwa hiyo, nashauri tujaribu kubadilisha taswira hii tuangalie kama hizi halmashauri tunaweza tukazigeuza zikawa ule mkopo wake tunaotoa kwa wakulima kuwe na Taasisi ya kuweza kudai kabisa zile pesa na yenye *commitment* na kazi hiyo peke yake.

Mheshimiwa Spika, suala lingine Mheshimiwa Dkt. Mpango; naona kuna Benki ya Wakulima, ndugu zangu Wabunge hii Benki ya Wakulima tunawapelekea matapeli tu, hakuna mkulima ana-*qualify* kukopa kwenye zile Benki hayupo, wala mkulima wa kijjini hahitaji kukopa bilioni moja sana sana wanakopa laki mbili, hakuna sifa za kuwakopesha wakulima na ndiyo maana nikaona tujaribu kubadilisha haya mazingira tuwe na benki zinazoendeshwa na halmashauri zenyewe kutokana na hizi pesa tulizokwishazikopesha.

Mheshimiwa Spika, lingine, ni suala la makinikia, wazo la Serikali ni zuri sana, kwanza sisi tunaotoka kwenye dhahabu tunaona kama ni neema Mungu ametuletea, lakini naomba nishauri mfanyakibashara wa Tanzania siyo adui na sisi tumo humu kwa ajili ya kutetea watu wetu.

Mheshimiwa Spika, niliona Mheshimiwa Waziri wa Madini alitoa kauli akasema "kuanzia kesho hakuna kusafirisha carbon", Mheshimiwa Waziri anaongoza Taasisi za fedha; hawa walio na *illusion plant* kule kijjini, kule Mwanza na sehemu zingine, nataka niseme hapa kama yuko mtu atanibishia wote ni darasa la saba, lakini wamekopa benki na benki zinataka marejesho ukiawaambia leo wote mrudi Geita wengine Singida kuna changamoto. Mwingine unakuta siku hiyo ndiyo mwezi wake wa kulipa marejesho, *carbon* imezuiwa kusafiri.

Mheshimiwa Spika, mwingine amekopeshwa na yule aliye na *illusion* kule Mwanza, jinsi ya kukusanya ile hela ni

kazi, hata unapomwambia kesho arudi kule anapokwenda tena mfano mmoja tu ni Geita; maeneo wanayopewa wale wenye *plant* kuhamisha kujenga hakuna umeme, hakuna barabara, inachukua miezi miwili. Mtu anapigwa *interest* za benki, kwanini tunawaona wafanyabiashara kama maadui?

Mheshimiwa Spika, nimshauri Mheshimiwa Dkt. Mpango, maamuzi mengine haya tuwe tunayapa muda, mimi sikatai wazo na watu tumelipokea vizuri, lakini tungesema basi kwamba tunawapa siku 60 au 40 ili muweze kujandaa kuhamisha mashine zenu hakuna mtu ambaye angelalamika kwa sababu hata wakati wanakwenda kujenga huko walikokuwa ni Taasisi za Serikali zilitoa vibali na kukubali watu wawekeze, kwa nini tunakuwa tuna vigeugeu?

Mheshimiwa Spika, suala lingine, mara nyingi najitla *Chief* watu wanadharau, haya maneno yaliyotokea jana nilizingumza mwanzo kwamba mimi na abiria wangu tulikamatwa na samaki *piece* tatu, kwenye basi tukaombwa *ruler*, hamkujua? Sasa jana *ruler* Bungeni, lakini niseme tu ukweli kutoka moyoni mimi kama *Chief* kwa mara ya kwanza leo nimeamini Wagogo, watani zangu kumbe wana akili kubwa sana. Ulichokifanya Mheshimiwa Spika kusamehe na kusema ukichukizwa unasamehe Waziri ajitafakari! Hilo ni neno kubwa bora hata ungechukua hatua nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hilo neno la kwamba mtu amekuudhi kwa hatua ile halafu unakaa kimya, Wizara hii tumekuwa na Mawaziri nakumbuka watano tena wote Madokta, Mheshimiwa Rais wangu, Dkt. Magufuli, Dkt. Mathayo, Dkt. Kamani, Dkt. Tizeba wote hawa walifanya kazi yao nzuri na uvuvi haramu walikuwa wanapambana nao kwa *style* yao kama viongozi, leo tumeleta Mgambo sijui shule za *design* gani hizikila siku huwa nashangaa, lazima tufike mahali tuchukie. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, huwa nasema kila siku ni vizuri tukakaguliwa vyeti, watu wana elimu za kuunga unga

unamkabidhi Taifa kama hili tutakufa. Sasa hebu jiulize, yeye mwenyewe anakiri anasema mimi niliamua kuwaita ili tutekeleze zoezi la *operation*, yeye ndiyo mtunga sheria? Hajui Sheria za Bunge jinsi ya ku-*arrest* Bunge? Anazijua kabisa anaamua kukiuka kwa kutafuta *kick* na huu Urais utakuja kuwatokea puan. Hata sisi Wasukuma tumelia na tumelalamika tulipokosa msaada, tumefanya ulichokifanya wewe. Tumeamua kunya maza na kumuachia Mungu apambane naye. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tutaendelea jioni na tutaanza na Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Martha Umbula na wengine. Nawashukuruni sana kwa michango na tunaendelea vizuri..

Waheshimiwa Wabunge, mtachangia msiwe na wasiwasi kwamba eti wengine kila wakati wanasema wao siyo wachumi, hamna mtu ambaye siyo mchumi jamani. Kila mtu asipojua *elementary* ya *economics* basi tena. Maana yake hata mama anavyopika chakula anaangalia kwanza wako watu wangapi hapa! Anajua watu watano hawa, anajua maji hayatoshi haya, ugali huu hautoshi huu, uchumi huo. Hawezi kuwa yeye na mume wake halafu anapika debe la mchele, haiwezekani! Kwa hiyo uchumi ni maisha ya kila siku. (*Makofii Kicheko*)

Kwa kweli kama tulivyosema mwanzoni sisi hapa hatuna nia mbaya, kazi yetu kubwa kama Wabunge ni kushauri. Nikichukua samaki mmoja nikamweka hapo na *ruler* halafu Wabunge wote kila mmoja ampime samaki yule, unajua mtakuja na majibu mengi sana tofauti, kwa sababu tofauti wanazohangaika nazo ni sentimita moja, sentimita mbili, *not more than that* na inategemeana na mambo mengi sana.

Waheshimiwa Wabunge, hata macho kuna kitu kinaitwa *non-parallax*, mwininge anavyoangalia *ruler*

anaangalia hivi, mwagine anaangalia hivi halafu samaki ana tumbo unajua siyo karatasi. Ingekuwa ni karatasi hii kwa ruler is very easy lakini samaki ana chini halafu, kwa hiyo hata anayeweka ruler yuko subjective. Akitaka akupige fine anakutwanga tu, hii imepungua sentimita moja weka, hii imepungua hivi weka, biashara hii, hapana jamani. (Kicheko)

Halafu kitu chochote lazima kiwe na *plus or minus* hata kama Sheria yetu imesema sentimita 25 lazima uangalie *plus or minus*. Kama ni sentimita 24 huyu amejitahidi yaani hiki ni kitu sawa tu. Utaipata wapi hiyo exactly to the dot yaani unafanya nini? Mtihani wa sayansi wa Chuo Kikuu? Haiwezekani, kubishania sentimita moja, sentimita? Faini ya malaki, ya mamilioni, sentimita? Tunapotunga sheria tunatunga sheria kwa nia njema hatutungi sheria ili tuwe mechanical/katika kutekeleza, hapana. Nia ni njema kabisa ya nchi yetu na nia njema ya Serikali yetu na hakuna mwenye nia mbaya. (Makofi)

Sisi wote tunajua unawenza ukafuga samaki kwenye bwawa wakafikia mahali fulani wanadumaa tu. Una samaki 5000 kwenye Bwawa, umelisha vizuri, umefuata masharti yote, wamepungua sentimita mbili hata ulishe nini hawaongezeki sasa unafanyaje wale samaki 5,000? Uchimbe shimo uwafukie wote? Haya mambo yanahitaji kuyaangalia kwa roho ya... mmh! Kabisa! Watani wanamtania Mlinga, wanasema Mlinga kalishwa na Mama Celina weee, lakini bado hakunenepa (Makofi/Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni ya leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

Hapa (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yetu, tutaanza na Mheshimiwa Martha Umbulla, hayupo; Mheshimiwa John Peter Kadutu, naye hayupo; Mheshimiwa Innocent Bashungwa!

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mapendekezo ya bajeti mwaka wa fedha wa 2018/2019. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Serikali kwa ujumla, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais katika Wilaya ya Karagwe, tunashukuru sana kwa bilioni 70 ambazo Serikali ime-*commit* katika bajeti hii ya 2018/2019 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Rwakajunju, mradi ambao wananchi wa Karagwe wameusubiri miaka mingi sana, kwa hiyo tunamshukuru sana Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru Serikali kwa kutusaidia kupata Kituo cha Afya cha kisasa pale Kayanga na nashukuru Serikali kwa *commitment* ya kujenga kituo cha afya kingine katika Kata ya Nyaishozi, Kituo cha Afya cha Nyakayanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watalaaam wa Wizara kwa kutuletea mapendekezo ya bajeti ambayo kusema ukweli ni *improvement* ya bajeti zilizopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zipo na ndio maana tumekaa kama Bunge kuchambua mapendekezo haya na kuboresha na ni matumaini yangu kwamba, Mheshimiwa Waziri Mpango kwa kuanza mapendekezo ya Kamati ya Bajeti ni mazuri sana tunawapongeza sana Kamati ya Bajeti kwa mapendekezo mazuri. Kwa hiyo, naamini sana Mheshimiwa Dkt. Mpango akichukulia mapendekezo ya

Kamati ya Bajeti kama msingi akaongezea na haya ambayo tunashauri, naamini kabisa tutapitisha bajeti ambayo ina weledi mkubwa kwa Watanzania. (*Makof*)

Mheshimimwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nina machache ya kuchangia. Nianze kwa kusisitiza sana Serikali, hii ni bajeti ya *fiscal year* ya nne tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani. Tumekuwa tukilia sana kuhusu suala la stahiki za Walimu. Kuna Walimu wamemaliza toka mwaka 2015 mpaka sasa hivi hawajapata ajira na hawajapata ajira si kwamba shule zetu hayahitaji Walimu, kuna upungufu mkubwa wa Walimu katika mashule yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha akae na wenzake katika Serikali walliangalie hilli kwa umuhimu wake na kwa manufaa ya watoto wetu ambao ni kizazi cha ni Taifa la kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Walimu ambao walipandishwa madaraja toka mwaka 2012, lakini mpaka sasa hivi mishahara yao hajarekebishwa *ku-reflect* yale madaraja ambayo wamepanda. Kwa hiyo, kiujumla changamoto ya upungufu wa watumishi ipo hata upungufu wa Wauguzi katika vituo vyetu vya tiba. Serikali wanafanya kazi nzuri ya kuweka miundombinu ya vituo vya afya, hospitali na zahanati, lakini itakuwa haina maana kama tunakuwa tuna majengo mazuri lakini hayana Wauguzi kwa ajili ya kuhudumia Watanzania. Kwa hiyo, hili naomba pia naomba waliweke katika vipaumbele vya mwaka huu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kuchangia ni hili suala zima la takwimu ambazo Mheshimiwa Waziri kila mwaka wa fedha akisoma wastani wa kipato cha Mtanzania na uhalisia wa mtaani unaona kuna ukakasi. Sishangai na nitasema kwa nini. Ukiangalia mapendekezo ya bajeti hii ya 2018/2019, Serikali imefanya kazi nzuri katika kuhakikisha upande wa yule mpokea malighafi kwa maana ya msindikaji au *manufacturing*

wameweka unafuu mkubwa sana na ndio maana tunapendekeza bajeti hii ni mwanzo mzuri wa kusaidia nchi kwenda kipato cha katikupitia uchumi wa viwanda, kwa hiyo ni hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwaombe Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yao, waangalie hii 67% ya Watanzania ambao ni wakulima, wafugaji, wavuvi na hawa Machinga na Mamalishe hiyo ndio *component* kubwa. Kwa hiyo, unafuu wakiukita kwenye hiyo asilimia 67 ya Watanzania ile tunayoita *source economic transformation* tutaiona kwa haraka sana, lakini tukiendelea hivi hii asilimia 33 ambayo sana sana ambayo ni *trade sector, manufacturing* na *service sector*, sawa na yenye ni *component* muhimu, lakini, *component* hizi mbili kwa upande mmoja mkulima, mfugaji, mvuvi na mfanyakibashara mdogo mdogo machinga, mamalishe tukiweza kuwa-align vizuri na ile *component* ya ambayo ina receive kile kinachotengeneza yaani malighafi kwenda kwenye *manufacturing sector* tutakuwa tumefanikiwa kama nchi na tutainua Watanzania kutoka kwenye umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kwa sababu wameshaandaa kama ilivyo sasa hivi na *improvement* itakuwa ni *incremental*, sasa nishauri angalau mwaka huu wa fedha waangalie yale mazao matano tuliyyofanya kipaumbele, waangalie namna gani tutamsaidia mkulima wa haya mazao matano angalau hii *disposable income* yaani kuanzia tarehe Mosi Julai, mwezi unaokuja tutakapoanza kutekeleza hii bajeti aanze kuona *impact* ya moja kwa moja kwenye kipato chake cha mfukoni. Tukifanya hivyo wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anasoma bajeti ijayo wastani wa kipato cha kila Mtanzania hatapata ukakasi ambao anaupata sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie *informal sector*, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamekuwa wakizungumzia sana, lakini naona bado iko changamoto ya namna gani tunafanya kui-tap ili iweze kuwa sehemu ya

formal sector. Sasa nimezungumzia changamoto za Machinga, Mamalishe, Wafanyabiashara wadogo wadogo hawa wote wapo kwenye hii *informal sector*. Hii ni *potential* ya kuongeza kwenye *tax base* ambayo bado iko *null*. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia jinsi Tanzania bado tuko chini ya viwango vya kimataifa, ukichukua *ratio* ya *tax collection as percentage* ya *GDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tuweze ku-*broaden tax* lazima tufike mahali hii *informal sector* ikiwezekana ndani ya Serikali kuwe na chombo maalum cha kuihudumia ikiwezekana hata Wizara, kwa nini, kwa maana hii ni asilimia kubwa ya Watanzania. Ukienda kwenye miji, ukienda kwenye mitaa kule vijijini akimama wanafanya kazi kwenye juu kali, wana familia zao kupitia kwenye vipato hivi vidogo wanatosmesha watoto, wanatibu familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini kama Serikali tusifike mahali angalau kila halmashauri kunakuwa na mkakati maalum wa kuhakikisha hawa akinamama wanaofanya biashara ndogo ndogo barabarani tunawawekea miundombinu na kupitia miundombinu hiyo sasa tunawaingiza kwenye *formal sector* hata Serikali itapata mapato lakini wanyonge hawa nao wataweza kujikwamua kutoka kwenye umaskini. Kwa hiyo, ifike mahali Serikali iangalie hii *informal sector* ikiwezekana kuundwe chombo maalum ikiwezekana hata Wizara kwa ajili ya kushughulika na changamoto zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie changamoto ambayo ipo kwenye zao la kahawa. Natoka Mkoa wa Kagera, tunazalisha kahawa kwa wingi na tunachangia asilimia kubwa sana katika uzalishaji wa kahawa hapa nchini. Tumesema hapa Bungeni kwamba, stakabadhi ghalani kuna *potential* kubwa ya kumsaidia mkulima wa kahawa kutoka kwenye umaskini, lakini matayarisho bado kuna walakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, hivi sasa kule Kagera na maeneo mengine nchini msimu wa kahawa

umeshaanza, lakini sasa hivi mwananchi akipeleka kahawa kwenye Vyama vya Msingi, kwenye risiti anaandikiwa kilo lakini haandikiwi bei ambayo amezuia. Kwa hiyo, napenda kuomba Serikali huu mfumo wa stakabidhi ghalani walichukulie kama yai kwa sababu usipokwenda vizuri huko mbeleni kuna hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wananchi wakulima wa Tanzania wanategemea mazao haya ya biashara katika kujikwamua katika umasikini. Kwa hiyo, zao la kahawa naomba waliangalie kwa umakini mno, waende vijiji waangalie changamoto za wakulima wa kahawa na Serikali waweze ku-*intervene* ili stakabadhi ghalani iweze kumsaidia mkulima wa kahawa kweli. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bashungwa.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, baadaye Mheshimiwa Hadija Hassan Aboud ajiandae.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hoja hizi mbili ambazo ziko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu, kazi ni ngumu sana lakini wanaiweza, ni kazi ngumu kweli kweli. Hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kutoa hoja moja ambayo hailingani sana na hoja hii iliyo mbele yetu. Ziwa Rukwa miaka ya 60 na 70 mpaka 80 mwanzoni

ilikuwa inatoa samaki wengi sana aina ya *tilapia* ambayo inaitwa ngege, walikuwa maarufu sana kwa Nyanda za Juu Kusini mpaka Zambia tulikuwa tunakula samaki hao. Miaka hii sasa hivi hao samaki hawapo, tumebakti tudogo hata huu mkono hauenei. Hata Serikali ikisimamisha uvunaji, miezi mitatu, miezi sita samaki havikui vinabaki pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hofu, kwamba kwa sababu katika Wilaya ya Chunya ambako ndio Mto Rupa unatokea ambao unaingia kwenye Ziwa Rukwa kuna uchimbaji mkubwa sana ambapo hapo zamani walikuwa wanatumia zebaki kusafisha madini ya dhahabu, nina wasiwasi kwamba samaki hawa wamekuwa *contaminated* na zebaki ndio maana havikui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalomba Serikali ifanye utafiti haraka, ifanye utafiti tujue kama ni zebaki ipo basi tujue tiba ni nini tusije tukaharibu afya za watu. Kama imeshindikana basi Serikali ifanye mpango wa kupandikiza samaki wengine katika ziwa Rukwa ili tuendelee kuvuna kama tulivyokuwa tunavuna zamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naliunganisha na hoja ya kodi, *tax measures* ambazo Mheshimiwa Waziri ameweke mojawapo. Mheshimiwa Peter Serukamba juzi akichangia alidadavua sana kitaalam akiipongeza Serikali kwa kuanzisha *electronic tax stamps*, alidadavua kitaalam. Mimi nataka niiseme *ki-layman*, Watanzania tumekuwa tunanyweshwa mapombe makali, magongo kwa miaka mingi sana kwa sababu ya *tax stamps* ambazo zinaweza kuigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifika mahali hapa Tanzania ilikuwa nusu ya *consumption* ya konyagi hapa nchini nusu ni *original* na nusu ni *fake*. Sasa ukinywesha *population* ya Watanzania gongo kwa muda wa miaka minne, mitano utapata watu wa ajabu sana. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuweka hii *electronic tax stamp* ambayo haiwezi kuigwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faida zote ambazo watapata za *ku-count real time* kupata kodi kuongezeka kwa mara dufu, lakini hili la Watanzania kunyweshwa gongo mimi namsifu sana kwa hilo Mheshimiwa Waziri na siyo gongo tu kwa konyagi hata kwenye *brand* hata kwenye vitu vingine wanaiga *tax stamps* wananywesha Watanzania. Aliwahi kusema Mheshimiwa wa Jimbo fulani hapa kwenye jimbo lake watu wanaume walikuwa wanashindwa kuhudumia ndoa, wanakwenda nchi nyingine kwa sababu ya mambo kama haya. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwa kutumia uchumi wa jiografia kuweza kukuza mapato ya *economy* ya nchi, kupanua bandari ya Dar es Salaam, kujenga bandari ya Bagamoyo, kupanua bandari ya Mtware, kujenga *SGR* na kuirekebisha *meter gauge*. Kwa hiyo, tutakuwa na reli mbili kwa upande wa kaskazini *standards gauge* ambayo ina mita 1.067 na *meter gauge* ambayo ni mita moja kamili. Vilevile reli ya TAZARA ambayo yenyewe ni *cap gauge* yenyewe upana wake ni mita 1.067, tutakuwa na aina tatu za reli. Hizi za Kaskazini zitaungana za Kenya, Uganda lakini hii ya TAZARA itaungana na South Africa na Zambia na Nchi zote za SADC huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja juhudhi zote ambazo tunafanya za kujenga reli mpya na kukarabati ya zamani reli ya TAZARA tuisihau katika uchumi wa jiografia. Yenyewe inahitaji tuiweke umeme ibaki hivyo hivyo ni *cap gauge* tuiwekee umeme ili tuweze kuweka ma-*train* ya kwenda kwa kasi. Vilevile Serikali inaponunua mabehewa sasa, mabehewa ya hii reli mpya ya *standard gauge* inunue mabehewa na vichwa ambavyo ni *adjustable* ili viweze kutumika katika reli zote tatu. Vitumike kwenye SGR, vitumike kwenye *meter gage* na vitumike reli ya TAZARA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba niisihi sana Serikali, imejenga uwanja wa ndege wa Songwe,

ni jambo nzuri sana, inahudumia *Southern Highlands* yote pamoja Nchi za Kusini mwa Afrika jambo nzuri sana. Hata hivyo, huu uwanja wa ndege hauna ukuta wa usalama, jengo la abiria halijakamilika, taa za kuongoza ndege hazipo, ni kama Serikali imekula ng'ombe wote, lakini mkia imebakiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara mbili nimeruka na ndege kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya tumeshindwa kutua tumerudi Dar es Salaam. Ni hasara sana kwa shirika la ndege lakini vile vile inamuumiza yule abiria sana kwenye mwili wake. Naomba sana Serikali ifanye juhudzi zote ili kukamilisha kujenga ukuta wa usalama, waweke hizo taa za kuongoza ndege na wakamilishe ujenzi wa jengo la abiria ili uwanja wa ndege wa Songwe uendelee kuhudumia *Southern Highlands* kama ilivyopangwa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea kwa kifupi inatosha, lakini naomba sana kusisitiza sana kwamba, napongeza sana hizi juhudzi za Serikali za kuweka *Electronic Tax Stamps* ambazo zitakuza mapato ya Serikali mara dufu na zitapunguza wananchi kuweza kuathirika kwa kunywa gongo na *product* nyiningine za ajabu ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwambalaswa. Tunaendelea na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na baadaye Mheshimiwa Peter John Kadutu ajiandae.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa mpango mzuri wa maendeleo uliotuletea ikiwemo kuipa kipaumbele Sekta ya Kilimo. Kwenye mpango Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya kilimo kwa kusaidia upatikanaji wa pembejeo, masoko na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijielekeze katika ukulima wa mbogamboga. Katika kilimo hiki cha mbogamboga sasa hivi vijana wamehamasika sana na wakulima wadogo hujunga katika vikundi au mmoja mmoja katika kilimo hiki cha mbogamboga. Kwa bahati njema sana mazao ya mbogamboga yanahitajika ndani ya nchi lakini pia nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni moja usafiri wa ndani kuhakikisha mazao haya yanafika kwa wakati katika maeneo husika lakini pia usafiri wa nje wakati wanapopata tenda za kusafirisha mazao hayo nje ya nchi kunakuwa na tatizo la usafiri kwa kuzingatia kwamba mazao mengi ya matunda na mbogamboga yanatoka kwenye Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na kwingine. Ni vyema sasa Serikali ikaimarisha Kiwanja cha Ndege cha Songwe ili wakulima na wasindikaji na wazalishaji wa maeneo hayo wapate urahisi wa kusafirisha mazao yao nje ya nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika ukulima huu wa mbogamboga napenda niongelee kuhusu suala la vifaa vya kilimo na hususani vifaa vya kilimo vya mbogamboga kama *green house*. Vifaa hivi vya kilimo vinatozwa VAT vya asilimia 18 na kwa maana hiyo sasa mkulima mdogo au kijana aliyemaliza masomo yake anataka kujingiza kwenye ukulima huu wa *green house*, vifaa hivi vinakuwa ni vya bei kubwa sana. Hivyo, anashindwa kuwekeza kwa maana ya vifaa vyenyewe kwamba vifaa vya ujenzi, vifaa vya mipira ya kumwagilia na vinginevyo vinakuwa na garama kubwa sana ambapo vijana na wakulima wadogo wanashindwa. Naomba Serikali iliangalie hili kwa upana ili kupunguza VAT hii ya asilimia 18 kwa vifaa vya uzalishaji wa matunda *green house* na nyinginezo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea dhamana ya mikopo kwa wakulima wadogo na vikundi vidogo vidogo vya wakulima imekuwa ni tatizo kupata mikopo kutokana na kwamba hawana dhamana yoyote ambayo itawalinda kupata mikopo hiyo. Naomba sasa Serikali itafute njia bora zaidi na nyepesi zaidi ambayo itakuwa kama ni dhamana

kwa vijana wetu na vikundi vyetu vidogo vidogo vya wakulima kuweza kukopesheka. Kwenye sekta hiyo ya kilimo kuna tatizo pia kwenye kodi kubwa VAT ya vifungashio. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vMheshimiwa Mwenyekiti, ifungashio vya mazao ya kilimo na mbogamboga imekuwa na VAT kubwa ambapo wakulima wanashindwa sasa kuhimili vile vifungashio vyenye ubora ambavyo vitawezu kusababisha kusafirisha mazao yao nje ya nchi na badala yake wanajikuta mazao yao tunauziana wenywewe hapa ndani ya nchi na tunakosa soko la nje lakini pia tunakosa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili Mheshimiwa Waziri alizingatia kwenye vifungashio pia vya mazao ya kilimo na mbogamboga. Kwa sababu sasa hivi wawekezaji wetu wa kilimo wanaagiza vifungashio kutoka nje ya nchi na kuviingiza Tanzania. Tufanye mipango sasa vifungashio hivi vizalishwe ndani ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tozo nyingi ambazo zinamfanya mwekezaji kuwa na mlolongo mkubwa wa tozo mbalimbali. Naiomba Serikali sasa iziangalie tozo hizi ziweke mazingira wezeshi itakayomfanya mwekezaji awe analipa eneo moja tu na kumaliza shughuli zake na kuanza kuwekeza, tujenge mazingira wezeshi kwa wawekezaji wetu wa nje na ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea hapo hapo ssa hivi naigusa sekta ya maziwa. Sekta ya maziwa inatupa lishe lakini pia inatupa afya bora na kwa kuzingatia kwamba maziwa yanapozalishwa yanakuwa na matatizo na mambo madogo madogo ambapo tunahasishwa sasa tunywe maziwa yaliyosindikwa ambayo ndiyo yenye ubora kwa afya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo kwenye uwekezaji wa sekta ya maziwa nako pia kuna mlolongo mkubwa wa kulipa vitu mbalimbali kama hiyo mambo ya

fire, VAT na vinginevyo ni vingi sana mpaka wazalishaji wa maziwa wanashindwa sasa kuhimili vile vikwazo vidogo, naomba hizi changamoto ndogo ndogo Serikali iziangalie kwa hawa wawekezaji wa maziwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye sekta hiyo ya maziwa ukiondoa hayo mlolongo wa mambo hayo mambo yanatakiwa kulipa, kwenye kuwekeza maziwa, maziwa yanayozalishwa kwa muda mfupi hayatozwi VAT lakin ukizalisha maziwa ya muda mrefu yanatozwa VAT. Kwa maana hiyo sasa wawekezaji wanaweka kwenya maziwa ambayo ya muda mfupi ambayo hayatozi VAT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema sasa tukaliangalia hili ili wawekezaji wetu wawekeze maziwa muda mrefu ili waweze kusafirisha nje ya nchi kwa sababu yatakuwa yanadumu kwa muda mrefu na tutapunguza lile tatizo la sisi kuagiza maziwa kutoka nje na kuyaingiza ndani ya nchi kwa sababu ya kwetu sisi ni ya muda mfupi yake yanatoka nje ya muda mrefu, hili nafikiri tuliangalie sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwenye sekta ya maji kwa kuwa tuliomba tuongezewe Sh.50 kwenye lita ya mafuta kwa ajili ya Mfuko wa Maji, nashauri Serikali kama hili haliwezekani tutafute njia mpya njia mbadala ya kuongezea huu Mfuko wa Maji ili tuweze kutatua matatizo ya maji ndani ya nchi yetu. Kilio kikubwa kimekuwa kwenye maji na tumeweka kwenye mpango kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji tutahitaji maji, tutahitaji mabwawa, tutahitaji visima. Kwa hivyo ni vyema pia tukaliangalia ili kuongeza kwenye Mfuko wa Maji ili tuweze kujenga hayo mabwawa, visima na miundombinu mingine ya umwagiliaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwenye sekta ya uvuvi, ni vyema pia Serikali ikaiangalia kwa upana wake sekta ya uvuvi. Sekta ya uvuvi ni eneo moja ambalo litaipatia Tanzania fedha za kigeni, litaipatia ajira vijana wetu pia tutapata lishe bora kwa kula samaki ambapo watakuwa wengi tunawavua hapa nchini. Pia tujikite katika uwekezaji,

naomba Serikali, hii bandari ya uvuvi ipewe kipaumbele ili imalizike na baada ya kumalizika kwa bandari ya uvuvi, Serikali sasa tumeshajikita katika kununua ndege sasa tujikite tena pia Serikali kwenye kununua meli ya uvuvi. Naipongeza Serikali kwa hilo, tumenunua ndege sasa tujikite tena tujipange, tujifunge mkanda, tununue meli ya uvuvi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na suala la umeme. Umeme ni uchumi, umeme ni siasa na umeme ni usalama. Huduma hii ya umeme katika bajeti ya mwaka jana tulizungumzia kuhusu suala la umeme Zanzibar baina ya *ZECO* na Shirika la Umeme *TANESCO*. Tunaomba sasa huu mchakato umalizike kwa kuwa mtumiaji wa umeme wa Zazibar inabidi alipe *VAT* mara mbili kwa sababu tukinunua umeme tunalipa *VAT*, mtumiaji mdogo analipwa *VAT*sasa ni vyema sasa *VAT* hii iwekewe mikakati iwe inalipwa sehemu moja tu ili kumpunguzia mzigo mwananchi mdogo ili asielemewe na mzigo na kwa sababu hii ndio maana kumekuwa na malimbikizo makubwa sana ya umeme kule Zanzibar kwa sababu suala hili bado halijapita ufumbuzi wapi *VAT* hii ilipwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwenye huduma za mama, afya na mtoto; naipongeza Serikali kwa kulipa kipaumbele suala la afya ya mama na mtoto. Pia naiomba Serikali kila kwenye kituo cha afya basi iweke chumba cha kujifungulia mama na mtoto na chumba pia cha kupumzika baada ya kujifungua ili kuweka usalama wa mama na mtoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali za kusamehe kodi mbalimbali za kilimo ikiwemo mambo ya ngozi na mambo mengine ya kilimo. Hapa naipongeza Serikali sana kwa kuliona hili, lakini pia nataka Serikali itupie macho katika haya mambo niliyoinisha kwenye sekta ya maziwa, sekta ya mbogamboga na sekta nyingine za uvuvi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khadija. Tunaendelea na Mheshimiwa Kadutu, baadaye Mheshimiwa Peter Msigwe ajiandae.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili nitoe mchango wangu kidogo kwa bajeti Kuu ya Serikali. La kwanza nizungumzie mambo ya jumla, kwenye jimbo letu kuna mambo hayajanyooka. Kumekuwa na shida, uchaguzi kila siku napiga kelele uchaguzi wa kata zetu tatu haukufanyika na mpaka sasa Serikali haijatoa maelezo yoyote kwamba nini kitafanyika, lakini watu hawa wamemchagua Rais, wamemchagua Mbunge, lakini kama tuliwapa uraia hawa kwa masharti ni vizuri tukaondoa masharti. Nchi yetu kama ilitoa uraia kwa nia njema, lakini tunaanza kuwabagua na jambo hili sio zuri sana kwa mustakabali wa maeneo yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niseme Waheshimiwa Mawaziri waache kubagua, watembelee na majimbo mengine hata kama, niishie tu kusema hata kama. Mawaziri kuna maeneo wanapishana Mawaziri wanne wanakwenda sehemu moja, tunashuhudia lakini kuna maeneo kama Uliyankulu hawataki kabisa kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka afike Waziri Mkuu na Waziri Mkuu alikuja kutusalimia kwa sababu alikuwa *DC* wetu, lakini wengine kila siku hapa tunapigizana kelele, lakini mtu akiuliza hapa, hii nazungumzia mimi Waziri atakwambia tu niko tayari kuambatana na wewe, lakini muda ukifika ziara inapeperuka. Wananchi wetu wanakata tamaa kwamba hili eneo lilitengwa toka miaka yote toka enzi za Mzee Maswanywa, Mzee Sitta, Mzee Kapuya watu hawaii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Uliyankulu linataka dhamira ya dhati, kama hawatupendi sisi tutajua namna ya kupendwa. Nawasihi sana waje bwana, basi waje waangalie tu hata kaburi la Mirambo, hawataki na yenywewe, nadhani wamenisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kumaliza habari ya wakimbizi na kambi za wakimbizi ni jambo muhimu likaisha kama kuna sheria tunaziona ngumu, kama tunaona uamuzi wetu wa kuwapa uraia ulikuwa na shida tutamke, watu hawa sasa hawawezi kujenga kwa sababu kambi haijafungwa lakini ndani ya kambi kuna watu hawataki uraia wa Tanzania na hawataki kurudi Burundi, tunafanya nini? Najua mdogo wangu Mheshimiwa Mwigulu ananisikia vizuri na anajua vizuri. Kama Serikali walimalize hili kwa hiyo, watu wamekaa pale *stranded* hawajui kama watahamishwa au kama wataendelea kukaa hapo, matokeo yake wanatufikiria tofauti hasa wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema wakati mwingine wanasema nasema sana, nimechaguliwa asilimia 70 ya raia wake wamenichagua, sasa piga hesabu wakigeuka? Ndio hofu lazima tuambizane, wakigeuka ni matatizo. Haya mara waseme hifadhi, kwa hiyo sisi watu wa Ulyankulu tupo tu kwa sababu watapita watatoka Tabora, wataenda Kaliua, Urambo, wataenda Kigoma lakini Ulyankulu lazima aje Ulyankulu awe na dhamira kweli leo nakwenda kwa Mheshimiwa Kadutu, hivi hivi hatuwezi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuliwahi kusema hapa suala la kugawa maeneo, lakini sasa hivi Serikali inasema wanabana matumizi hawataki kugawa maeneo. Jamani Tabora ilivyo, hiyo sehemu ya Sumbawanga ilikuwa Tabora, Katavi yote ni Tabora, mkoa bado ni mkubwa kuliko kawaida, wataugawa lini, mpaka watakapotaka kuwagawia wengine ndio na sisi watupitishie humo, hiyo sio haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ipo siku hapa tutasimangana hapa, kuna eneo watatoa eneo jipya la utawala ndio watakumbuka sasa na Ulyankulu. Tunataka sisi Ulyankulu iwe Wilaya, iwe halmashauri na uwezo huo tunao *own source* ya Wilaya ya Kaliua ndio inayoongoza kwa Mkoa wa Tabora kuliko hao wengine, sisi tunaweza kuleta hapa *own source* Bahi, nani wote hawa tukawasaidia, lakini hawataki kutupa eneo, sijui mpaka lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema ahadi za Rais zitatekelezwa, sasa hii ni ahadi ya Rais wakati wa uchaguzi. Wakati wa uchaguzi kulikuwa na mambo mawili, kuna ahadi za Rais, lakini kuna llani ya Uchaguzi. Sasa hizi ni ahadi za Rais alituambia siku tatu akiingia ofisini tunapata Wilaya na tunapata halmashauri, lakini mpaka leo! Sasa wameleta habari kwamba ghamama kubwa na nini, lakini yako maeneo madogo wamewapa mkoa, wengine wilaya, watukumbuke basi na sisi Mkoa wa Tabora. Upo mkoa tulishapendekeza Mkoa wa Nzega na Mkoa wa Urambo ambao JK aliacha amependekeza. Sasa yale yalijotendwa na wazee wetu walioondoka tuyatekeleze basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi zile zilizomo ndani ya ilani lazima tujipime, sasa tumebakiza labda mwaka mmoja tu na nusu, je, tumetekeleza kwa kiwango gani? Yako mambo mengi hivi hakuna hata uratibu wa kuyaondoa moja baada ya lingine, wametuahidi lami, wametuahidi hiki tena ndogo ndogo tu kilomita tatu, kilomita ngapi, hakuna hata dalili. Hata hivyo, tunakuwa tunaona yapo mambo ambayo hayamo kwenye ahadi, hayapo kwenye ilani yanatekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatupendi kwa kweli kuyasema lakini wakati mwingine hivi watu wa Ulyankulu huko wamenituma, halafu nakaa napiga makofi tu hapa mimi siwezi bwana. Tusaidieni ili hata uchaguzi wa 2020 watu mpete, hata tukisimama pale tunapiga kampeni wakati huo mimi mstaafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumze sasa juu ya fedha za maendeleo, hapa juzi wenzangu wamezungumza wengi tu hapa juzi wakaitwa Wenyeviti na Wakurugenzi hapa, tumewaita wapangue mpango huu, tunataka miradi ya mkakati tutatoa huko miradi midogo midogo achaneni nayo, wakaja hapa wakamaliza wakarudi kwenye halmashauri wakaitisha *Finance* pamoja na Baraza, watu wakalamba posho. Leo hii ni tarehe 20 maana yake zimebaki siku 10 tu, watuambie Serikali wanao uwezo kweli wa kuleta pesa kule? Kwa

maana hiyo, Mheshimiwa Waziri ni kwamba halmashauri zile ambazo hazina *own source* zitakufa kifo cha kimya kimya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nimetoka huko kwenye halmashauri, nazijua vizuri kweli, lakini wakati mwingine tarehe 28 wataingiza pesa ambayo haitatumika mwisho wa mwaka na *CAG* atahoji kwamba hizi pesa vipi mbona hawakuzitumia tutaleta maswali mengine. Mheshimiwa Dkt. Mpango ajaribu katika hali ya kibinadamu sasa juu ya madeni ya mawakala wa pembejeo na wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi uhakiki wa mawakala ambao hawafiki 1,000 unaweza kufanana na wafanyakazi zaidi ya 800,000. Wafanyakazi mnahakiki na imejulikana huyu tupa kule huyu huku, tupa huku, kazi imekwisha. Hivi uhakiki wa madeni ya wazabuni pamoja na mawakala wa pembejeo hivi kweli hawaoni ni tatizo. Mawakala sasa hao kila Bunge wapo hapa na wakati mwingine wanaishiwa hata pesa ya kula. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tunahangaika kuwalisha, siku moja Mheshimiwa Jacqueline hapa mpaka analia, hivi kweli wanataka watu tuanze kulia wote huko haifai. Kazi leo Mheshimiwa Waziri waifanye tu kwa nia ya kibinadamu kwamba watu wamekopa maeneo, sasa hata mali zao watafilisiwa. Kama mtu alidanganya watoe basi orodha, hawa wafuatao ndio wako halali, hawa wengine utapeli *jazz band*. Watu watajua ili jambo hili lifike mwisho kwa sababu sasa kwa mfano sisi wengine vijiji huko na kilimo kwa mfano cha tumbaku, yaani bila mbolea huwezi kufanikiwa, bila mtu kukusaidia wakulima wetu wamezoea hiyo, hawana nguvu za kununua pembejeo wenywewe, tusaidieni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje suala la kilimo; kwenye vitabu vya Mheshimiwa Waziri amesema kweli kwamba pato la Serikali asilimia 30 linatokana na kilimo, lakini hebu atafakari mwenywewe, kilimo wameipa asilimia ngapi basi ya pesa hizi?

Maana kilimo hatukizingatii. Mwaka jana hapa zao letu la tumbaku maana yake sisi ukizungumza siasa lazima uzungumzie tumbaku hata kama huipendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Serikali ika-*delay*kutoa uamuzi, niseme tu natoka kwenye eneo linalolimwa tumbaku nyingi Tanzania, kwa hiyo, najua vizuri. Matokeo yake hapa tukajichanganya Serikali imechelewa kutoa maamuzi wakulima wetu wamekwenda kuuza tumbaku kwa bei ya chini *zero point*. Wamepata hasara, mtu alikuwa ame-*plan* kupata milioni ishirini, anaishia milioni mbili laki tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali lazima iangalie, hili zao tunasema asilimia thelathini ya pesa inakwenda Serikalini inazalisha mazao ya kilimo, lakini sisi hatutaki kuhudumia kilimo. Unasikia korosho wanalamika, kahawa wanalamika, ndugu zangu kule Kanda ya Ziwa pamba wanalamika, kilimo kipi sasa ambacho tumefanikiwa matikiti? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda matikiti yamekuwa mengi, mtu anaweza akasimama hapa akasema tumefanikiwa, lakini kila eneo la kilimo, kelele hata kwa ndugu zangu kule Wanging'ombe maua sijui nini, wote kule ni malalamiko. Hakuna yaani sijui lumbesa sasa haitajwi yaani shida tupu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, wajaribu kukaa, kweli wote humu hatuwezi kuwa wachumi, lakini tuna macho na akili. Tunaona, mambo haya wayarekebishe twende mbele, tumebakiza mwaka mmoja tu, yaani bajeti yenye kuweza kujadili kwa utulivu imebaki moja, ile nyingine watu wote humu watakuwa akili kwenye uchaguzi. Hakuna tena majimboni, watu wanatafakari nani ananifuatafuata huku, hakutakuwa na mjadala mzuri, umebakii mmoja, hebu wajaribu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lingine tumeshafanya Serikali imefanya mambo hayo makubwa ya ununuzi wa ndege, sijui ujenzi wa reli, hebu sasa twende kwa wananchi

wa kawaida, yale mapato ya pesa, watu wapate wananchi wa kawaida wazione. Unajua ukimweleza mwininge, kwa mfano, kule Ulyankulu ukimweleza habari ya *bombadier*mimi nasema ukweli tu, wakinichukia na wanichukie, *bombadier* mfano Ulyankulu wao wanaamini hizi hela za Serikali zinatokana na tumbaku. Sasa ukiwaeleza habari za *bombardier*, barabara mbovu, hospitali mbovu hawaelewii wapeleke sasa huduma hizi ziende kwa wananchi, barabara kule vijijini ziboreshwii, hao *TARURA* wapewe pesa, tutakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapa.. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa John Peter Kadutu. Tunaendelea na Mheshimiwa Peter Msigwa baadaye Mheshimiwa Yusuph Salim na Mheshimiwa Devota Minja wajiandae.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Niseme tu katikati ya Bunge kwamba nasikitika tu kwamba, kwa sisi tuliokuwepo Bunge liliopita kabla ya Bunge halijaanza tulikuwa tumepeewa semina elekezi pale *Blue Peal* Dar es Salaam, kutenganisha mihimilli hii mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi wakati mwininge sisi kama Wabunge tunasahau kabisa mhimili wetu una kazi gani dhidi ya Serikali. Kama Bunge lingekuwa linafanya kazi yake vizuri huu ndio wakati wa kuonesha power ya Bunge dhidi ya Serikali. Hii *separation of power* iliwekwa makusudi kwa sababu binadamu ana tabia ya ubinaksi, anataka yeye awe juu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ilivyowekwa Mahakama, Bunge na Serikali ni kuhakikisha yule anayeinuka zaidi avutwe mkia. Sasa kwa bahati mbaya Bunge letu tunadhani Serikali ina nguvu kuliko sisi. Ndio maana Wabunge wengi hapa wanapiga magoti na kuombaomba wakati Serikali kimsingi kupitia Waziri wa Fedha imekuja hapa

kutuomba sisi tuidhinishe kutumia matumizi hayo. Ni wakati huu ambao Bunge lilitakiwa liiadabishe Serikali kwa matumizi ambayo Bunge halikuidhinisha. Sasa kwa sababu hatujui nguvu ya Bunge tumekuja hapa tunajibembeleza na naomba zahanati, naomba *dispensary*, naomba Kituo cha Afya wakati haya mambo ndio wakati wa Bunge kusema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wa Wabunge kujua *what is our power*, nguvu zetu ni zipi? Ndio maana CAG amekuja hapa ambaye ni jicho la Serikali, ni jicho la Bunge. Yeye ni Mkaguzi baada ya Serikali kuomba ruhusa ya kutumia pesa, sisi hatuna uwezo wa kwenda kukagua huko, CAG amekwenda kukagua kwa niaba yetu, anakuja anasema nimeona hili, nimeona hili halijapangwa vizuri, Wabunge wengine hapa wanamlaumu CAG. *Ignorance* ya kujua wajibu wetu kama Wabunge na hii tuna li-cripple Bunge tunasababisha watu wengine ambao ni wabinafsi wakue zaidi kuliko Bunge linavyotakiwa liwepo. Niwaombe ndugu zangu na nimpongeze Mheshimiwa Kadutu amefanya kazi ya Kibunge bila kujali itikadi za vyama kwa matatizo tuliyonayo kwenye majimbo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango; mara tu alivyochukua Uwaziri alipoanza hapa alikuwa anahutubia kama yupo kwenye *Lecture room*, alikuwa kinadharia sana. Tulikwambia *this is not a lecture room*, sisi tupo kwenye *ground*. Tunakutana na watu, tunaishi na watu, hizi kodi ambazo leo amezitoa *we told you three years back*, kwamba hizi kodi zitaleta matatizo kwenye uchumi *you never listen*. Sasa hivi amerudi kwenye mgongo mwingine, halafu Wabunge hapa wanasema tunampongeza, tunaipongeza Serikali, yeye ndiye alitupeleka kule. Bado tunaendelea kusitiza, huu utaratibu wa uchumi unaokwenda sasa hivi, huko mbele tunakwenda ku-crush na utaweka historia tunakwenda ku-crush kwa sababu uchumi tunaokwenda nao sio halisia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi Mheshimiwa Sugu amesema hapa sisi tunaozungumza, najua Mheshimiwa Rais

anasikia, *actually* sisi ndio tunaompenda Rais kuliko wengi wenu huko. Kwa sababu wanampaka Rais kwa mgongo wa chupa hawamwambii ukweli. *They economy going crush* kwa sababu huwezi kuniambia uchumi unakuwa, toka Serikali ya Awamu ya Tano nimeingia kwenye jimbo langu akinamama wale wengine wameuziwa *fridge* au wamenyang'anywa, wamenyang'anywa *television* na makochi kwa sababu hawawezi kulipa mikopo. Sasa utaniambiaje uchumi unakua kwa sababu hawawezi kufanya *business*, uchumi haukui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimuulize swalii Mheshimiwa Mpango, naomba anijibu *honestly*, Serikali ya Awamu ya Tano inaendesha hii nchi utadhania sisi ni Sudan ya Kusini, *trial and error* ambayo imezaliwa juzi. Serikali hii haina *consistency* kwa sababu nchi hii tokea tumepata uhuru ni Chama cha Mapinduzi kimekuwa kikitawala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana wakati wa Mwalimu Nyerere kuna makosa mengine aliyafanya aliendelea kurekebisha kwa mfano hizi Serikali za Mitaa aliwahi ku-*centralize* akaona makosa akarudisha. Tunaweza tukamsamehe kwa sababu ndio kwanza tulikuwa tunapata Uhuru, Iakini alivyokuja Mheshimiwa Mwinyi tukahama *direction*, tukahama mwelekeo, tukaacha mambo ya ujamaa, tukawa na *free market* katika nchi hii. Alivyokuja Mheshimiwa Mkapa naye akaanza, tukaanza kuweka wawekezaji akatengeneza mazingira ya wawekezaji tukaanza kuwa *friendly* kwa wageni ambaa tuliwafukuza mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja Mheshimiwa Dkt. Kikwete ametengeneza mazingira mazuri ya kuwa na marafiki wa nje, kuwafanya *investors* waje. Sasa swalii kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango aniambie namwona hapa wakati wa Mheshimiwa Kikwete alikuwa Katibu wa Tume ya Mipango ambayo sasa hivi unataka kuifuta. Wakati wa Rais Mheshimiwa Dkt. Kikwete, Mheshimiwa Dkt. Mpango alisimamia Kilimo kwanza, alisimamia *SAGCOT*, alisimamia *Big Results Now*, alisimamia Gesi, alisimamia *PPP* na wali-encourage *D by D*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye Awamu ya Tano amegeuka, ameenda kwenye mambo ya Stiegler's Gorge, kwenye *Standard Gauge* ambayo mikopo yote hii anaichukua sio *concessional loans*, anachukua mikopo ambayo ni ya gharama kwa nchi hii, *tell us wewe ni mchumi unayeamini nini?* Atuambie hapa uchumi ule aliokuwa anaendesha Mheshimiwa Dkt. Kikwete ambaye alitengeneza mazingira mazuri ulikuwa na makosa au alimuingiza chaka? Sasa hivi ameweka *u-turn, where are we heading as a Nation?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wakati wa Serikali ya Kikwete ulikuwa una-*embrace investors*, ulikuwa una mazingira mazuri ya kuwaleta wawekezaji. Uchumi huu unagombana na wawekezaji, wanaonekana wote wizi katika uchumi huu ambao ye ye ndiye Waziri. Wafanyabiashara wote wanaonekana ni wezi, wafanyabiashara wanaonekana hawalipi kodi, atuambie ni uchumi upi ambao anauamini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu ye ye sio mchumi, ni *engineer*, tunategemea Mheshimiwa Waziri ambaye ni Mchumi ampe maekelezo mazuri ambayo yatasaidia nchi yetu iende. Leo naongea kwa masikitiko makubwa kwa sababu tunaua *Local Governments* kwa uchumi wa namna hii, vyanzo vyote amechukua kwenye *Local Government* anavileta *Central Government* kuna maumivu makubwa ambayo yanapatikana kwenye *Local Government*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango atoe majibu ni uchumi upi anauamini, *what do you believe as an economics?* Nani anamdanganya kati ya Mheshimiwa Dkt. Kikwete na Rais wa sasa? Kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Kikwete alitengeneza mazingira pamoja na udhaifu wa Serikali ya Awamu ya Nne, alitengeneza mazingira mazuri ya kuwa na mahusiano na watu wa nje, aliletta wawekezaji kulikuwa na mazingira mazuri, leo haya yoote umeyakataa, leo uko kwenye... (*Makofii*)

TAARIFA

MWENYEKITI: Mheshimiwa Peter taarifa tumsikilize.

MBUNGE FULANI: Hivi mbona nyie Mawaziri hamuwi wavumilivu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji ni kwamba, kimsingi sisi sote tunafahamu kwamba katika shughuli tulizokuwa tunafanya mojawapo ya mambo yaliyokuwa yanaangaliwa ni mazingira mazuri ya uwekezaji. Pia changamoto mojawapo iliyokuwepo ni tatizo la umeme, sisi sote tumeshuhudia humu kukiwa kunatokea migawo ya umeme, kukiwa na changamoto za hali juu na leo sasa zinavyochukuliwa hatua kama hizo, mtu anavyokuwa huwezi ku-*appreciate*, nadhani sio jambo jema.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Peter Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namtaka Mheshimiwa Dkt. Mpango aniambie kichumi, nimesema wakati wa Mheshimiwa Dkt. Kikwete yeye alitu-*encourage* kwenye mambo ya *SAGCOT*, *SAGCOT* inazungumza kuhusu umwagiliaji kwamba tumwagilio, *Stiegler's Gorge* inataka bwawa lile lijae. Sasa ni kwa namna gani tunaweza tukatekeleza *SAGCOT* na wakati huo huo tukaenda na *Stiegler's Gorge* kwa maji yaleyale, ambayo upande wa *SAGCOT* tunataka tumwagilio kwenye kilimo cha umwagiliaji na wakati huo huo tunataka bwawa la umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndio mambo ambayo kama Bunge tunatakiwa tujadiliane bila kujali itikadi za vyama. Nasema tutapigana makofi hapa lakini *the economy is sinking* na tunakwenda ku-*crush* sio muda mrefu kwa sababu tunakopa mikopo ambayo ni gharama kubwa. Makusanyo ni triliioni kumi na nne tu na bado tunaenda

kwenye *negative*, hatuna hiyo pesa naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango na juzi nilimuuliza kwenye Wizara yake kwamba ni kiasi gani cha pesa ambacho ni cha *TRA*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu Mheshimiwa Dkt. Sware amezungumza hapa hela zote ambazo wanadaiwa hizo ni kiasi gani ambacho wanakusanya kwenye *TRA*, lakini tukija hapa tunapongezana pongezan. Huu ndio wakati wa kuonesha *the power of the Parliament*. Tulitakiwa tushikamane kwamba ni kwa nini Serikali hii inalikosea adabu Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuuliza kwa nini Serikali inafungua miradi ambayo Bunge halijapitisha. Inaanza kuanzisha halafu tumekaa hapa tunapigania makofi kwa sababu Serikali ikileta maji kwenye jimbo langu *is not a fever am the tax payer representative*, mimi nawakilisha wapiga Kura wangu kule, kwa hiyo, siwezi kumpigia magoti Mheshimiwa Dkt. Mpango hapa. (*Makof*)

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa Taarifa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuu kumpa taarifa Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwamba suala la kupongezana hata yeye analijua na anajua ni kwa kiasi gani kwamba Serikali imefanya mambo makubwa kwenye Jiji la Iringa. Muda mfupi uliopita wakati tukiwa kwenye sherehe za Mei mosi Mheshimiwa Mchungaji Msigwa alimsifia sna Mheshimiwa Rais na alifisia sana Serikali yetu kwamba imefanya mambo makubwa sana hata katika Jimbo la Iringa Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokifanya hapa sisi kuipongeza Serikali kinafanana na kilekile ambacho

ye ye alikifanya pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya kwenye Jimbo la Iringa Mjini. Kwa hiyo tunafanya kazi ya kupongeza mazuri kama Mheshimiwa Mchungaji Msigwa alivyoongoza njia nzuri ya kupongeza mazuri yaliyofanywa na Serikali yetu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Peter Msigwa taarifa hiyo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi *is crying for my endorsement, am smart enough*, nikitaka kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Magufuli naweza kuchukua *TBC* au *ITV*. Msiwe mnavizavizia ndio nasema hapa simpongezi hapa ndio nasema sasa simpongezi kwa sababu ana washauri ambao mnampotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi huko nje wanalalamika, *there is no money kwenye mifuko*, haya ndio ya kujadili kama Bunge, wengi huko mitaani kwenye majimbo yetu mimi saa hizi ukienda jimboni kwangu file la mahitaji liko hivi. Limekaa hivi, sijasoma nahitaji mtoto shule, ada, sijui nini, mafaili makubwa yamejaa hivi, hata mimi mwenyewe sina hela na nyie wenyewe ndio hayohayo, halafu tukija hapa tunadanganyana. Tuoneshe nguvu ya Bunge wewe mwenyewe Mheshimiwa Jenista unalalamika huna hela, tukikaa, saa hizi tuanze kukaa tunadanganyana tunapongezana, hakuna hela, huu uchumi Mheshimiwa Spika amezungumza asubuhi hapa uchumi kila mtu anao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema juzi *I am a theologian by profession*, lakini huwezi kuniambia kwamba siwezi kuguswa kama hamna hela! Hata mama kule nyumbani anajua kama uchumi umekaa vibaya, uchumi haupo, tusidanganyane hapa, haukui! Wazimbabwe wanasema mtoto ambaye analia njaa leo huwezi kumwambia jana nilikupa chakula. Hakuna chakula huko mitaani tusidanganyane hapa hakuna chakula, hayo mambo ya ndege, kwanza ndege wametuletea *disaster*, wanapata hasara halafu hawasemi hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo lazima tujadili kama Bunge na lazima tuoneshe *power* kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango kwamba lazima awajibike. Hela ambazo ametumia bila kupata vibali vya Bunge anatakiwa awajibike. Sasa tumekaa hapa tunapongezana ametumia hela nyingi bila kibali cha Bunge, sasa Bunge lina kazi gani? Vinginevyo Bunge limemezwa, linawafanya wale watu wabinafsi wainuke zaidi.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Peter, nilikuongezea kengele ilishalia mwanzo. Tunaendelea na Mheshimiwa Yussuf Salim, baadaye Mheshimiwa Devota Minja ajiandae.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: *Bismillah Rahman Rahiim.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango na Naibu Waziri wake na kwa sababu bado tunaendelea na swaumu basi nitazungumza kwa upole na kuwashauri zaidi. Hivi Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri hawa watu wanaposimama wakalalamika kwamba hakuna fedha huko mitaani, Mawaziri wanaposimama kwamba hawajapelekewa fedha, fedha za halmashauri haziendi, fedha zinatumika vibaya hazionekani, hivi wao kama waungwana haya hayawaumi? Kwa nini hawajitathimini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawashauri leo kwa nini wanakosa fedha, watu wa fedha wataalam wa mambo ya mahesabu ya pesa wametuambia hapa, kwamba tuna upungufu ya trillioni 1.2 ili kuweza kukidhi mahitaji yetu. Sasa kwa nini hawazipati? Hawazipati kwa sababu wakiwa katika mipango yao bado hawajapanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi siku zote huwa nazungumza humu, Tanzania kamwe tusitegemee

maendeleo kama nchi wakati hatuna *National vision*, hatuna tunataka nini? Leo wanaizungumzia Tanzania ya viwanda, nikimuuliza Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango katika kipindi cha miaka kumi na Waziri wa Viwanda yuko hapo, katika kipindi cha miaka kumi tunataka viwanda nya aina gani? Vikubwa vingapi? Viwanda nya aina gani, nya kat i vingapi? Viwanda vidogo nya aina gani vingapi na mkakati wake upi? Hamna. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf subiri, Mheshimiwa Mwijage.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na swaumu niliyonayo nimelazimika kusimama. Tunayo Dira ya Taifa ya kujenga nchi ya uchumi, uchumi wa Taifa, uchumi uliojumuishi, kupitia uchumi wa viwanda. Tunajenga viwanda vile ambavyo vinachakata mali zinazopatikana nchini, lakini tunatengeneza viwanda ambavyo vinazalisha bidhaa nyngi zinazotumika. Katika kundi hilo tumebakiza *item* mbili mafuta ya kula na madawa na tunatengeneza viwanda ambavyo vinatumia rasilimali tulizopewa na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, *vision* ipo, mpango upo na mkakati wa maunganisho nausimamia mimi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Yussuf.

MHE. YUSSUF S. HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru namheshimu sana msanii huyu. Nazungumza tena atuambie suala la maendeleo ya nchi huwezi kulipima kwa mwaka mmoja au miwili au mitatu. Tukubaliane hapa nawasaidia tukubaliane huwezi kupima maendeleo ya nchi kwa miaka miwili, mitatu, sasa ndani ya mwaka mmoja hadi miaka 10 utuambie tunataka viwanda vidogo hamsini na mkakati wake huu na vitapatikana hivi, hivi, hivi. Tunataka viwanda nya kat i ya ishirini vitapatikana hivi na mkakati wake huu. Tunataka viwanda vikubwa vitano vitapatikana hivi, hamna hicho kitu ni usanii tu, sawa. Sasa nawapa *really* mifano wakajifunze. (*Makofii*)

MHE. ALLY M. KEISSY: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Ally Keissy hebu kaa chini, usitake kuniharibia, mie nafundisha watu biashara hapa, usitake kuniharibia, kaa chini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf, subiri atoe taarifa yake. Mheshimiwa Keissy.

TAARIFA

MHE. ALLY M. KEISSY: Mheshimiwa Mwenyekiti, afute kauli yake kumwita Mheshimiwa Waziri msanii. Kusema kweli ni kosa kubwa. Afute kauli yake mara moja kumwita Mheshimiwa Waziri msanii. (*Makofi*)

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: (*Hapa allongea nje ya microphone*)

MHE. ALLY M. KEISSY: Huwezi kumwita Mheshimiwa Waziri msanii. Funga mdomo wako wewe! (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy, naomba ukae chini, Mheshimiwa Yussuf.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Wewe tatizo lako hata kufunga hukufunga. Pilipili usiyoila wewe yakuwashia nini? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia hivi, tuwe na huo mkakati. Sasa nawapa mfano mmoja na waende wakajifunze. Huyu Waziri wa mafuta wa Oman alipoingia pale, wale walikuwa wanazalisha mafuta lita 600,000. Alipoingia akakuta wachimbaji wa mafuta yote ni makampuni ya kigeni. Akataka wazawa wachimbe yale mafuta ili ile fedha izunguke ndani ya nchi yao. Akaenda kwa mfalme akamwomba kiasi cha fedha, akawaita matajiri akawaambia kaeni mchimbe mafuta kwa kiwango hiki kinachotakiwa. Asilimia 50 Serikali itawakopesha na asilimia 50 watoe wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi makampuni yanayochimba mafuta Oman ya kizalendo ni 15. Wanazalisha wenyewe, wafanyakazi ni wao wenyewe na kabla ya hapo hawajaanza wao, walitoa vijana wao kwenda kusoma, wakaja wakasimamia, leo wanasmamia uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kama Serikali wametenga fedha kiasi gani kuwaita wafanyabiashara kwamba wao wanaweza kiwanda kikubwa, waweke kiasi hiki na Serikali itawakopesha kiasi hiki? Tukiwa na viwanda vitatu au vinne kama kile cha *Kagera Sugar*, kina wafanyakazi zaidi ya 3,000 pale, tukawa na hivyo kumi, tutakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na chini ya vile ambavyo vina wafanyakazi 2,500, tutakwenda wapi? Tukiwa na hivi vidogo tutaenda wapi? Leo unasema wapiga matofali ni kiwanda? Kwa hiyo, ni lazima tufanye hivyo. Tukifanya hivyo, fedha itarudi katika muda mfupi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, huwa nazungumza kwa jazba, achukua mantiki ya ninayozungumza, asichukue ukali wa maneno yangu, huwa nazungumza kwa jazba kwa sababu nazungumza kwa uchungu sana, kwamba kwa nini wenzetu waendelee, sisi tushindwe kuendelea? Kwa hiyo, huo ni mfano mmoja ambaao nimetoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili, hapa wanashindwa kukusanya kodi kwa sababu wameharibu biashara; nchi zote hizi. Mozambique, Malawi, Zambia, Uganda, Rwanda, Burundi na Kenya zilikuwa zinakuja Tanzania kununua bidhaa. Sasa kwa sababu wameharibu biashara, kwa sababu hawajui biashara, wamepandisha kodi, wanataka kukusanya kingi kwa wakati mmoja, badala ya kukusanya kidogo kidogo na Waswahili walisema: ndogo ndogo nyingi, si kubwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo toka hapo nje, hao wajasiriamali, hao wadada wanaouza hapo, wanaenda

kuchukua bidhaa Uganda. Kwa nini wakati nchi zote hizo zilikuwa zikija Tanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakija Tanzania kununua maana yake nini? Maana yake hoteli, gesti, migahawa, magari, tunaingiza fedha. Leo wamepandisha kontena hapa hailipiki. Kwa hiyo, bidhaa zile zile zinapita Dar es Salaam, zinaenda Zambia, halafu zinarudi Tanzania zinauzwa. Sisi tunafanya nini? Hivyo ndivyo biashara inavyoendeshwa? Sisi tunazaliwa, hatuna fedha, kwetu siyo matajiri, lakini baba yangu anaauza dagaa kwa fungu, anaauza malimao, kitunguu na binzari; biashara tunajua. Ndogo ndogo nydingi, si kubwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wao wamepandisha ushuru, wafanyabiashara wameacha kuleta biashara, nchi zote hizi za Maziwa Makuu zilikuwa zinakuja Tanzania kununua biashara, leo hawaji tena, ni Watanzania wanatoka kwenda kuchukua mashuka na mashati wanakuja kutuuzia Wabunge hapa. Kwa nini? Ni kiasi gani cha fedha tunapoteza? Kwa hiyo, hebu wakae chini wampange, tuone kwa namna gani tunaweza kupata fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala lingine ambalo litawasaidia kwa haraka kupata fedha. Wameanzisha Reli ya Kati, *Bombardier* na *Stiegler's Gorge*, itawachukua miaka mingapi kurudisha fedha? Nawapa njia nydingine ambayo ni urahisi tu, wataweza kurejesha fedha, ndani ya mwaka mmoja wataanza kuzalisha na kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ukanda huu wa bahari; Tanga mpaka Mtwara. Wahamasisheni wawekezaji wa ndani, wawawezeshe, waweke miundombinu bora, wahamasishie nje wajenge na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utalii yupo hapa, tujenge hoteli angalau 20 katika ukanda ule. Ndani ya mwaka mmoja, tumejenga hoteli *rooms* 50, 50 tu, sawa? Baada ya mwaka mmoja, hoteli hizo tayari wageni wanaingia, pesa ile itaanza kurudi. Sasa tunachukua fedha nydingi tunaenda kuikwamisha! (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mfano mwingine hapa, Bunge lililopita hilo wanalo sema hao tulikuwa tunazungumzia gesi, gesi, gesi. Ni dola milioni ngapi tumekopa tukawekeza kwenye gesi? Leo gesi tayari tumeiacha, tunaenda kwenye *Stiegler's Gorge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni nini sasa? Baya zaidi ni pale n ninaposema hatuna *vision* ni kwamba yale aliyoyaanzisha Mheshimiwa Rais Dkt. Kikwete leo tumeyaacha na ni mamiloni ya pesa, tumeshayaacha tunaanzisha mengine; na haya baada ya miaka 10 akija Rais mwingine yanaaachwa, tunaanzisha mengine. Hili deni la Taifa kila mwaka litaendelea kukua. Wanalaumiwa hivyo, Waheshimiwa hawaoni aibu? Hawaoni tabu kila siku, watu wazima kunyooshewa vidole? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tujipange, tufanye kitu kwa uwezo wetu, tusiongeze kimo kwa kupanda kinu. Hatujafikia huko ambako wanataka kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapa mfano wa utalii, Dubai tu hapo, wanataka kutoka watalii...

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf malizia.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Niache nimalizie dada yangu, au una taarifa muhimu nisimame?

MWENYEKITI: Malizia Mheshimiwa Yussuf.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie Dubai, wanataka kutoka watalii 5,000,000 hadi watalii 10,000,000; wamewawezesha katika *same bank* na *plan* yao wajenge hoteli 150 ikifika 2020. Wana-*import* kila kitu. Kwa hiyo, baada ya miaka mitano ikifika 2020 ndani ya mwaka 2021 wanaanza kuzalisha. Kwa hiyo, kwa nini hatuigi haya mambo mazuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri, waangalie mfumo wa biashara, kwa nini wafanyabiashara wetu waende Uganda na nchi zote za Maziwa Makuu wakati walikuwa wanakuja hapa? Leo hawaji, tunapoteza kiasi gani cha fedha? Warudini katika kujenga angalau hoteli 20 au 30 katika ule ukanda, tutazalisha baada ya mwaka mmoja na fedha nydingi tutapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa kunyooshewa vidole kila siku, watu wazima, sisi wengine inatuumma. Kwa hiyo, nawashauri tuyafanye hayo na tuangalie namna bora. Nami nawaambia tena, katika viwanda hawajajipanga wazee wangu, wajipange vizuri watuambie.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Yussuf. Tunaendelea na Mheshimiwa Devotha Minja, baadaye Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, ajiandae.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kupata fursa hii niweze kuchangia bajeti kuu. Wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha bajeti hii, nilikuwa najaribu kumwangalia sana hata usoni kwamba anachozungumza na kilichomo ndani ya moyo wake kinaonekana ni tofauti kabisa. Nina wasiwasi sana kama Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha haya hivi anakwenda *field* au anatuletea tu taarifa hapa ambazo hajui hali halisi ya uchumi wa nchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri anatuletea taarifa ambayo Deni la Taifa ni shilingi triliuni 46, sisi tunakusanya shilingi triliuni 32, hawa watu wanaotudai wakicharuka, kitakachofanyika ni kwamba nchi itauzwa na

sisi tutauzwa. Kwa maana hiyo, sioni *realistic* ya bajeti yake hapa. Tulitegemea kwamba angekuja na mipango ambayo inatuonesha ni jinsi gani tunakwenda kupunguza hilo deni na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati bajeti inawasilishwa tulikuwa tuki-*observe* pia nchi nyininge zinavyowasilisha bajeti zake. Ukiangalia Kenya, Uganda, Mawaziri wako *serious* wanaonesha ni jinsi gani wamejipanga kuhakikisha bajeti wanayokwenda kuiwasilisha inakuwa na *impact* kwa wananchi wao. Ukija ukiangalia kwetu huku, bajeti siasa, Waziri ashukuru na wananchi wake na majirani zake wa Zuzu na kadhalika. Hakuna mwaka ambao bajeti imekosa mvuto kama huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata waliokuwa wanafuatilia kwenye televisheni, wananchi unawaauliza hivi kwa nini hamfuatilia bajeti? Wananchi wanasesma aah, ni *business as usual*, hakuna jipya, maisha ni magumu. Hawana hata muda watu wa kutoka maofisini wakakae waangalie bajeti ya Serikali inasemaje, kwa sababu hawategemei kuongezewa hata senti tano ya mshahara. Kwa hiyo, lazima tujiulize ni kwa nini wananchi hawako na sisi wakati tunawasilisha vitu muhimu vya Taifa hili? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Waziri anasema kwamba pato la Taifa limepanda. Hivi, kweli limepanda kwa watu gani? Mheshimiwa Waziri aende *field* aone kwa macho yake mawili, pato la Taifa limepanda unapita kila nyumba unakuta imeandikwa inauzwa kwa mnada wa benki fulani? Pato gani hili ambalo limepanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapita huko mtaani, maduka yamefungwa, pato la Taifa limepanda! Mheshimiwa Waziri atuambie, pato la Taifa limepanda, benki zinashusha riba! Namwambia hata zikifikisha asilimia mbili, Watanzania hawana nguvu ya kukopa. Kwa nini? Biashara hazifanyiki. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata mabenki yakazane kushusha riba, kama huu uchumi haujarekebishwa, bado namna ya wananchi kurudisha fedha hizo hawana, wataendelea ku-*default* na ndio maana wanaogopa. Ndicho kilichobaki kwa mabenki sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pato la Taifa limepanda, sasa hivi mpaka Benki za Serikali zenyewe zinashindwa kufanya kazi. Twiga *Bankcorp* juzi wame-*merge* na *Postal Bank*, haina mtaji, imefilisika. Benki ya Wanawake hivi sasa inachechemea, hata kulipa mishahara haiwezi. Pato la Taifa limepanda! (*Makofii*)

Mheshimimiwa Mwenyekiti, tunataka Mheshimiwa Waziri atuambie, hivi hili pato la Taifa kupanda, kuna *impact* gani kwa mwananchi wa kawaida? Tuwe na huruma na hawa wananchi ambao wanakamuliwa, sisi tunapata kulipwa mishahara, kama kweli hatuwezi kuwasemea na kuangalia ni namna gani ya kuwasaidia wananchi hawa wakanyanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri anasema, katika mipango yake, kwenye bajeti hii *TRA* wakakusanye shilingi triliioni 20. Hivi, shilingi triliioni 20 zinakwenda kupatikana kwa namna gani? Nimeangalia kama kuna vyanzo vipyta ambavyo wame-*identify*, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo ni vile vile, watu ni wale wale; hii tunakwenda kuwakamua wananchi mpaka jasho la damu. Kwa sababu ukiangalia *TRA* sasa hivi; namwona Kamishna wa *TRA* anazunguka kama pia; yuko Dodoma, wapi na wapi, eti anaenda kuvizia na yeze watu gani wamenunua bidhaa bila risiti? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Kuna shida *somewhere*. Hakuna hela! Kwa hiyo, anatoka ofisini hakukaliki, anakwenda mikoani naye anakaa vichochoroni kama hawa *junior officers* wanavizia wananchi ambao ni wateja wametoka kununua bidhaa. Haiwezekani! Lazima wafike mahali waone hili kwamba hali ni mbaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika watu wanao-*frustrate* wafanyabiashara ni pamoja na *TRA*. Hivi siku wafanyabiashara wakiamua sasa hawafanyi tena biashara, wanaauza kunde kwa sababu hazina kodi; hivi watapata wapi mapato? Ndipo wanakoelekea hivi sasa, kwa sababu *TRA* sasa hivi wanazunguka na mifuko ya *sulphate* imejaa makufuli kwamba wakikukuta na kikosa kidogo wanafunga kwa sababu wamepewa majukumu kuhakikisha wanakusanya. Kwa hiyo, wafanyeje? Wanatumia nguvu! Kwa hiyo, wanakomoa ili kuhakikisha kwamba makusanyo yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna tena kuelimisha wafanyabiashara kuhusu *TRA*. Mfano mzuri, wengine nasi ni wafanyabiashara, tunajua. Maofisa wa *TRA* wanakuja kwenye biashara yako, asubuhi wanakwambia *print Z Report* na Waziri anaelewa, *Z Report* inatolewa baada ya mtu kuwa amemaliza mauzo yake, anafunga siku. Sasa wewe saa mbili unataka *Z Report*. Kwa maana hiyo unaua *system* nzima ya makusanyo. Halafu wanafungua *draw* wanaangalia una shilingi ngapi? Wana *compare* na *Z Report*. Hivi tunapeleka wapi wafanyabiashara hawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaelewa mfumo wetu wa kutoa risiti za *EFD machine* uko *slow*. Imefika mahali *TRA* mpaka wanapandikiza watu. Wanawaleta *purposively*ili kuhakikisha kwamba akishanunua bidhaa, kwa sababu mfumo wetu siyo kama *petrol station* kwamba ukijaziwa mafuta inatoka, hapana, lazima utumie mikono, dakika tano wakati mwininge *system* iko *down*, uweze kupata risiti. Wanachokifanya, anachukua bidhaa anaondoka, wanakuja Maofisa wanakwambia hujatoa risiti. Kwa hiyo, huu ni uonezi wa hali ya juu. Kama kweli Serikali imeamua kukusanya mapato siyo kwa kuwaonea wafanyabiashara kwa kiwango hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *importation* na *exportation*, nimesikia eti wanataka ku-*discourage importation* ili kulinda viwanda. Viwanda vipi? Leo tunasema kwamba mafuta, mtu anakaa kwenye gari hawazi,

anasema, kuanzia leo hakuna kuingiza mafuta nchini. Uzalishaji wetu wa mafuta ya kula ni asilimia 30. Asilimia 70 tunaiapata wapi? Tunategemea watoe kauli hizo wakati wameshapandisha uzalishaji kwa asilimia 100, ndiyo watuwekee hizo *restrictions* kwamba mafuta yasiingie nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la *importation* na *exportation* ni la kimahusiano zaidi kwa Mataifa na Taifa. Hivi leo tunaweka *restriction*, bidhaa zetu huko nje zinakoenda, zisipopokelewa inakuwaje? Kwa maana hiyo kama mtu anaamua kwamba sasa hakuna kuingiza mafuta kutoka asilimia 25 wamepandisha mpaka 35 mafuta hakuna, nchi ina uwezo asilimia 30, hivi wanataka kuwarudisha wananchi kula chakula bila mafuta? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, hivi *traffic* kwenye makusanyo, wako upande upi? Kwa sababu *traffic speed* walijonayo wanawazidi hata *TRA*. Hizi tochi ziliuka kwa lengo la kupunguza ajali au kuongeza mapato, watuambie! Kwa sababu tangu tochi zimekuja, nashangaa unawasikia ma-*RTO* wanaeleza tumekusanya kiasi hiki, si kutuambia ajali zimepungua kwa kiasi hiki, wanatuambia tumekusanya kiasi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi lengo la tochi watuambie kumbe siyo kupunguza ajali ni kukusanya! Labda ni *indirect way* ya kukusanya, atueleze Mheshimiwa Waziri. Maana inafika mahali sasa *Traffic* wanapanda juu ya miti, wanatokea porini, ni *fine*. Imefika mahali madereva wanasema; ah, mimi sasa nalazimika ninunue tochi. Maana ya kununua tochi ni nini? Unaweka pesa mfukoni, kila unapokutana nao Sh.30,000/= unatoa unaendelea. (*Makofii*)

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Devotha Minja. Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni na baadaye Mheshimiwa Amina Mollel, ajiandae.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo, lakini pia niendelee kushukuru kwamba nimepata fursa ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Serikali yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la kwanza na kila mwaka naendelea kushauri hivyo; tubadilisheni mfumo wa bajeti yetu, badala ya kupanga matumizi kwanza, tukusanye kwanza halafu ndio tupange matumizi, ndio tutakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ndani ya Bunge tubadilishe mfumo wa *Budget Cycle* yetu. Badala ya kipindi hiki ambacho tunakuja kukaa, hakuna tunachoweza kubadilisha, tungekuwa tunakaa kwanza tunakubaliana kwamba haya yapitishwe, haya yapande, halafu ndio tukija huku inakuwa ni kupidisha tu, mambo yote tunakuwa tumewekana sawa. Hapo ndio tutakuwa na mafanikio. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba mwaka huu hawakupandisha kodi katika maeneo mengi, isipokuwa zile ambazo zinatoka nje ya nchi ili kulinda viwanda vya ndani. Kwenye *excise duty* hawajapandisha kabisa, lakini lengo ni kuhakikisha kwamba tunakusanya mapato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri kwamba wangewekeza zaidi kwenye maeneo ambapo watapata mapato yasiyo ya kikodi, hapo ndio uchumi wetu utakua. Fedha hizo tungewekeza kwenye maeneo ya miradi ambayo *returns* zake ziwe zinakuja kwa haraka, tutapata mapato. Hata kwenye ukusanyaji wa kodi, tusiwe tunapandisha viwango vya kodi au tozo badala yake tutanue wigo, watu wengi zaidi walipe kodi. Kila Mtanzania akilipa kodi, nina uhakika tutakusanya kodi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote naendelea kushauri hapa kwamba sekta isiyokuwa rasmi inaendelea kukua.

Zamani ilikuwa asilimia 50, sasa hivi iko asilimia 70. Iko siku tutafika asilimia 100 kutokana na ada, tozo, kodi, ushuru; yaani ni utitiri umejaa. Tumeambiwa wanaleta *blue print*, lini wataileta? Lini itafanya kazi? Ukiondoa kitu kimoja kwa mwaka mmoja, hujasaidia viwanda vyta ndani, wala hujasaidia uzalishaji wa ndani. Kazi ya kwanza ilitakiwa hizi kodi, ada na tozo mbalimbali wangezifanyia kazi wangeona uchumi wetu unakua na uzalishaji wa ndani (*local production*) ungekua haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyetu havikui, uzalishaji wetu hata huko kwingine haukui kutokana na hizi tozo, kodi, ada na ushuru mbalimbali, ni kubwa sana. Hiyo yote haihusiani na Wizara ya Fedha tu, Wizara zote kila moja ambayo inahusika ilitakiwa wakae pamoja waziondoe. Hii *blue print* bado wanachelewa sana kuileta, tusitegemee tutakuwa na maajabu kwenye viwanda. Viwanda vyetu haviwezi kukua hata siku moja haya yasipobadilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kabla ya hizo Kanuni zote ambazo Mawaziri wamepewa mamlaka, ikiwezekana Bunge tubadilishe sheria au sijui nimefikiri vibaya, ila ilitakiwa Kanuni zije hapa kabla hazijaruhusiwa kwenda kuwa *printed* kwenye *Government Gazette* ili kabla Waziri ye yote hajapandisha tozo yoyote, sisi Wabunge tuwe tunajua kwamba hii sasa inaenda kupitishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii hapa wamekaa kimya wote kwa sababu hata bajeti hii ikiwa ndogo, kwenye tozo kule kwenye Kanuni anaenda kupandisha anavyotaka. Hiyo ndiyo inafanya ukuaji wa uchumi wetu udumae kabisa; badala ya kwenda *positive* inarudi inakuwa *negative*. Kwa hiyo, naomba hizo Kanuni sisi kama Wabunge wote tuziangalie upya, kabla ya kufika kwenye *Finance Bill*, kama kuna marekebisho tufanye hayo marekebisho kwa sababu tutaendelea kumlaumu Waziri wa Fedha, nyingine haziko kwake, ziko kwa Mawaziri wengine wote na kila mmoja anang'ang'ania tozo zake au ada zake asiziteremshe. Kila akiamka kila akipenda anapandisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hiyo ndiyo itafanya uchumi wetu ukue kama hizo kanuni zote zitakuwa zinapitia Bungeni. Nihavyojua, sheria inasema jambo lolote ambalo inahusu kupandisha kodi yoyote au tozo yoyote, lazima lipitie Bungeni. Sasa sijui lini imebadilika? Sasa naomba hilo lifanyiwe kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwamba wamekuwa na *tax amnesty*. Nampongeza sana kwa hilo, watu wengi wataenda kulipa. Ila naomba tunge-*extends* iwi tu kwenye *tax administration* kwa upande wa kodi ambazo wanakusanya kama *TRA*, wangeweka kwa upana wote, yaani kwenye *Regulatory Boards* zote, watu wanadaiwa vitu vya ajabu ajabu. Watu wanaamka kule wanadai vitu vya miaka 10 nyuma. Wangeweka kwamba zote wangezisamehe kwa muda wa miezi sita tuanze moja. Nina uhakika tutakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, hapa tulikubaliana kwamba *Local Government Development Grant* ambayo Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania wote ndiyo tunaitegemea huko kwenye Halmashauri zetu. Tumekubaliana hapa watatoa fedha za Elimu na Afya kutokana na ile miradi tulyopanga; lakini nimepitia *Volume IV*, sioni mahali imetajwa kabisa *Local Government Development Grant*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya *reallocation* mwezi wa Saba, Nane na wa Tisa hizi pesa hazitakuja, tutaumia. Lazima wote tukubaliane kwamba hapa ifanywe *reallocation* na tuone kwenye hii bajeti kwamba *Local Government Development Grant* iwepo na hizo fedha ziendelee kuja. Hizo ndiyo zinatusaidia huko kwenye kujenga Zahanati, Vituo vya Afya, kujenga na shule. Tusipofanya hivyo, tutaumia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauripia kwenye utafiti, tufanye *reallocation* tuhakikishe kwamba kunakuwa na pesa kwenye utafiti. Hatuna! Pesa kwenye utafiti tunategemea wafadhili wa nje, tunaweka pesa kidogo sana. Mtu wa nje

akikuletea pesa, anapeleka mahali ambapo naye ana maslahi yake, hapeleki mahali ambapo sisi tunapahitaji. Kwa hiyo, kwenye utafiti tuwekeze. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunashukuru wameondoa kodi kwenye tauzo za akinamama, *animal feeds* na kwenye maziwa, lakini wameondoa VAT, yule mtu hawezi kudai *import taxes*. Naomba tukifika kwenye *Finance Bill* waje na *measures* kwamba tunafanyaje ili viwanda vyatya ndani viweze kupona bila wao kukusanya *import taxes* au kupata *refund*, itakuwa *importers* wanapata faida badala ya wazalishaji wa ndani. Hapa tutakuwa hatujasaidia wazalishaji wa ndani, tutakuwa tumewasaidia wale ambao wana-*import* ndani ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze kwamba wameweza kupunguza *income tax* kwa viwanda vipyta kwa Sekta ya Ngozi na Sekta ya Madawa. Naomba hata vite vyatya zamani wangewaruhusu wapate *20 percent*. Siyo kwenye hiyo tu, viwanda vyote vipyta, sekta zote wangewapa tu hiyo *tax incentive* ya *20 percent* kwa sababu ni ndogo, hakuna kiwanda ndani ya miaka mitano kitakuwa na faida kubwa. Kwa hiyo, hawatapoteza sehemu kubwa. Kwa hiyo, kama ni ndogo, itakuwa ni moja katika maeneo ambayo watapata *tax incentive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *ETS*. Namwomba Mheshimiwa Waziri, ndani ya hizi siku chache apate takwimu sahihi ya idadi ya chupa au idadi ya *units* ambazo tunazalisha nchini, halafu apige hesabu na hizo bei ambazo tulipewa kama bei elekezi ambayo wanategemea kupiga hizo *stamp*. Ni bora wangepandisha asilimia tano kwenye ushuru kutokana na *inflation* kuliko kwa hizo bei ambazo tumepewa. Lengo hapa ni kuhakikisha kwamba wale wote ambao hawaoneshi *records* zao vizuri au wana-*under declare* tuweze kuwapata. Ila lengo siyo kwamba hao tuwakomeshe na kupandisha gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la *ETS* tumeifanyia kazi vizuri, naye ana uwezo wa kupata *units*

ngapi tunazalisha kwa mwezi na kwa mwaka halafu kutokana na hiyo, sisi tulivyopiga hesabu, *stamp* haitakiwi kuzidi shilingi moja au shilingi mbili. Kwa hesabu zetu, tunazalisha zaidi ya *units* bilioni tano kwa mwezi. Ukipiga kwa miezi 12 ni bilioni 60 mara shilingi mbili ni *120 billion*, inatosha hiyo kurudisha uwekezaji wake pamoja na kupata faida. Kwa hiyo, kwenye *stamp* hii kwenda shilingi kumi na tatu, ni bora angepandisha asilimia tano kwenye *inflation* kuliko hizo *rates*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye pombe kali. Bado huko kuna udanganyifu mkubwa unafanyika kwenye suala la uzalishaji na ndiyo maana kuna watu wanaweza kuuza bei ya chini kuliko gharama za uzalishaji kwa sababu kuna upotoshaji. Hapo sisi tunaamini kuna zaidi ya shilingi bilioni 400 au 500 zinazopotea. Ni eneo ambalo nashauri walifanyie kazi na wataweza kupata kodi nyingi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naendelea kusisitiza Sh.50/= kwa kila lita ya mafuta yanayoingia nchini, hiyo ndiyo itakuwa ukombozi wetu. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote safari hii tuifanyie marekebisho sheria na tuombe hiyo Sh.50/=, ndiyo mahali ambapo tumeona kuna mafanikio kwa ile Sh.50/= tuliyoiweka mara ya kwanza na *REA* imefanikiwa kutokana na hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Muda wako umemalizika Mheshimiwa Jitu? Ahsante.

Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Mollel na baadaye Mheshimiwa Allan Kiula na Mheshimiwa Vedastus Mathayo, wajiandae.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi nichangie bajeti ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya na nampongeza Mheshimiwa Rais na Waziri mwenye dhamana. Vilevile nampongeza sana Spika wa Bunge pamoja na Katibu wa Bunge Bwana Kagaigai, kwa sababu wamekuwa ni mfano wa kuigwa kwa kuzingatia haki za msingi na kufuata Sheria za Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mwaka 2006 juu ya haki za watu wenye ulemavu. Nampongeza sana Mheshimiwa Spika na Katibu wa Bunge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu, katika suala zima la elimu bure kwa watu wenye ulemavu limekuwa na faida kubwa sana. Nasema hivyo kwa sababu siku za nyuma katika suala zima la elimu katika jamii zetu, hasa wazazi walikuwa wanaangalia kwamba kipaumbele apewe nani. Kipaumbele hiki apewe mtu mwenye ulemavu. Kwa hiyo, kama kuna watoto wawili katika familia, mzazi yuko tayari kumpeleka mtoto asiyé na ulemavu na mtoto mwenye ulemavu anaachwa nyumbani na wengi wao walikuwa wanafichwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba haki ya kupata elimu ni ya msingi na ni haki pia kwa watu wenye ulemavu. Katika Bajeti ya Serikali Mheshimiwa Waziri sijaona, bado sijaridhika hasa katika kundi hili la watu wenye ulemavu kuzungumzia ni kwa jinsi gani. Kwa maana hiyo naomba tu Serikali na Mheshimiwa Rais, kwa sababu pamoja na kwamba jitihada nzuri na kazi nzuri imefanyika katika kuhakikisha kwamba elimu ni bure mpaka kidato cha nne, lakini bado naomba elimu kwa watu wenye ulemavu iwe ni bure kuanzia elimu ya msingi mpaka elimu ya chuo cha Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani nasema hivyo? Kama nilivyosema hapo awali, mtu mwenye ulemavu tegemeo lake kubwa liko katika elimu, hana namna nyingine yoyote ambayo inaweza kumwezesha huyu mtu akaweza

kujitegemea mbali ya elimu. Kwa sababu ukimpa elimu umemkombo na elimu hii ndiyo itakayomsaidia aweze kupata ajira. Vile vile bila ajira kwa mtu mwenye ulemavu na hasa hata wale ambao wamesoma, asipopata ajira bado inakuwa ni shida. Kwa hiyo, ile elimu aliyopata itamsaidia aweze kuona ni kwa jinsi gani anaweza akajajiri kwa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali kuhakikisha kwamba inatoa elimu bure kwa watu wenye ulemavu kuanzia elimu ya msingi, sekondari na vilevile elimu ya chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mzuri tu, nawaombea mapumziko mema mapacha wawili ambao walifariki hivi karibuni, Maria na Consolata. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika suala zima la mkopo, aliwapa watoto hawa ruzuku ambayo siyo mkopo, kwa sababu alliona umuhimu wa watoto hawa kwa jitihada zao mpaka wakafika elimu ya chuo cha kikuu. Kwa hiyo, akaona ni namna bora kabisa kuhakikisha kwamba anawapa ruzuku ili waweze kusoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtu mwenye ulemavu mpaka anapofika chuo kikuu au anapobahatika kumaliza elimu ya sekondari akaenda kidato cha nne, cha tano na cha sita na baadaye kwenda chuo kikuu ni sawa na usemi wa Kiswahili unaosema: "Ukimwona nyani mzee, ujue amekwepa mishale mingi." Kwa hiyo, changamoto wanayopata watoto wenye ulemavu na watu wenye ulemavu ni kubwa na ni mara mbili ya wenzetu wasio na ulemavu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali kuona umuhimu wa kuwapa elimu bure watu wenye ulemavu kuanzia elimu ya awali mpaka chuo kikuu. Siyo hayo tu, tuone ni kwa jinsi gani tunawawezesha kwa kupata vifaa. Nafurahi sana Waziri mwenye dhamana ni mama, wanasema: "Uchungu wa mwana aujuae mzazi." Tuone sasa ni kwa jinsi gani tunawawezesha vifaa vipatikane katika shule zote. Pia hawa Walimu ambao wanasona katika Vyuo,

tuone ni kwa jinsi gani tutawawezesha wapate vifaa vyatua kuwasaidia pia katika kufundishia ili basi tutatue zile changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba sana na namwombaa sana Mheshimiwa Rais aone ni kwa jinsi gani atalikomboa hili kundi la watu wenyewe ulemavu. Natambua jitihada zake, tumeona ni kwa jinsi gani katika Wizara mbalimbali wapo watu wenyewe ulemavu na hawajamwangusha. Hata katika Bunge lako, katika Baraza tumeona Mheshimiwa Ikupa anavyofanya kazi vizuri na hii imetuonesha kwamba watu wenyewe ulemavu ukiwapa nafasi wanaweza. Sasa usipowapa elimu itakuwa ni sawa na kutwanga maji kwenye kinu. Naomba sana katika hilo ili basi tuweze kuwasaidia watu wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ukurasa wa 15 wa Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza kuwa asilimia 10.4 ya Watanzania hawana ajira na vijana 800,000 wanaohitimu Elimu ya Chuo Kikuu ni vijana 40,000 tu wanaopata ajira. Kwa miaka mitatu ina maana kwamba tutazalisha watu 2,280 wasio na ajira. Kwa sababu kati ya hao 40,000 ukiondoa katika hiyo 800,000 wanabaki watu 760,000. Kwa hiyo, utaona ni kwa jinsi gani tatizo la ajira lilitayo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri aliendelea kwa kusema kwamba Sekta ya Kilimo ambayo ni tegemeo, inaajiri asilimia 66 ya Watanzania. Pamoja na kwamba kuajiri asilimia hiyo bado inachangia pato lake kwa wastani wa asilimia 30, lakini pato hili linakua kwa kasi ndogo sana ya 3% mpaka 7%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongezo sana Mheshimiwa Rais kwa sababu hivi karibuni tumeona jitihada zake, ambapo amezindua mpango mkakati wa kilimo. Katika suala hili sasa tuone ni kwa jinsi gani kilimo chetu tunakifanya kuwa cha kisasa. Nchi ya Misri ambayo inategemea maji kutoka Mto Nile, wamewenza kwa kiasi kikubwa sana kufanikiwa katika suala zima la kilimo. Siyo

hao tu, ukienda nchi ya Israel mapinduzi ya kilimo ni makubwa sana na hata Mheshimiwa Mama Mbene siku akichangia bajeti hii alielezea pia nchi ya Vietnam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa nchini Tanzania mvua ni shida na hii ni kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, je, tunajipangaje kuhakikisha kwamba kilimo chetu, mbali ya kuajiri asilimia hiyo 66, lakini vijana hawa 800,000 ambao wanahitimu vyuo vikuu, tuone kwamba wale wanaobaki ni kwa jinsi gani wanawenza kujajiri katika suala zima la kilimo. Vile vile katika kilimo tuone kuna mpango mkakati gani wa kuwawezesha vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tumeona kwamba vijana wengi wameingia katika kilimo cha kisasa ambacho ni kilimo cha kibashara kwa kulima hasa kwa kutumia hizi *green house*. Je, Serikali sasa inawawezesha vipi hawa vijana na hasa ukizingatia kwamba nchi ya Tanzania tuna maeneo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya maeneo makubwa tunawawezesha vipi vijana ili waweze kujajiri wao kwa kulima kilimo chenyetija ambacho kitaweza kuwasaidia wao na familia zao? Hili ni jukumu ambalo Serikali inapaswa kuhakikisha kwamba inajipanga na itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la ajira. Kwa sababu vijana tukianza kuwawezesha na kuwafundisha tangu chuo kikuu; na tumeshaona kwamba sasa hivi Mheshimiwa Rais ana dhamira ya dhati kabisa kuwakomboa vijana na hasa katika mapinduzi haya ya kilimo, sasa basi twende kuwawezesha vijana waingie katika hicho kilimo cha biashara ambacho kitawasaidia kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona baadhi ya vijana ambao wamefanya vizuri na wanasafirisha bidhaa za shambani ambazo wanalima mpaka nje ya nchi. Mmoja wa vijana hao ni Khadija Jabir ambaye amekuwa ni mfano wa kuigwa. Sasa tunawaandaaje vijana wengine, tuwapate kama akina Khadija Jabir ili nao waweze kujilingiza katika

mapinduzi haya ya kilimo? Kwa sababu pia tunakwenda katika viwanda rasilimali nyingine hasa malighafi nyingine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Malizia Mheshimiwa.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu bado. Ni kengele ya kwanza.

MWENYEKITI: Kengele ya pili tayari. Malizia kidogo.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimalizie kwa kusema kwamba napongeza pia kwa kuona umuhimu wa kufuta kodi katika baadhi ya vifaa ambavyo vinachanganya katika vyakula vya kuku. Kuku hivi sasa ni tegemeo kubwa sana la wajasiriamali. Kwa hiyo, kwa kuondoa kodi hizi zitawasaidia sana wanawake ambao ndiyo wajasiriamali wakubwa na jamii yote kwa ujumla ili waweze kuwekeza katika ujasiriamali wa kufuga kuku. Siyo hilo tu, hili pia litawasaidia waweze kuendeleza na kuwasomesha watoto wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushuru sana na naunga hoja mkono. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Allan Kiula, baadaye Mheshimiwa Vedastus Mathayo na Mheshimiwa John Heche waijandae.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuweza kunipatia nafasi jioni ya leo nami niweze kuchangia kidogo. Ninayo maneno machache sana ya kusema, lakini ni muhimu yakasemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayofanya na Msaidizi wake Naibu Waziri, wanafanya kazi kubwa sana. Unajua suala la uchumi ni suala mtambuka na ni suala ambalo

linahitaji umahiri wa hali ya juu. Kwa hiyo, ukisoma kitabu kimoja kimoja unaweza usipate mwelekezo vizuri, ndiyo maana inabidi usome nyaraka zote halafu ujue tunaelekea wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi kwenye suala zima la ukusanyaji wa mapato. Jambo la kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kutoa *tax amnesty* kwa watu ambao wanadaiwa kodi, kwa kuondoa *interest* na *penalty* zote zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposoma kwenye kitabu nikagundua kwamba kutakuwa na tatizo moja, wamesema kwamba ndani ya miezi sita hiyo *amnesty* ndiyo itaweza kutolewa. Ila nafikiri kwenye miezi sita, kutakuwa na mazungumzo (*negotiation*), kwa sababu wale wanaotaka kupata huo msamaha inabidi waende kwenye Ofisi za *TRA* wakazungumze nao, wakubaliane na watakuja kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pesa kiasi cha shilingi bilioni 500 nafikiri inatarajiwa kukusanya ndani ya mwaka mzima. Kwa sababu, kama mtu atakuja mwezi wa Nane wakazungumza naye na hawesi kulipa *in lumpsum*, atalipa kidogo kidogo, ina maana lazima atakwenda mpaka Januari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni muhimu kwa sababu baada ya miezi sita mamlaka husika itakapokwenda kwenye Kamati itakuja kuonekana kwamba hizi pesa hazijakusanya, kumbe ni suala la *administration*. Kwa hiyo, suala hilo ni muhimu likaangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la *Revenue Forecasting*. Nimeangalia hii *schedule* jinsi mapato yatakavyopatikana, *Tax Revenue* na *Non Tax Revenue*, lakini nikawa najiuliza swali moja. Mwaka 2015/2016 nafikiri *TRA* ndiyo walifilia ile *target* iliyo kuwa imewekwa. Unaposema *target*, maana yake inakwenda *in line* na *projected plan* ambayo inakuwa imeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zile *data* za kufanya hizo *revenue forecasting* zikiwa haziko sahihi sana kwa maana ya *sector wise* ndizo zina-*lead* kwenye kufanya ile *revunue forecasting* ileté majibu ambayo siyo sahihi. Kwa hiyo, jambo hilo inabidi liangaliwe ili tuwe tunawapa malengo sahihi hasa wenzetu wa *TRA* kwamba waweze kukusanya kulingana na uchumi unavyoruhusu, kwamba uchumi unaruhusu kodi kiasi gani iweze kukusanya? Kwa hiyo, ni jambo muhimu sana hilo likaangaliwa na wataalam wetu wakaweba kulifanyia kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala la mawasiliano (*telecommunication*). Ukiangalia nchi za jirani, Sekta ya Mawasiliano ina mchango mkubwa sana wa kodi. Sasa hapa kwetu Tanzania sijui kuna tatizo gani kwa sababu bado mchango katika Sekta ya Kodi haujawa wa kutosheleza kwa maoni yangu. Kwa hiyo, nafikiri uko umuhimu wa kufanya utafiti wa kutosha kuona mapato yanavuja wapi, au kwa nini Sekta ya Mawasiliano hajatoa mchango wa kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hesabu ya haraka tu, ukiangalia idadi ya Watanzania walioko na wanaotumia simu; sasa mapato yanayopatikana watu hawatumii simu? Watu wanatumia simu, lakini nafikiri kuna namna ambayo inafanyika ambayo siyo sahihi aidha kwenye kutengeneza hesabu zao, zile *expenses* zinakuwa nyingi mpaka huko kwenye *profit* kunaathiri kwenye *profit*, lakini pia ku-*capture data* kwa ukamilifu wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *EFD*, bajeti imesema kwamba watalipa 0%. Nikawa najuliza swali, sasa hivi kuna *suppliers* ambao wana *stock*. Ile *stock* wanaifanya nini? Kwa sababu *stock* ilikuwa imelipiwa kodi. Sasa wanafanya nini ili kuweza ku-*mitigate* au kuweza kufanya kwamba kuwe na *fair play* kwamba, hawa watakaoingiza zero na hawa ambao walishaleta tunafanya jambo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, hatua kubwa imechukuliwa na *TRA* na Wizara kwa ujumla

kuhakikisha watu wanatumia mashine za *EFD* na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amelisemea sana hili suala. Tumekwenda kwenye hii *informal sector*. Nashauri kama itawezekana, zitafutwe *EFD*, halafu itafutwe *sample group* ambapo watu watapewa *EFD* bure kwenye *informal sector* waweze kutumia hizo *EFD* na tuone *impact* yake itakuwa ni nini? Itakuwa kama ni motisha kuweza kuwafanya watu waone umuhimu wa kutumia *EFD*, lakini pia watajifunza kufanya mahesabu ya kuweka na kutoa (*simple book keeping*), litakuwa ni jambo zuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia suala la kodi zilizo kwenye malimbikizo (*tax objection*) na lenyewe ni suala muhimu sana ambalo Wizara na *TRA* kwa ujumla wanatakiwa wasimamie waone kwamba zile *tax objection* zinakuwa cleared. Kwa kutumia *window* hii ya *tax amnesty* inaweza pia ikasaidia kupunguza zile *objections*. Kwa hiyo, lazima kuwe na *massive campaign* ya kuweza kuwaelewesha watu wakajua hili jambo kwa sababu, watakuwa wanarudi nyuma, wanajificha kwa sababu, hawajui faida yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nilibahatika kufika *SAS, South Africa* kule, waliwahi kutoa *tax amnesty* na watu walilipa na walikuwa treated fairly na ilikuwa ni siri yao na kodi ilipatikana. Kwa hiyo, ni jambo muhimu sana kuwe na *massive campaign* na iwekwe bajeti ya kutosha kwa sababu ndiyo uwekezaji wenyewe. Kwa hiyo, tusibanie pesa mahali tunakoweza kupata pesa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye lile la *non tax revenue* tumeona *BoT* walitoa gawio, *NBC* na *CRDB*. Ninachotaka kusema hapa, mashirika yanayosimamiwa na *TR* sasa imefikia wakati mchango wake uweze kuonekana. Kama mchango wa mashirika hayo ukiweza kuonekana, ndipo tutarudi hata huku kuweza kufikiria kwamba tupunguze baadhi ya viwango vya kodi au tuondoe kodi ambazo ni kero. Natambua kwamba ukisoma bajeti iko very tight kwa sababu vyanzo ni vilevile na lazima uwe na *normal flow*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukipunguza *Pay As You Earn* utaleta madhara makubwa sana kwenye *revenue collection*. Jambo hilo naliyahamu na ni muhimu tukalifahamu wote tuangalie huku kwa *TR* anatuletea nini? Pamoja na hivyo, *TR* naye awekeze zaidi sasa. Kwa sababu, pamoja na mashirika yaliyopo, lakini lazima tuongeze uwekezaji kule ili tuweze kupata pesa za kuweza ku-*finance* bajeti yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nampongeza Mheshimiwa Waziri. Mimi natoka Singida tunalima sana zao la alizeti. Dodoma wanalima alizeti; kwa ku-*protect* viwanda vya ndani kwa kupandisha kodi, mafuta yatokayo nje ina maana uzalishaji wa ndani utaongezeka. Tatizo kubwa lilopo ukienda hapo Kibaigwa, ukaenda mbele kidogo, ukarudi Singida ukaenda Shelui, utakuta mafuta mengi yako barabarani. Sasa tunafanya utaratibu upi wa kuweza kuwasaidia hao wakulima kwanza kulima wapate mbegu bora, lakini pia kuweza kuyakusanya hayo mafuta yawe katika kiwango kinachokubalika na yaingie kwenye masoko rasmi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, watu hawa wanategemea masoko ya watu wanaopita barabarani na wakati mwagine uratibu wake sasa hata kodi hawalipi pia, lakini tukiweza kutengeneza *centres* katika maeneo hayo; na ndio hao wafanyabiashara wadogo wadogo ambao tunawazungumza, wajasiriamali, nafikiri mafuta yale ni mengi sana na hata tunaweza tukaya-*count*. Nina hakika kabisa hatujui kiasi gani cha mafuta kinachozaishwa na wazalishaji wadogo wadogo. Kwa hiyo, jambo hilo ni muhimu likaangaliwa kwa kushirkiana na Wizara ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yote yakifanyika kwa ukamilifu wake, nina imani kwamba ile 32 *trillion* ambayo tunatarajia kuweza kuipata *this year*, itaweza kupatikana. Pia, mamlaka zinazohusika, wafanyakazi wa *TRA* basi wafanye kazi kwa juhudu na weledi mkubwa. Tunajua wanafanya kazi kubwa, lakini basi wahakikishe kwamba pesa au kodi inayostahili kukusanya inapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda kusema haya maneno machache, nafikiri yatakuwa yamemsaidia Mheshimiwa Waziri. Nashukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Allan Kiula. Tunaendelea na Mheshimiwa Vedastus Mathayo, baadaye Mheshimiwa John Heche na Mheshimiwa Zaynabu Vulu, ajiandae.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hii hotuba ya Waziri wa Mipango na Fedha. Kwanza, nashukuru kwa hotuba nzuri ambayo hasa ukiangalia imelenga kuwasaidia sana watu wa chini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mambo mawili ya muhimu ambayo ndiyo kama maneno yangu ya utangulizi. Moja, natambua kwamba Serikali hii ni Serikali ya wanyonge, ni Serikali ambayo ingependa kuendelea kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini, wala hilo halina ubishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuulize tu Mheshimiwa Waziri wa Mipango; swali la kwanza ni suala la watumishi waliokuwa wa kiwanda cha *MUTEX*. Hao watumishi toka waachishwe kazi ni zaidi ya miaka 20. Toka walipoachishwa kazi wamekuwa na madai yao ya kimsingi. Vile vile hawa watumishi wametoka katika mikoa mbalimbali. Wote mnafahamu kwamba fedha hizo zilitengwa, lakini hawajalipwa hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikilisema hili hata nakumbuka mwaka huu mwanzoni Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Musoma. Alipokuja, wananchi wa Musoma walimpokea kwa mabango, akaahidi kwamba atahakikisha wamepata mafao yao. Mheshimiwa Waziri anafahamu, Mheshimiwa Naibu Waziri nimekwenda kwake mara nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii Serikali ya wanyonge inashindwa nini kumaliza tatizo dogo hili la watumishi ambao walitumikia Serikali hii kwa uwezo wao wote katika kipindi chao kikubwa, lakini mpaka leo wanataabika wanatolewa kwenye nyumba hata walizokuwa wanaishi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati wa uhitimishaji kusema kweli, hili lazima Mheshimiwa Waziri alitolee maelezo ya kina ambayo wale wananchi labda yanaweza yakawatia moyo, ambayo yataonesha hizo fedha zao kama safari hii wanaweza kuzipata ili waendelee na maisha yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swalii lingine ni suala la kuwaondoa kazini watumishi hewa. Hakuna mwenye tatizo na hilo, lakini namna ya watumishi wengine jinsi walivyoondolewa. Ukiangalia katika Majimbo yetu mbalimbali, wako baadhi ya watumishi ambao waliondolewa tu kwa sababu ya upotoshwaji. Mfano, kuna mtu ambaye alisoma darasa la saba, baada ya hapo akaajiriwa, akaendelea kujiedeleza, akapata *Certificate*, akapata *Diploma*, mwengine mpaka akapata *Degree*. Wakati ule wanajaza zile taarifa zao binafsi, alipofika kwa Afisa Utumishi pale akaambiwa wewe sasa elimu yako siyo ya darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu, elimu yako siyo ya darasa la saba andika kwamba una elimu ya kidato cha nne. Leo huyo tumemwondoa kazini, tumeacha mtu wa darasa la saba. Hivi kweli ukiangalia tu katika ule utendaji wa kawaida, umemwacha wa darasa la saba halafu umetoa mtu ambaye ni *graduate*. Hao leo wanahangaika mtaani, hawana pa kwenda, wala hawajui wafanye nini, wala hawajui hatima ya maisha yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani hii Serikali yetu ambayo ni Serikali sikuvi, hebu itoe majibu sahihi na ione namna gani ya kuwasaidia hawa watu ambao wengi wao walipotoshwa. Badala ya kusema kwamba amemaliza

darasa la saba akaambiwa kwamba kwa sababu amejiendeleza, basi elimu yake ni zaidi ya darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda na watu wengi kusema kweli tunalizungumzia ni kwamba nchi yetu kama ambavyo amesema Mheshimiwa Waziri, uchumi wetu umekua. Tukija kwenye hali halisi katika kuangalia wananchi wa chini, wale wananchi wa kawaida katika maisha yetu ya kawaida, huo uchumi hatuuoni. Hiyo nami nakubaliana kwamba inawezekana uchumi wetu umekua katika zile sekta ambazo haziojiri watu wengi. Sasa kwa sababu hiyo, ndiyo maana kila mara tukiangalia hali ni ngumu. Sasa kwa sababu, sisi Wabunge jukumu letu ni ushauri, nami napenda nimshauri Mheshimiwa Waziri Mpango, kama ataona ushauri unafaa, basi waweze kuufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, sifahamu ni kwa nini Watanzania wengi hatupendi kulizungumza hili. Kusema kweli suala la uzazi wa mpango ni suala ambalo halikwepeki kama tunahitaji kukuza uchumi wetu. Kwa sababu, ukiangalia fedha nyingi sasa pamoja na kuzipeleka kwenye huduma za jamii, lakini inaonekana kule nako hatujafanya kitu. Mfano, ukiangalia kwenye afya peke yake zimetoka shillingi billioni thelathini na kitu, leo tunazungumzia shillingi billioni mia mbili na kitu, lakini ukienda kule hospitali, bado dawa hazitoshi, bado huduma za afya hazitoshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye shule, mfano kwenye shule moja, katika Kata yangu moja, darasa la kwanza peke yake wanaandikishwa watoto wasiopungua 800. Kwa hiyo, ni kwamba hata kama tutaongeza bajeti, bado maisha yataendelea kuwa magumu kwa sababu fedha nyingi tunaendelea kuzimalizia kwenye huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni ushauri wangu kwamba hebu tuone namna ya kuli-*address*. Maana katika nchi nyingine, asilimia kubwa ya watu ni wale wenye *manpower* ya kufanya kazi, lakini katika Tanzania asilimia 60 wote ni watu ambao ni tegemezi. Kwa hiyo, tunadhani

kwamba bila kuli-*address* hili litaendelea kutupa tabu na kila siku fedha zitaonekana hazitoshi na uchumi wa nchi bado utaendelea kuwa ambao siyo mzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni ushauri, wote tunakubaliana kwamba siyo chini ya 60% ya Watanzania ni wakulima. Kama hivyo ndivyo, nini kifanyike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie yale mazao ambayo kwanza masoko yake yanapatikana. Nami nije na mfano wa zao moja tu la mpunga. Zao hili ukiangalia katika nchi zote zinazotuzunguka, ukienda Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Kongo na Zambia ni watu ambao wanahitaji mchele. Kwenye suala la kilimo cha mpunga kinahitaji maji, mbolea na hakina majira. Sasa kumbe kitu ambacho tungeweza kufanya, tungeweza ku-*identify*katika mabonde tullyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungewapeleka huko *JKT* wakawapeleka vijana huko, wale vijana wakafanya kazi, watavuna ule mpunga. Kwa hiyo, tungakuwa na masoko ya uhakika ambayo tunadhani kwamba wale vijana watakuwa wamejipatia ajira na ni kwamba maisha yao yataboreka kuliko hivi ambavyo tunaendelea kuhangai na bado maisha yetu au maisha ya watu wetu yanaendelea kuwa magumu. Kwa hiyo, kama tutaona ni jambo jema, basi na lenyewe tukilichukua ni imani yangu kwamba litatusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo naona kama bado hatujipanga vizuri sana ni elimu. Leo ukiangalia kwenye upande wa elimu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nimalizie tu kwa kusema kwamba, naomba mwisho Serikali ione uwezekano wa kulipa wale Wazabuni wote ambao wamei-*supply* Serikali,

wametusaidia, lakini mpaka leo wale watu wanadai na hawajawahi kulipwa. Kwa hiyo, Serikali iweze kuwalipa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus. Tunaendelea na Mheshimiwa John Heche, baadaye Mheshimiwa Zainab Mndolwa na Mheshimiwa Maftaha Nachuma, wajandae.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nami kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti yetu hii ya mwaka huu. Nianze na jambo la kwanza la ugatuaji wa madaraka, yaani *D by D* na Halmashauri. Niliwahi kuwa Diwani, kwa hiyo, nazungumza kitu ninachokifahamu na umuhimu wa Halmashauri hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwe kwenye *record* kabisa kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango atakuwa Waziri wa kwanza na Serikali hii kuua Halmashauri za nchi hii. Nchi hii ina viji 18,000. Jimbo langu peke yake lina vitongoji 500. Hawa watu mwaka 2017 walianza na waraka wa kuzuia Madiwani kuwachukulia Watumishi wa Halmashauri hatua. Ilikuwa namba moja kuua Halmashauri zetu. Wakaja na kuondoa pesa zote kutoka Halmashauri kupeleka Hazina *then Benki Kuu*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wakaja kuchukua vyanzo vyote vya Halmashauri ikiwemo mabango na *property tax* wakapeleka kwenye ukusanyaji wake. Wakaja na mfumo wa kuondoa ripoti za Halmashauri kutoka *quarterly* kwenda kwenye nusu mwaka na sasa kwenye kitabu chake hiki anaanzisha Akaunti ya Pamoja, kwamba pesa zote ziwe zinakusanya zinawekwa kwenye akaunti. Tarime tukitaka kufanya matumizi asubuhi, tunampigia simu Mheshimiwa Dkt. Mpango ndiyo atuletee tuzibe tundu la choo lililobomoka kwenye Kijiji ha Kemakorere, kwenye Kitongoji cha Nyangasare; viji 18,000. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Sera ya Afya ya nchi hii ilivyo, tukiwa na zahanati kwenye kila kijiji, tuna zahanati 18,000. Tukienda na shule, tuna shule 18,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye Kata tuna Kata zaidi ya 7,000. Tukiwa na Kituo cha Afya kila Kata, tuna Vituo vya Afya 7,000. *Bulb* ikiharibika kwenye nyumba ya mtumishi wa zahanati ya kitongoji fulani, tuombe pesa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango, Dar es Salaam. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanataka ku-centralize waongoze nchi hii kutoka Dodoma, hii siyo Rwanda na hawataweza.

MBUNGE FULANI: Wala siyo Uganda.

MHE. JOHN W. HECHE: Wala siyo Uganda hii.

MBUNGE FULANI: Au Namibia.

MHE. JOHN W. HECHE: La kwanza hilo. Kwa sababu, wame-copy kutoka Rwanda, kutoka Namibia na kutoka Uganda. Rwanda ni mkoa kama Mkoa wa Mara. Tarime peke yake nimesema tuna vijiji 88. Hii nchi ina vijiji 18,000; Mheshimiwa Waziri atakaa hapo awe anapigisha simu kwamba tundu la choo limeharibika kijiji fulani anapeleka pesa, anaweza hilo? Wasitake kuua nchi hii. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna kichaka Serikali hii imekuwa ikitumia kwa miaka yote kufanya ujisadi, ni kichaka cha umeme. Hapa kwenye ukurasa wa nane, katika kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango hiki, anasema, nampongeza Rais kwa ujenzi wa umeme wa *Megawatt* 2,100 sijui wa Bonde la Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujisadi mkubwa wa umeme *Richmond* ulikuwa ujisadi wa umeme wa CCM; *Tegeta Escrow* ujisadi wa umeme wa CCM; *Songas*, ujisadi wa umeme wa CCM; na mpaka leo nchi hii hajawahi kupata umeme wa

kudumu. Leo ukiwaauliza hata Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mawaziri wote hao, kulikuwa na kelele kubwa sana hapa kuhusu wizi wa *Tegeta Escrow*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge na Bunge lilikaa mpaka usiku wa manane hapa, likataja watu. Leo walioko gerezani, nami nataka Mheshimiwa Waziri aje anijibu; ni Harbinder Singh na Rugemalila peke yao. Je, hao ndio walioiba bilioni 309 za nchi hii? Nataka waje watujibu hapa. Kwa sababu anatengeneza ufisadi mwiningine wa kwenda kuiba pesa za Watanzania zaidi ya shilingi bilioni 10 kwenye *Stiegler Gorge*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimuulize Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango, hivi ni utaratibu wa kawaida, leo wanakwenda kwenye nishati wanaonesha kwamba wanahitaji shilingi bilioni 700 kwa ajili ya mradi ambao hatujui na Bunge hili halijui ukamilishwaji wake utakuwa wa shilingi ngapi? *Total amount* ya kukamilisha ule mradi ni kiasi gani ili tujue tunapoidhinisha shilingi bilioni 700 bado Bunge hili litadaiwa kiasi gani ili ule mradi ukamilike? Sasa wanataka kuanza kuleta shilingi bilioni 700, kesho shilingi bilioni 800, keshokutwa shilingi bilioni 900 *Tegeta Escrow, Escrow* nytingine na *Richmond* nytingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Gujarat India, juzi walisema linakwenda kuzalisha umeme wa *Megawatt* 5,000 kwa umeme wa Solar kwa gharama ya Dola bilioni 3.384 ambazo ni sawa na shilingi trilioni saba. Mimi, Mheshimiwa Kitandula na Waheshimiwa Wabunge wengine mwaka 2017 tulikwenda Marekani na hii *initiative* ya *Power Africa*, tumekuwa na Mheshimiwa Kitandula pale na Waheshimiwa Wabunge wa CCM walikuwepo; nchi hii ina *potential* ya umeme kutoka kwenye *Solar* na kwenye *wind*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *wind* peke yake ukichukua Makambako, Singida na Same, tuna uwezo wa kupata umeme *Megawatt* 24,000. *Solar* ambayo India wanatumia shilingi trilioni saba kupata *Megawatt* 5,000 sisi tunakwenda kutumbukiza shilingi trilioni 10 kwenye *Megawatt* 2,100

ambazo India wamepata zaidi *Megawatt* 2,900 zaidi kwa bei ya chini ya shilingi triliuni mbili. Huo umeme hautapatikana, wataua viumbi hai pale Selous, wataua pori la Selous na hawatakaa wapate huo umeme wa *Megawatt*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Dkt. Mpango aje atuambie hapa, dunia nzima kwenye viwanda wanatumia umeme wa *gas* na wanatumia *nuclear power*. Mheshimiwa Waziri viwanda vyake hivyo vya kutumia umeme wa maji ambao alikuwa na Bwawa la Kihansi, Hale na Mtera, hayakudumu hata miaka 30 ukajaa udongo mle na hayafanyi kazi. Atuambie hilo bwawa lao la *Stiegler's Gorge* la shilingi triliuni 10 za Watanzania *life span* yake ni miaka mingapi? Ili tuweze kulinganisha hizi shilingi triliuni 10 na *life span* ya hilo bwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anakuja hapa anatuambia *SGR*, hawawaambii Watanzania ukweli. Mapato yetu kwa mwaka mmekusanya *maximumly* wamepata shilingi triliuni 14.

MBUNGE FULANI: Hawajawahi kuvuka.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara ni shilingi triliuni saba, deni la nje shilingi triliuni tisa, wana nakisi ya shilingi triliuni mbili. Hizo pesa za *SGR* ambazo wanasema ni za kwao za ndani, ziko wapi kwenye hizi shilingi triliuni 14? Wawaambie watu ukweli, *SGR* wamejenga wapi hata mita moja? Watuneshe! Wanaenda wanaweka vizimba, wanazindua. Wale Wakandarasi wameshindwa kuwalipa hata petrol, wameondoka. Wawaambie Watanzania ukweli. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anakaa hapa anakuja anatudanganya hapa eti tunamsifia Mheshimiwa Rais kwa kujenga ukuta wa Mererani, hivi watu pale wanaiba kwa mikataba au wanaiba kwa kupora *Tanzanite* na kuondoka nayo? Wale wale ambao

tuliwalalamikia; wale wale walilalamikiwa na wachimbaji wadogo wa Mererani wamewarudisha mle mle ndani ya ukuta, yaani ni jambo la ajabu! (*Kicheko/Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamewapa nini? Watuambie Mheshimiwa Dkt. Mpango. Watuambie kwamba wanawadanganya Watanzania; leo anakuja hapa anatuambia apandishe bei ya bidhaa. Sisi kwa mfano, tunaishi mpakani, tuna *advantage* hiyo ya kuishi mpakani. Leo sukari kutoka Kenya Sh.1,200/= Tanzania pale Sirari. Sukari ya kutoka *Kagera Sugar* Sh.2,200/=, anataka mtu wa Tarime aumie kwa *expense* yako? Mfuko wa *cement* wa Bambuli Sh.4,000/=, mfuko wa *cement* wa Twiga Sh.22,000/=, hawataki Mtanzania wa Tarime anunue mfuko Kenya? Kama wanataka viwanda vyao vishindane, vilete *cement* kwa bei *competitive* na ya Kenya, Watanzania wenyewe wachague watanunua wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawawezi kuzuia Watanzania kupata vitu vya bei rahisi na vyenye ubora eti kwa *expense* ya viwanda vya Wahindi ambavyo siyo vya Serikali hii. Siyo vya kwao, wao hawana hata kiwanda cha nanii; ana viwanda cha tofali, cherehani tano, sijui viwanda vya maandazi, hivyo ndivyo wanavyoweza Serikali ya Awamu ya Tano. Hakuna viwanda vingine, hakuna. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Heche malizia, muda wako umemalizika.

MBUNGE FULANI: Bado muda, bado dakika tano.

MWENYEKITI: Umeridhika? Bado alikuwa anamalizia sentensi ya mwisho.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tafadhali.

MHE. JOHN W. HECHE: Mpe anipe taarifa.

MWENYEKITI: Muda wako umeisha.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Nakuomba kweli Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Sasa ananiambia; Mheshimiwa Heche, naomba ukae chini.

MHE. JOHN W. HECHE: Namtafuta sijamwona anayeniomba taarifa. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Sawa hata kama hujaniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashindwa kuvumilia kwa sababu...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Eng. Stella, acha tumalizie na Mheshimiwa Zainab Mndolwa na baadaye...

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kutoa taarifa kwa sababu, hatupo tayari kuona ukipotosha umma...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zainab Mndolwa na baadaye Mheshimiwa Maftaha.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, nami napenda kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunipa afya njema kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Fedha. Pili, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu...

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba mtulizane.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoo wa Dar es Salaam ni kitovu cha biashara katika nchi yetu na

wafanyabiashara wa Dar es Salaam wanachangia pato kubwa la Taifa, lakini wanakabiliwa na changamoto nyingi sana. Moja ya changamoto ni utitiri wa kodi. Ili mfanyakibashara aanzishe biashara, kuna *process* nyingi anapitia. Lazima apate leseni na hupewi leseni mpaka ukakadirive mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiutaratibu ingefaa zaidi mtu kabla ya kufanya biashara kwanza apewe muda maalum halafu baadaye ndiyo wanamkadiria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natolea mfano Dar es Salaam, ukienda pale Mnazi Mmoja Anatoglo, unataka leseni unaambiwa kwanza nenda *TRA* pale *Summit Tower Lumumba*. Ukipika Lumumba wanakuuliza eneo la biashara liko wapi? Unaambiwa liko Kariakoo. Wanakadiria biashara kulingana na eneo na wala siyo biashara unayoifanya. Hii ndiyo inayopelekea wafanyabiashara wengi kufunga maduka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaambiwa huko Kariakoo ni mkoaa wa kodi shilingi milioni tatu. Mtu anakadiria akiwa ofisini; hajui biashara unauzwa shilingi ngapi na hujaanza kuweka hata *display*. Ni tatizo kubwa sana kwa wafanyabiashara na hii ndiyo inawafanya wafanyabiasha wengi kufunga biashara zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *TRA* sasa hivi imepata mwanya; usipotoa risiti kutoptana na matatizo ya *EFD* sasa hivi, kitu cha Sh.5,000/= unaambiwa faini yake shilingi milioni tatu. Mwingine anashindwa sasa kulipa shilingi milioni tatu, mtu wa *TRA* anapata mwanya anakwambia sasa tuzungumze. Mnakosa mapato, mtu anapewa shilingi milioni moja yanaisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa Waziri katika kuliendea hili, najua binadamu siyo malaika, anafanya makosa na makosa mengine yanatokana na hizi mashine; na mashine zenyewe inaelekeea labda zina hitilafu. Wakati mwingine umetoea bidhaa unataka uandike risiti

unakuta mteja kaondoka, kumbe ameshawasiliana na *TRA* anakuja kukukamata anakwambia toa shilingi milioni tatu. Tuweke faini ambazo ni *reasonable* zinazolipika ili Serikali iweze kupata mapato yake kulikoni kuishia katika rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna kikosi cha Zimamoto sasa hivi kimetokea kule Dar es Salaam, kinataka kila *frame* ya duka iweke *Fire Extinguisher*. Najiuliza sana Mheshimiwa, mfanyabiashara anafungua duka 12.00 asubuhi, anafunga saa 11.00 jioni. *Short* ya meme ikitokea usiku wa manane *fire extinguisher* iko ndani ya duka lake, itamsaidia nini kuzima moto kama siyo biashara? Mfano tu, tutoe sisi Wabunge wote, watu wa Zimamoto waje waseme kila Mbunge achukue *fire extinguisher* aweke chumbani kwake, kweli itawezekana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba utitiri huu wa kodi unapelekea wafanyabiashara kuonekana mwisho wa mwaka akipiga hesabu hapati faida, anafunga duka lake. Tuelekeze nguvu zetu katika kuwasaidia wafanyabiashara ambao huwa wanaleta ajira kwa vijana wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ambayo siyo rasmi hususan ya Machinga pia wanakwamisha wafanyabiashara kufunga maduka yao Kariakoo. Mfanyabiashara analipa kodi ya takakata na asipokutwa na *dust been* analipa faini shilingi 50,000/=. Nje, Machinga hana *dust been* na hajui takataka zake anatupa wapi, anauza bila risiti. Ile kauli mbiu ukiuza toa risiti na ukinunua dai risiti, ni kwa baadhi ya wafanyabiashara, lakini sio wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi, sekta isiyo rasmi isajiliwe, watu waweze kulipa mapato na kila mtu kama ni haki wote wafanye biashara kwa haki na walipe kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *tendency* ya watu watu wetu wa Tanzania wanaona biashara zinazouzwa barabarani ni rahisi kuliko za madukani. Kwa hiyo,

wafanyabiasha wanakwazika, hawapati faida katika maduka yao, mwisho wa mwaka umemkadiria mapato makubwa, hajui atalipaje, ndiyo maana maduka yanafungwa. Kwa hiyo, naomba irekebishwe, mtu apewe *grace period* at least miezi mitatu kisha ndiyo wanamkadiria. Mapato, maana yake amepata. Mtu hajaanza kuweka bidhaa unamkadiria mapato, ameuza nini? (*Makofi*)

Waheshimiwa kuna kodi nyingine ambazo kwa kweli zinasikitisha sana. Nitazungumzia tozo ambazo zinatozwa marehemu kwenye hospitali zetu. Mtu amefiwa na ndugu yake, amemuuguza kwa gharama kubwa, anaenda kulipa matibabu pale na yuko *mortuary*. Akifika *mortuary* tena anambiwa marehemu kalala siku tatu, Sh.60,000/=. Pale siyo *guest*. Yule ni Mtanzania, alikuwa analipa kodi wakati wa uhai wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, katika tozo alizozifuta naomba afute na tozo za maiti katika hospitali zetu. Tufatufe sehemu nyingine ya kukusanya kodi lakini siyo kwa maiti, tuwaonee huruma wafiwa na marehemu wenyewe ambao wameshatangulia mbele ya haki na wakati wa uhai wao walikuwa wanalipa kodi kama Watanzania wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia pia suala la viwanda. Tuna viwanda vingi takriban 53,050 katika nchi yetu na kuna viwanda 3,306 ambavyo vinafanya kazi. Naishauri Serikali, kwanza tuanze na vile viwanda vikubwa vilivyobinafsishwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Lukuvi hapa kaona kuna watu walimilishwa mashamba wakashindwa kuyaendeleza, wakafutiwa hati zao. Sasa twende kwenye viwanda pia; viwanda vingi vilikuwepo na wawekezaji wameshindwa kuviendaendeleza. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati wanatafuta mapori ya kufyeka na kutengeneza viwanda vipya, tuanze kwanza na viwanda vya zamani, tuvifufue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitolea mfano hapa Mkoa wa Morogoro, kuna takriban viwanda vingi. Mwaka 1985

Morogoro ukifika ilikuwa unapata ajira, lakini nyumba hupati. Kulikuwa kuna kiwanda cha *Canvas*, *Ceramics*, *Moproco*, *Magunia*, *Tanneries*, *Morogoro Shoes*, *Polyester*; viwanda ni vingi zaidi ya kumi. Kuna Sukari Kilombero na Sukari Mtibwa. Vivanda vile tuvifuatilie. Viko zaidi za kumi na ajira zake siyo watu wawili watatu, vinaajiri watu wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati tunatafuta mapori ya kujenga viwanda, naishauri Serikali ipitie viwanda vyote vile vya zamani ambavyo hawaviendelezwi; kuna viwanda vya mafuta Moprocce, tulikuwa tunapata mafuta mazuri sana, lakini sasa hivi uzalishaji wake ni wa kususua. Tuvifuatilie tuone kama wale wawekezaji wameshindwa kuviendeleza tuvichukue ili tuwape wawekezaji wengine kuliko kuhangaika sasa hivi wananchi hawana ajira, viwanda vikubwa unaambiwa kiwanda kinahitaji watu wanne watano. Halwezekani hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombeni sana wakati tunatafuta mchakato wa kukata mapori, tuangalie viwanda. Tanga kulikuwa na Kiwanda cha Mbolea, kimekuwa. Sasa hivi wanaweka *depotya* mafuta. Kiwanda cha Mbolea kilikuwa kinasaidia wakulima wetu, naomba sana Waheshimiwa kila mkoaa unajua kabisa Tanga kuna wakulima wa matunda. Tuanzishe viwanda vya matunda ili wakulima nao wapate sehemu ya kuuzia bidhaa zao. Tuanzishe viwanda ambavyo malighafi zake zinapatikana hapa hapa Tanzania kuwezesha wakulima wetu kulima na kwenda kuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natolea mfano *General Tyre*. Kiwanda hiki malighafi zake zinapatikana mikoa miwili tu; mpira unapatikana Tanga na Morogoro, lakini mashamba yake pia yana mgogoro mpaka sasa hivi. Ndiyo maana mwekezaji anashindwa kufanya uzalishaji. Kwa hiyo, nashauri kwa kuwa ardhi ya Tanga na Morogoro iko katika mikoa mingine, tuhamasishe wakulima wetu, tuwape mikopo Serikali isimamie hili ili mikoa mingine ilime kilimo cha mpira ili kuweza kupata malighafi katika kiwanda chetu cha *General Tyre*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia pia mambo ya miundombini. Madaraja yote Tanzania watu wanapita bure, lakini daraja la Kigamboni kuna tozo, watu wanatozwa pale. Wanatozwa kwa sababu *NSSF* pia imeshiriki ujenzi wa daraja lile. Sasa naishauri Serikali, ni muda mrefu sana sasa lile daraja watu hata ukiwaelezea wanaona limekaa kibashara zaidi. Walielewa na matarajio ya wananchi wengi ni kwamba Daraja la kigamboni litakuwa kama ilivyokuwa Ruvu, daraja la Mkapa na Daraja la Kilombero watavuka bure. Sasa liko kibashara zaidi, linawakwaza wananchi wa Mkoa Dar es Salaam hususan Wilaya mpya ya Kigamboni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa huruma yake, najua kuna deni kubwa *NSSF* wanadai, lakini tuwasaidie watu wa Kigamboni. Kama ni kulipa hilo deni, basi madaraja ya Mkapa na Kilombero nayo yatozwe ili kusaidia daraja la Kigamboni nao watu wapite bure kama madaraja mengine. Kwa sababu inaonekana sasa lile halifanyiwi *service*, ni daraja kama madaraja mengine. Pale linaonekana liko kibashara zaidi, hata ukipita, utakuta Polisi wana *SMG* wanalinda yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie, hii huduma tunayoitoa kwa wananchi wetu iwe sawa na huduma katika mikoa mingine. Najua *NSSF* wanadai, lakini watafute mbini ambayo itasaidia sasa wananchi wa Kigamboni nao wapate faraja katika daraja lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Tanga. Nikinunua bidhaa kutoka Kariakoo nikipeleka kwetu Bumbuli nalipia tu usafiri, silipii chochote. Sasa Tanzania ni Muungano, ni nchi moja, angalau hata nikitoka Zanzibar, nikiingia Dar es Salaam, basi ushuru mdogo mdogo hata kama ni zawadi tuachiwe. Maana ukifika pale inaonekana ni nchi mbili tofauti, unadaiwa ushuru. Tufanye kama ninavyotoka hapa Tanga kwenda zangu Dar es Salaam nikiwa na bidhaa hata kama ni zawadi nilipie tu katika chombo cha usafiri, lakini siyo kulipia ushuru kama ilivyokuwa sasa na kuwapa nafuu ndugu zetu Wazanzibari na wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Zainab Mndolwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha na baadaye Mheshimiwa Abdallah Chikota ajiandae.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: *Bismillah Rahmani Rahim.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanhah Wataalaah* naomba nianze kuchangia hotuba hizi mbili, hotuba inayozungumzia Hali ya Uchumi wa Taifa na Mpango pamoja na Bajeti ya Serikali kwa kuanza na maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waingereza wanasema: “*an old is wise, the more it hears, the less it speaks.*” Waswahili wanasema kwamba, ndege huyu anayeitwa bundi ni ndege ambaye ana busara sana, lakini ukisikia bundi anazungumza, basi ujue kuna uchuro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza nitaongea maneno mazito kwenye Bunge hili katika hotuba hizi mbili ambapo sijawahi kuzungumza ambayo ni maagizo ya Wanamtware. Jambo la kwanza, ili nchi yoyote iweze kuendelea, lazima kuwe na hali ya amani na utulivu. Hali ya amani inatengenezwa na Serikali iliyoko madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeduwa nazungumza ndani ya Bunge hili kwa muda mrefu sana, kwamba Serikali kwa mwaka 2012/2013, ilitengeneza mazingira ambayo hivi sasa nami nimechaguliwa kama Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini, ambalo ni Jimbo mama Kanda ya Kusini na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mikoa ya Kusini wana majumba ama wana viwanja vyao Jimbo la Mtwara Mjini. Hii inadhihirisha kwamba Mtwara Mjini ndiyo Jimbo mama Kanda ya Kusini. Wananchi wakanichagua mimi Maftaha

Nachuma kuwa Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini, nije kuwakilisha kero za wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya kwanza ambayo walinipa wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini ni kuja kuzungumza ndani ya Bunge hili kuiambia Serikali iliyoko madarakani suala zima la maslahi ya gesi. Jambo la pili, ambalo walinituma wananchi wananchi wa Mtwara kuja kuzungumza ndani ya Bunge hili, kufikisha kilio chao, ni suala zima la migogoro ya ardhi ambayo Serikali ya Awamu ya Nne na Serikali zilizopita huko nyuma zilidhulumu wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini kwa kiasi kikubwa sana. Hali ilikuwa ni tete kweli kweli, wananchi wakanituma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa kwanza mkubwa ni mgogoro amba Serikali illichukua maeneo mwaka 2012/2013. Maeneo ya wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini, panaitwa Mji mwema, Serikali iliahidi kulipa fidia. Eneo la Mji Mwema, limekuwa linazungumzwa suala hili, nimeleta swali siku ya pili, baada ya kufika Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wakati anaomba kura Mtwara Mjini, alielezwa kero hii na wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini. Mwaka 2017 alipokuja Mtwara alielezwa jambo hili na wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini pale kwenye Uwanja wa Mashujaa. Nikazungumza ndani ya Bunge hili zaidi ya mara tatu. Nimefikisha, nikapewa *Hansard* mbili ndani ya Bunge hili, kwamba Serikali iko tayari kulipa fidia ya wananchi hawa, wananchi 2,200. Hapa naomba nilithibitiishie Bunge hili, kwa sababu hili limekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezuia maandamano zaidi ya mara 10, wananchi wanataka kuandamana kwa sababu wamechukuliwa maeneo yao, wakaambiya wasiyaeendeleze. Nilipewa *Hansard* hapa na Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwamba wanaenda kulipa. Mwisho wa siku

wanakuja ndani ya Bunge hili, wanasema hatuwezi tena kulipa kama Serikali. Nikiuliza upande wa pili naambiya, Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango hataki kupeleka fedha kuititia Taasisi ya *UTTPIID* ambayo ilichukua maeneo haya ya Jimbo la Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme Wanamtware wanisikie. Kilio chao walichoniagiza nije kueleza ndani ya Bunge hili, wakaandamana kwa kiasi kikubwa ili niweze kutangazwa tarehe 26, nilivyoshinda zaidi ya vyama vitano pale Mtwara Mjini. Naomba nisome hii *Hansard* na Mwenyezi Mungu aweze kunishuhudia leo kwamba leo kilio cha Wanamtware nimeflikisha kwa mara nyiningine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Hansard* ya mwaka 2017 anasema: "Mheshimiwa Spika, fidia stahiki itaanza kulipwa kwa wananchi 2020 kuanzia mwezi Juni, 2017 hadi robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/2018. Taasisi ya *UTTPIID* (narudia tena Taasisi ya *UTTPIID*) ambayo iko chini ya Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Halmashauri, inatarajia kutumia shilingi bilioni 7,523 kwa ajili ya malipo ya fidia kabla ya kuanza kwa kazi ya upimaji wa viwanja. Ofisi ya Rais TAMISEMI, ilitoa kibali cha kuendelea na utekelezaji wa mradi kuititia barua yenye kumbukumbu Namba GB203/234/01/117 ya tarehe 2 Septemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ulipaji wa fidia haukuanza mapema kutokana na Kampuni husika ya *UTTPIID*, kutokuwa na Bodi. Bodi imeshaundwa na makubaliano ya pamoja yamefanyika katika Kikao cha tarehe 2 Mei, 2017 baina ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, *UTTPIID*na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina *Hansard* mbili ndani ya Bunge hili, Serikali ikiahidi kulipa fidia hizi pesa, shilingi bilioni saba kwa wananchi hawa wa Jimbo la Mtwara Mjini. Katika Mtaa wa Mji Mwema. Jambo hili limekuwa tete sana Mtwara. Nimezuia maandamano zaidi ya 10. Narudia tena, sasa nazungumza ndani ya hili Bunge lako Tukufu, safari hii

nikiondoka hapa kwenda kwenye Jimbo la Mtwara Mjini, kwa sababu wananchi wamenituma kwa mara nyingine tena, naenda kutangaza maandamano makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maandamano hayo, aje kuyapokea Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu kaambiwa maneno haya ndani ya Jimbo la Mtwara Mjini zaidi ya mara mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo wamenituma wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini nizungumze hapa, ni suala hili, wenzangu wamezungumza; suala la pesa za korosho ambazo zilikusanywa, kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha korosho Mtwara na maeneo mengine. Kwa sababu Jimbo la Mtwara Mjini pia nina *AMCOS* zaidi ya mbili pale; nina *AMCOS* ya Mikindani na ya Naliendele. Zimekusanywa pesa za *Export Levy*. Pesa zilizokusanywa ni zaidi ya shilingi bilioni 210 ambazo zilitakiwa ziende kununua *sulphur* kuendeleza kilimo cha korosho. Zile pesa hazijaletwa Kusini kwa ajili ya kuendeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana sana na hoja na mwelekeo wa Serikali hivi sasa, kwa sababu nchi zote zilizoendelea duniani walikuwa na sera tunasema, *Strong State Intervention*, kwamba lazima Serikali iwe na meno katika kusimamia uchumi. Napongeza hilo kwa sababu Serikali dira yake ni hiyo. Wenzangu wamezungumza kwamba tunahitaji kuwa *decentralization* sasa hivi inakufa, hapana. Ili nchi iweze kuendelea, lazima kuwe na *Strong State Intervention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kununua ndege ambazo zinaenda kuchochaea Utalii hivi sasa Tanzania nzima. Ndege ni kielelezo kwamba ili nchi iweze kuendelea wageni waweze kuja ndani ya nchi kuleta pesa za kigeni, lazima tuwe na usafiri. Katika hilo niwashauri sana kwamba lazima tutoke na sisi kwenda kujenga mahusiano nje ya nchi ili tuweze kushawishi wawekezaji, kama Wabunge, kama Serikali, kama wananchi, Watanzania waweze kuja kuwekeza Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayazungumza haya kwamba zile fedha za korosho ambazo Serikali ilikusanya shilingi bilioni 210 tunaomba zirudi. Mheshimiwa Dkt. Mpango, kazungumza hapa kwamba mwaka huu anapendekeza sheria kwamba pesa zote zinazokusanya kupitia Bodi za Mazao zipelekwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali, zikusanywe na *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema sheria haiendi *retrospective*. Sheria hairudi nyuma. Zile pesa zilikusanya kabla ya hii sheria, shilingi bilioni 210. Wananchi wa Mikoa ya Kusini, Mtwara na Lindi ambao ndio walimaji wakubwa wa korosho, mwaka huu wamekosa *sulphur* sababu hizi pesa hazijaenda. Wanasema katufikishie kilio hiki Mbunge wetu, kwamba tunataka zile pesa ziweze kuletwa ziendeleze hata kwa mwakani. Vinginevyo watafanya maandamano makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza maneno haya, sijawahi kuzungumza ndani ya Bunge hili. Hiki ni kilio cha wananchi wa Kusini, ni kilio cha wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini. Nimekuwa natumia busara nyingi sana, kila mtu anafahamu ndani ya Bunge hili kwamba ukisikia maandamano yameanza Kusini, yameanzia Mtwara Mjini. Nimekuwa natumia busara nyingi sana kuongea na vyombo vyaa Serikali, kuongea na vyombo vyaa Dola na kuwashawishi wananchi kuleta amani na utulivu ndani ya Majimbo ya Kusini kwa kuanzia na Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili namwomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, amekuwa hajibu maswali yangu, amekuwa hajibu hoja zangu; nimezungumza maneno haya wakati amewasilisha Bajeti yake, hakujibu hata moja. Hajajibu hata hoja moja na anazungumza kwamba ni maneno ya wananchi wa Mtwara. Mheshimiwa Dkt. Mpango amekuwa hajibu hoja za wananchi wa Mtwara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ananisikia

ninavyozungumza maneno haya, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aje kupokea maandamano makubwa kwa wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini na Mikoa ya Kusini kwa kupokwa haki zetu hizi. Wananchi hawawezi kuchukuliwa maeneo zaidi ya miaka mitano mpaka hivi sasa hawajalipwa fidia zao na wala Serikali haisemi chochote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sana Mheshimiwa Dkt. Mpango atakapokuja kuhitimisha hoja yake, mwaka 2017 niliunga mkono Bajeti hapa, nikasema ndiyo. Kama hatatoa hizi pesa shilingi bilioni nane hata kwa kunyang'anya, kwa kukopa na kufanyaje, waleteni. Wachukue kwenye korosho walipe wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini, yale maeneo ya Mji Mwema, wanalamika sana, wameambiwa kwamba eti wapimiwe tena viwanja, wamechukuliwa zaidi ya miaka mitano, halafu virudi tena. Haiwezekani, huku ni kuwadharau wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

WAZIRI YA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza mchangiaji, kataja neno "maandamano," nataka tu akumbuke kibali cha maandamano. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ameshakusikia Mheshimiwa Maftaha. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyopo mezani kwetu. Nianze kwa kuwapongeza viongozi wa Wizara hii; Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri ambayo

wameifanya hadi wakaja na Kitabu cha Bajeti. Mchango wangu utajikita kwenye Sekta ya Kilimo na itajikita sana kwenye zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuongea sasa hivi, amezungumzia *Export Levy* na Mheshimiwa Bundala muda fulani alizungumzia *Export Levy*. Nami nitaendeleza hapo hapo, kwamba kwa miaka mitatu mfululizo, tumeona Serikali ikiufanya uwekezaji mkubwa sana kwenye zao la korosho, kwa hili naipongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilianza kutoa tozo ikaweka matumizi sahihi ya fedha ya Serikali kwenye Mfuko wa Zao la Korosho na Bodi ya Korosho na hata kufikia hatua ya kuvunja Bodi ya Korosho. Mwisho ikatolewa *incentive* kwa wakulima, mwaka 2017 zikatolewa pembejeo ambazo wakulima walipewa bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji huo ulifanya uzalishaji wa korosho uwe *double*. Kwa sababu uzalishaji wa korosho nchini, mwaka 2015/2016 ilikuwa tani 155,000. Mwaka 2017 ilikuwa tani 315,000, kwa uwekezaji mdogo tu huo. Nasikitika sana kwamba kinachoendelea mwaka huu ni kudhoofisha Sekta ya Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianza majadiliano na Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakumbuka, tulienda ofisini kwake kama Wabunge wa Mkoa wa Mtwara na Lindi wanaozalisha zao la korosho, kuhusu upatikanaji wa fedha za pembejeo. Alitujibu vizuri tu kwamba kuna kasoro kwenye ile sheria, kwa sababu Sheria ya Korosho ilisema fedha hizi zitatumwiwa baada ya kutengenezwa kanuni. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alitengeneza kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake sasa, tunaona ukurasa wa 69 kwamba Serikali inadhamiria kwamba ile Sheria ya Tasnia ya Korosho ambayo ilikuwa inakusanya korosho, asilimia 35 zinakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na asilimia 65 zinakwenda kwenye

uendelezaji wa zao la korosho. Sasa inakusudiwa kufutwa na nimechungulia kwenye *Finance Bill* ipo, inafutwa ili fedha zote ziingie kwenye Mfuko Mkuu. Hapa tunaua korosho. Hapo wanafanya siasa ya Mikoa ya Mtwara na Lindi iwe ngumu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hili tuungane. Kwa taarifa ya Kituo cha Utafiti Naliendele sasa hivi, wamejikita kwenye Mikoa 17. Kwa hiyo, wale wenzangu wa Chunya, Singida na Tabora, fedha hii ikiondoka hawatawaona wataalam wa Naliendele wanakwenda kwao kwa ajili kuliendeleza zao la korosho. Kwa hiyo, tuungane ili fedha hizi zirejeshwe, Kituo cha Utafiti Naliendele kifanye kazi yake, nao wazalishaji wapya wa korosho wapate hayo matunda ambayo yameonekana kwenye zao la korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye hili kuna changamoto nyangi sana, kwa sababu madhara yake, kama nilivyosema kwanza, sasa hivi hakuna kinachoendelea kwenye *sulphur*. Inasikitisha sana, mwaka 2017 Serikali ililetatani 28,000 hazikutosha, lakini mwaka huu tuliambiwa kwamba zimetolewa shilingi bilioni 10 kupelekwa *TFC* ili waagize pembejeo ya *sulphur*, hakuna hata kilo 50 ambayo imeeingia sasa hivi nichini. Shilingi milioni kumi hizi zimekuwa dana dana. Kwa hiyo, mwaka huu wakulima wamechanganyikiwa kuhusu *sulphur*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, fedha hizi zingetumika kulipa vikundi vidogo vidogo vya wazalishaji wa miche ya mikorosho. Kwa bahati mbaya sana wakulima hawa au vikundi hivi walishazalisha hiyo miche, miche imeshachukuliwa kwa wakulima, hawajapewa hata shilingi. Kwa hiyo, Mbunge ukionekana kule unazunguka zunguka wanakwambia Mbunge fedha zetu tulizotumia kuzalisha miche ya mikorosho bado hazijatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli ambayo itaenda kuua kabisa tasnia ya korosho ni kwamba asilimia ya fedha hizi ziliikuwa zinakwenda Kituo cha Utafiti Naliendele kwa ajili ya utafiti wa zao la korosho. Kule hali ni mbaya. Tulikutana

na wataalam wanasema kule hakuna kinachoendelea. Madhara ya kwanza ni upungufu wa mbegu za korosho. Mbegu za korosho lilikuwa jukumu la Kituo cha Utafiti Naliendele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoondoaa fedha hizi na wao wamesimamisha uzalishaji wa mbegu za korosho. Kwa sababu kuna mikoa mipyaa 17 ambayo imeingia kwenye uzalishaji wa korosho, mahitaji yao wao ni tani 165 za korosho. Kwa hiyo, mwaka huu hizo hazitaingia kwenye tasnia ya korosho. Madhara ya pili ni kwamba watashindwa kuendeleza kilimo cha korosho kwenye maeneo mapya. Kama niliyyosema, Chunya, Kyela, Singida na Tabora, walishaanza uzalishaji. Kwa hiyo, wale hawataawaona tena wataalam kutoka Naliendele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maskitiko yetu makubwa ni kupotea kwa ajira. Kituo cha Utafiti Naliendele lilikuwa kinatumia sehemu ya fedha hizi kwa ajili ya ajira ya watumishi wa pale, takriban watumishi 77 watapoteza ajira na kituo kile sasa hivi kuna ajira za kudumu watumishi wawili tu, madereva. Kwa hiyo, fedha hii inapokosekana, Kituo cha Utafiti cha Naliendele kitapoteza watumishi 77 na kitabaki na madereva wawili tu. Hebu angalia tasnia ya korosho inavyoteketea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango asiingie kwenye kumbukumbu mbaya kuua zao la korosho katika nchi yetu. Hebu naomba tutafakari hili turejeshe. Naelewa kwamba lengo lake ni kufanya matumizi mazuri ya fedha hizi, tusimamie, kama udhaifu ni Watendaji wa Bodi ya Korosho, tuwajibishe, lakini siyo kuchukua fedha shilingi bilioni 211 ambazo zingeingia katika kuendeleza zao la korosho na kuzipeleka kwenye Mfuko Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili ni kuhusu *produce cess*, ushuru ambao Halmashauri au mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatakiwa kulipwa. Sheria inasema kwamba wapewe 3% ya *farm gate price*. Kumekuwa na upotoshwaji

wa sheria hii unaofanywa na Wizara ya Kilimo na Bodi ya Korosho. Wanachaji 3% kwa bei dira, siyo sahihi. Kwa 3% inatakiwa iwe bei ya mnadani, ndiyo ushuru ambaao unatakiwa uende Halmashauri na mlipaji sio mkulima, ni mnunuzi wa korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye marekebisho hayo, tusimamie vizuri. Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imefika mpaka Mahakamani. Kwanza ilienda kuomba ushauri Ofisi ya AG Mtwara. Ofisi ya AG Mtwara ikajibu vizuri kabisa kwamba *definition ya Farm Gate Price* ni bei ya mnadani na siyo bei dira. Kwa hiyo, naomba hii wakati wa kufanya majumuisho, Mheshimiwa Waziri na hususan Waziri wa Kilimo, aiagize Bodi ya Korosho kwa sababu kila msimu huwa anatoa mwongozo; aiagize Bodi ya Korosho msimu ujao watoze ushuru wa Halmashauri kwa bei na mnadani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha zinazoenda kwenye Halmashauri siyo sadaka, zinatumika kwa ajili ya Maendeleo ya Halmashauri zetu. Halmashauri zetu vyanzo vingi tumewanyang'anya. Wamebaki na *produce cess* tu. Sasa walipwe kile wanachostahili na siyo 3% ya bei dira, iwe 3% ya bei ya mnada. Hii inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aiagize Bodi ya Korosho isi-*charge* hii 3% kwa mkulima, sheria iko wazi kabisa. Anayelipa *produce cess* ni mnunuzi (*buyer*). Mkulima akifika sokoni, hatakiwi kuchajiwa hiyo *produce cess*, anayetakiwa kulipa ni mnunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Chikota, mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Saada Mkuya.

MHE. SAADA M. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Serikali. Kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri

wa Fedha na Mipango pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *truly speaking* ni kwamba *this time* hii bajeti ni *very innovative* kwa sababu ya *measures* zake za kodi na naamini kwamba kwa vitendo kabisa tunakwenda kutekeleza ile azma ya *East African Community Budget* ya *Industrilization for job creation* na *shared prosperity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo machache ambayo nataka kuchangia. Kwanza ni kuhusiana na madeni ya *VAT* na *Excise* ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaidai Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bahati nzuri leo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imesoma Bajeti yake ya Serikali na inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trillioni 1.315. Kwa hiyo, kati ya mapato hayo ni pamoja na mapato ya *VAT* na *Excise* ambayo yanakusanywa na *TRA* kupitia *TRA* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania upande huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado kuna deni na Mheshimiwa Waziri nadhani analitambua. Kwa hiyo, tusaidiwe ili kule na kwenyewe maendeleo yaweze kutekelezwa. Kuna shida za maji, barabara; na tunaraji sana wakati tunaingia katika bajeti mpya, bado hizi fedha hazijapelekwa, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri hili alifanyie uharaka kwa ajili ya kwenda kukamilisha bajeti kwa SMZ. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusiana na tozo la *VAT* kwa upande wa ununuzi wa umeme. Tumezungumza sana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na hili safari hii tumelizingumza lakini limekuwa linakwenda mwaka kwenda mwaka kurudi, limezungumzwa sana na watendaji. Wakati *ZECO* inanunua umeme kama ni *essential supply*, kwamba inatozwa na *VAT* na *ZECO* anakwenda kuuza Zanzibar mwananchi wa Zanzibar ananunua umeme ukiwa na *VAT*. Kwa maana hiyo, isingekuwa *ZECO* kwa sababu tu sasa hivi imesema inasubiri hailipi, hailipi Zanzibar, hailipi

Tanzania kwa sababu ya huu mkanganyiko. Hata hivyo *ZECO* siyo mtumiaji wa mwisho. Kwa hiyo, kutokana na *principle* ya utozaji wa *VAT*, mlaji wa mwisho ndio anakwenda kutozwa *VAT*. Kwa maana hii ni mwananchi wa Zanzibar ambaye anatumia umeme ndiye ambaye analipa...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mhemishiwa Saada endelea.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mattar, naomba ukae chini.

MHE. SAADA M. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi wa Zanzibar ndiye ambaye analipa *VAT*. Sasa inakuwa haiwezekani *VAT* yenyewe pia *ZECO* ambaye ananunua umeme kwa ajili ya kwenda ku-supply kule na yenyewe itozwe *VAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nishati, nimependa siku ambayo anakamilisha bajeti yake, alisema vizuri sana kwamba nishati ama umeme ni siasa; umeme ni uchumi na umeme ni usalama. Amezungumza vizuri sana Mheshimiwa Waziri, lakini sasa hii isi-*apply* upande mmoja. Tunaomba nishati hii ama huduma hii muhimu iende vile vile isimamiwe kule na wananchi wa kule waweze nao kuendelea na uchumi wao kuweza kusimamia siasa pamoja na usalama uliopo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana kuitia *Finance Bill* Mheshimiwa Waziri wa Fedha lilekebishwe, *ZECO* asinunue umeme *TANESCO* ikiwa ni pamoja na *VAT*. Hili ni jambo ambalo linaweza likarekebishwa, maana yake imekuwa tabu miaka nenda, miaka rudi, lakini ni jambo ambalo tunaweza kulirekebisha kuitia *Finance Bill*. Kwa maana hiyo sasa, badala ya kupunguza hizi kero za Muungano, tunaongeza kero za Muungano kwa sababu tu ya masuala ya *administration*. Tunaomba na hili lizingatiwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna baadhi ya taasisi ambazo ni za Muungano ambazo zina-*operate* Zanzibar, haziliipi umeme *ZECO*, zinalipa umeme *TANESCO*. Wanachukua umeme wa *ZECO*, lakini malipo yanalipwa *TANESCO*. Nadhani hii haiko sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hili na lenyewe, lile deni ambalo lipo kutohana na huduma hii lilipwe, lakini usimamizi uwe mzuri zaidi. Taasisi za Muungano ambazo zina-*operate* Zanzibar zilipe umeme Zanzibar, umeme ndiko ambako unakotolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa haraka haraka nimefurahi sana kuona sasa *DCF* imekamilika na tutakwenda kutekeleza. Nimefurahi kwa sababu Zanzibar wameshiriki kikamilifu katika *development* mpaka *development* ya *Action Plan* ya *DCF*. Hili napata *experience* nzuri kwa sababu mimi mwenyewe wakati niko Wizara ya Fedha Zanzibar, nilishiriki katika *development* ya *Joint Assistance Strategy for Tanzania*. Utekelezaji wake ulikuwa ulikuwa ni shida kubwa. Shida kubwa ilikuwa inapatikana pale ambapo tupolikuwa tukizungumza hii mikakati miwili, wakati huo kulikuwa kuna MKUKUTA na MKUZA, tuweze *ku-harmonize* ili twende kwa pamoja tukatafute misaada ya Kibajeti. Haikuwezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa hivi hii *DCF*, tumei-*develop* vizuri, tume-*develop* sote, tunashukuru sana kwa ushirikiano uliokuwepo lakini *implementation* yake iwe ni ya kuweza kuhakikisha kwamba hizi *strategies* zetu zinakuwa *harmonized* na kwa maana hiyo tunapokwenda kutafuta misaada iwe tunakwenda pamoja, yaani pamoja na *inclusion* ya Zanzibar, isiwe tunakwenda *separate*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya kwenda *separate* maana yake nini? Maana yake Mheshimiwa Dkt. Mpango tumeweka safari hii *GBSkwamba* tuna kiasi cha fedha shilingi bilioni 545. Leo Zanzibar wanasoma bajeti yao, wamesema wao hawawezi kuingiza hii *GBS* kwa sababu hii ni fedha ambayo kwanza haina uhakika. Sasa Mheshimiwa Dkt.

Mpango, naomba atakapokuja kujibu hoja aliweke suala la jinsi gani Zanzibar itaweza kushiriki katika ku-mobilize external resources kupitia *General Budget Support* na DCF ili na yenye we ipate uhakika wa mapato yake ya kibajeti. Hoja zipo nydingi, lakini tunaomba kwa umuhimu wa pekee hili alipe nafasi aweze kulijibu katika hoja zake. (*Makofj*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la kiutawala zaidi, Zanzibar leo wakati inasoma bajeti; nadhani sisi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumesoma tokea Alhamisi, lakini ilivyo Zanzibar, yaani ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tungeweza kusoma bajeti kama vile tulivyokubaliana katika *East Africa*. Kwa nini hatusomi? Sababu zinaweza zikawa nydingi, lakini ninaloliona ni kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa vyanzo vya mapato kutokana na *tax measures* ambazo ziko katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linawezekana. *Tax Force* ya *Tax Reforms* tunaomba iwe ina-*include* Maafisa wa Kodi na wa Wizara ya Fedha ya Zanzibar. Sasa hivi kilichopo, Zanzibar inaalikwa ile siku moja kama ambavyo wanaalikwa wadau wengine wa nje. *SMZ* ni *part* ya SMT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wakati Maafisa wetu wanapoanza kubuni vyanzo vya mapato, wanapoanza ku-*develop tax measures* za mwaka wa fedha unaokuja *from day one*, Maafisa wa Kodi wa Zanzibar pamoja na Maafisa wa Sera za kikodi wa Wizara ya Fedha na Mipango ya Zanzibar wawepo katika *tax measures*. Hii itasaidia sana kuwa na uhakika wa bajeti hata kule upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halihitaji mabadiliko ya sheria wala mabadiliko ya kisera linahitaji uamuzi wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ili hawa watu washiriki tuweze kuondoa huu mgongano wa kikodi na vilevile tutapunguza hizi changamoto za Muungano zinazojitokeza. Pia tutaweza kufanya masuala mbalimbali; kwa mfano,

Mheshimiwa Dkt. Mpango safari hii, tumeangalia vizuri, angalau *corporate tax* imepunguzwa. Maana yake nini? Zanzibar hajapunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Maana yake ni kwamba kama kutakuwa na viwanda vipyta vitakuwa *attracted*sana upande huu ambapo hii *corporate tax* imepunguzwa kuliko kule. Tungekuwa tumekaa pamoja mwanzo, tukashauriana, tukakubaliana, nadhani hizi *tax measures* zingekwenda vizuri. Kwa maana hiyo, *industrialization for job creation and shared prosperity* ingeweza hata ku-*apply* kwa upande ule mwingine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulipo sasa hivi tunapokwenda ndipo tunapoleta mkanganyiko na kwa maana hiyo, baadhi ya kodi haziwezi kutekelezeka, kwa sababu upande mmoja haujawa tayari *simply* kwa sababu haujapata muda mrefu wa kuweza *ku-mainstream* na *ku-think about* hizi *tax measures*. Kwa hiyo, hilo ni suala la *administration* zaidi na naamini kabisa Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa uelewa wake, weledi wake, nia yake njema na nzuri kabisa, hili atalifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi na la umuhimu kabla sijamaliza, tunaomba sana fedha ambayo ilikuwa iende Zanzibar, ipelekwe ifanyie maarifa haraka iende ikasaidie shughuli za kiuchumi Zanzibar. Vile vile masuala ya VAT, tuisubiri *consultant* kwa sababu ni jambo ambalo linawezekana likarekebishwa kuititia *Finance Bill* hii ambayo ya mwaka 2018/2019. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, sina zaidi, lakini naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Naibu wake na Menejimenti nzima ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya jambo hili la leo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Saada Mkuya kwa kutukamilishia shughuli zetu za leo.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa michango yote ya leo, naamini Mheshimiwa Mpango na Naibu Waziri wake wameyasikiliza vizuri na naamini yale yenye manufaa yote watayafanya kazi.

Baada ya kusema hayo, niseme tu naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku, Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamis,
Tarehe 21 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhji)*